




**TANI** 26 korosho zilizosindikwa zauzwa Uholanzi

UKURASA 9


Ukurasa 14

2022 mwaka usio na matukio makubwa Tanzania

Ukurasa 15

2022 mwaka Ndugai alipoandika historia ni kuwa Spika wa kwanza kuachia ngazi

Ukurasa 19

siasa

JUMATANO DESEMBA 28, 2022

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Uingereza ilivyobadili viongozi kama 'mswaki'

2022 ni mwaka wa wamachinga biashara zao mijini bado kitendawili

Na Nimi Mweta

UKURASA 13


# Nipashe

Jumatano Desemba 28, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581173

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# HUZUNI

**AJALI** zaua wanane familia mbili, sababu ni zile zile... *Endelea Uk.* 2 & 21



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Waziri Mkuu mstaafu, Dk. Salim Ahmed Salim (katikati), alipomtembelea nyumbani kwake, Oysterbay, Dar es Salaam, jana. Kushoto ni Ahmed Salim ambaye ni mtoto wa Dk. Salim. **PICHA: OWM**

## TMA yahadharisha mvua kubwa kwa mikoa minane

UKURASA 2

## Dk. Mwinyi asema watu, mabadiliko tabianchi tishio usalama chakula

UKURASA 3

**MICHEZO** HATIMAYE FEITOTO KUBAKIA JANGWANI UK. 32

**KATUNI** UK. 6




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, akizungunza kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), katika ufunguzi wa semina ya kujenga uelewa kwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakiwamo mawaziri, naibu mawaziri na makatibu wakuu wa SMZ kuhusu matumizi ya baiteknoloji ya kisasa. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

# Huzuni ajali zikiua wanane

**Na Elizabeth Zaya**

NI huzuni. Hivyo ndivyo ilivyo baada ya watu wa wanane wa familia mbili kufariki dunia papo hapo katika ajali mbili tofauti za barabarani zilizohusisha magari madogo na magari makubwa ya mafuta katika mikoa ya Morogoro na Mbeya.

Wakati ajali hizo zinatokea na kutekeleza maisha ya nguvu kazi ya taifa na wengine kujeruhiwa vibaya, sababu za matukio hayo ni zile zile ambazo zimekuwa zikiimbwa siku hadi siku; ulevi wa madereva, uendeshaji magari kwa mwendokasi na kuyapita magari mengine bila tahadhari tena kwenye kona.

Katika ajali ya kwanza. Watu watano wakiwamo mume na mke, wamefariki dunia papo hapo katika ajali iliyotokea eneo la Iyovi, Mikumi, wilayani Kilosa, Morogoro baada ya gari dogo aina ya Toyota Allion, walikuwamo wanandoa hao kugongana uso kwa uso na lori la mafuta.

Aidha, katika ajali ya pili iliyotokea Mbeya, baba na mwanawe ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha pili, wamefariki dunia papo hapo pamoja na mtumishi wa ndani huku wengine wakijeruhiwa.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa dereva aliyekuwa amelewa na kuendesha gari bila kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Katika ajali ya Mikumi, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Fortunatus Musilimu, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kueleza ilitokea usiku wa kuamkia juzi katika kona kali za Itovi, barabara ya Morogoro - Iringa.

SACP Musilimu alisema gari hilo dogo lenye namba IT 6954 DNN lilikuwa likitokea katika Bandari ya Dar es Salaam kwenda mpakani Tunduma mkoani Songwe, liligongana na lori la mafuta aina ya Mercedes Benz, lenye namba za usajili RAE 518 C na tela namba RL 2686 lililokuwa likitokea Iringa kwenda Morogoro.

Alisema gari dogo lilikuwa likiendeshwa na Festo Shoo wakati lori likiendeshwa na Muthoni Richard, raia wa Rwanda na kwamba dereva wa gari dogo ni miongoni mwa waliofariki dunia.

Kamanda Musilimu alitaja wengine waliofariki dunia kuwa ni Grayson Ng`obo mkazi wa Mbeya na Janeth Luvanda ambao ni mke na mume.

Wengine ni Oswald Luvanda, mkazi wa Mbeya na ndugu wa Janeth Luvanda na Davis Haule, mwalimu wa Shule ya Wanging`ombe iliyoko mkoani Njombe.

"Waliofariki (dunia) katika ajali hiyo ni watu watano wakiwamo wanaume wanne na mwanamke mmoja ambao walikuwa katika gari hilo dogo la IT," alisema Kamanda Musilimu.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa gari dogo ambaye alitaka kuyapita magari yaliyokuwa mbeye yake bila kuchukua tahadhari.

Kamanda Musilimu alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Mtakatifu Kizito, Mikumi mkoani Morogoro.

**WADAU WAPAZA SAUTI**

Baadhi ya wadau, wakizungumza na Nipashe, walitoa maoni kuhusu wimbi la matukio ya ajali wakisema magari yanayotolewa katika Bandari ya Dar es Salaam kupelekwa mpakani Tunduma kwa ajili ya kupelekwa nchi jirani, maarufu kama IT, si salama kwa kupanda abiria kwa kuwa madereva huendesha kwa mwendokasi bila kufuata sheria za usalama barabarani.

Peter Kanivalo alisema: "IT siyo magari ya kupanda, madereva wake huwa wanaendesha kwa kasi mpaka damu inasimama."

Ashraf Hamisi alisema serikali kupitia Jeshi la Polisi Usalama Barabarani inapaswa kuchukua hatua dhidi ya magari ya IT kwa sababu yamekuwa yakipata ajali mara kwa mara na kwamba hali hiyo ikiendelea kupuuzwa, watu wataendelea kupoteza maisha.

"Haya mambo ya kupanda gari za IT yatatumaliza sana. Gari hizo siyo za abiria ni gari ambazo huwa zinatolewa sehemu moja kupelekwa sehemu nyingine, maana yake hata bima inayokatiwa inahusu gari lenyewe na dereva peke yake na haiwahusu abiria waliopakizwa na kusafirishwa humo.

"Gari hizi husafirishwa na madereva ambao siyo lazima wawe wajuzi na njia wanayopita, wengi huendesha kwa kasi wakilenga kufika kituo cha kupumzika kabla ya usiku haujawa mwingi. Nadhani ipo haja sasa ya Kikosi cha Usalama Barabarani cha Jeshi la Polisi kuongeza elimu kwa madereva kuwa kusafiri safari ya mbali kunahitaji maandalizi, nidhamu na uzoefu.

"Wasikurupuke kuendesha kwenda mbali kama hawana uzoefu kwa sababu wanakuwa chanzo cha ajali nyingi," alisema.

Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Watanzania 886 wamepoteza maisha kati ya Januari na Novemba, mwaka huu, kutokana na ajali za barabarani, huku wengine 573 wakijeruhiwa kwenye ajali 1,422 zilizotokea.

*Habari zaidi UK. 21

## TMA yahadharisha mvua kubwa mikoa minane

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari ya mvua kubwa kwa baadhi ya maeneo nchini, hususan kwenye mikoa minane, ikiwamo Morogoro, Mbeya, Songwe, Rukwa, Singida, Dodoma, Lindi na Mtwara, inayotarajiwa kunyesha leo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mchambuzi wa Hali ya Hewa kutoka mamlaka hiyo, Joyce Makwata, alisema tahadhari inatolewa hususan kwa wananchi na wakazi waishio kwenye mikoa hiyo, kwa kuwa athari ya mvua inatarajiwa kuathiri shughuli za kiuchumi.

"TMA inatoa angalizo la uwapo wa vipindi vya mvua kubwa maeneo ambayo yatapata mvua, maeneo hayo nchini kwa siku ya kesho (leo) kuwa ni Kusini mwa Mkoa wa Morogoro, Ruvuma, Njombe na Rukwa.

"Athari za mvua matarajio ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji na hata miundombinu kuathirika, wananchi wachukue tahadhari na ucheleweshwaji wa shughuli za uchumi na usafirishaji," alisema Joyce.

Aidha, alisema jana, angalizo pia lilitolewa kwenye mikoa ya Ruvuma, Njombe, Iringa, Morogoro, Mbeya, Songwe, Rukwa, Singida, Dodoma, Lindi pamoja na Mtwara.

Septemba, mwaka huu, TMA, ilitoa utabiri wa msimu wa mvua za vuli 2022 kwa maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, huku Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. Agnes Kijazi, akisema maeneo ya nchi yatapata misimu miwili ya mvua za chini ya wastani.

"Kutokana na mifumo ya hali ya hewa ilivyo kwa sasa na inavyotarajiwa katika kipindi chote cha msimu, kwa ujumla mvua za chini ya wastani hadi wastani, zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.

"Msimu unatarajiwa kuanza kwa kuchelewa na kuambatana na mtawanyiko wa mvua usioridhisha. Vipindi virefu zaidi vya ukavu vinatarajiwa katika miezi ya Oktoba na Novemba 2022, hata hivyo vipindi vya ongezeko kidogo la mvua maeneo machache ni wiki ya tatu na ya nne kwa mwezi Desemba, 2022," alisema Dk. Kijazi ambaye ni Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO).

Alisema kwamba mvua za vuli huisha mwezi Desemba, pia kunatarajiwa kuwapo na mwendelezo wa mvua kwa mwezi Januari, 2023.

Vilevile Dk. Kijazi alisema kuna matarajio ya vipindi vya joto kali kuliko kawaida katika msimu wa vuli maeneo ya Kaskazini mwa Mkoa wa Morogoro, mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

# Hospitali Mkoa Iringa yalia uhaba wa damu

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Iringa inakabiliwa na upungufu wa damu salama katika benki yake wakati kila siku wastani wa chupa 20 zinahitajika kwa ajili ya kuwasaidia kinamama wanaojifungua ambao uhitaji wa damu kwao ni mkubwa.

Akizungumza na Nipashe ofisini kwake hivi karibuni, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Dk. Alfred Mwakalebela, alisema, kwa mwezi mahitaji ni uniti 300, hivyo tunawaomba wananchi wa mkoa wa Iringa na wilaya zake kujitokeza kuchangia damu.

Dk. Mwakalebela alisema mahitaji ya damu ni makubwa. Aidha, makundi yanayohitaji damu kwa sasa ni wajauzito ambao wana shida ya kupungukiwa damu wakati wa kijifungua, watoto na majeruhi wa ajali.

Pia aliongeza kuwa, uhaba huo unatokana na watu kutokuwa na mwamko wa kuchangia damu pindi inapohitajika.

Aidha, sababu nyingine ni kufungwa kwa shule na vyuo, ambapo wanafunzi husaidia kuwachangia damu kwa hiari.

Mahitaji ya damu salama, kwa mujibu wa Dk. Mwakalebela, ni kati ya chupa 20 na 25 kwa siku sawa na lita 20, lakini kutokana na uhaba huo, benki ya damu imesalia na chupa 20 za damu salama.

"Kuna jambo lingine linalochangia uhaba wa damu katika benki ya damu ni imani potofu kutoka kwa baadhi ya watu kwamba kuchangia damu kunasababisha mtu kuishiwa damu kabisa, hivyo kufanya watu wengi kutojitokeza kuchangia damu," alisema.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi wenye nguvu na afya bora kujijengea tabia ya kuchangia damu hata kwa mwaka mara moja ili kupunguza uhaba wa damu salama kwenye hospitali ya mkoa.

"Suala hili halina madhara na pia ni thawabu kwa Mungu kwa kuwa unaokoa maisha ya binadamu mwenzako ambaye labda kwa kukosa damu angeweza kufariki dunia," alisema Dk. Mwakalebela.

Dk. Mwakalebela aliwashauri wananchi kuzingatia milo kamili badala ya kupendelea vyakula vya wanga kama vile, chipsi ambavyo haviongezi damu.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa, Dk. Alfred Mwakalebela, akiongea na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu uhaba wa damu hivi karibuni. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Mwinyi: Idadi ya watu, mabadiliko tabianchi tishio usalama chakula

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema dunia imekabiliwa na tatizo la kutokujitosheleza kwa mahitaji ya chakula kutokana na ongezeko la watu na mabadiliko ya tabianchi ambayo yanaathiri uzalishaji.

Dk. Mwinyi ameyasema hayo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, katika ufunguzi wa semina ya kuwajengea uelewa kwa viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusu matumizi ya baioteknolojia ya kisasa katika ukumbi wa Sheikh Idris Abduliwakil, Kikwajuni, mjini Zanzibar.

Alisema idadi ya watu barani Afrika ikiwamo Tanzania na Zanzibar, inatarajiwa ongezeka maradufu ifikapo 2050. Hali hiyo, alisema itasababisha usalama wa chakula kuwa na changamoto kubwa iwapo hatua sahihi hazitachukuliwa.

Rais alisema matumizi ya baioteknoloji ya kisasa ni elimu inayowezesha kufanyika mabadiliko ya vijinasaba (DNA) kwa kuvumbua mambo mbalimbali katika nyanja za afya, uchumi wa bluu, kilimo, ufugaji, mazingira na bidhaa za viwandani.

Pia Dk. Mwinyi alisema baioteknolojia ya kisasa iwapo itatumika kwa usahihi na ufanisi, inaweza kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii kwa haraka kama ilivyofanyika katika upatikanaji wa chanjo ya UVIKO - 19 iliyopatikana kwa muda mfupi.

Sambamba na hayo, alisema katika afya baioteknolojia ya kisasa inatumika katika kuzalisha dawa na chanjo mbalimbali, kutambua magonjwa na kutengeneza vyakula vyenye virutubisho ili kukabiliana na matatizo ya utapiamlo.

Rais Mwinyi pia alisema teknolojia ya kisasa inaweza kutumika katika kusafisha mazingira hasa katika kuondoa mabaki ya sumu zinazotokana na taka za viwandani na kupunguza matumizi ya viuatilifu, hivyo kuchangia katika kutunza hifadhi ya mazingira na afya za binadamu na wanyama.

Aidha, alisema teknolojia hiyo ni muhimu katika maendeleo ya viwanda kwa uzalishaji wa bidhaa kama za nishati mbadala ya biogesi, kutengeneza vyakula vya mifugo, dawa za kusafishia vipodozi vya binadamu.

Akiwasililisha mada kuhusu Baioteknolojia ya Kisasa, Matumizi, Fursa, Faida na Changamoto zake, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Aly Mahadhy, alisema kwamba kuwapo kasi ya ongezeko la idadi ya watu, mabadiliko ya tabianchi na ardhi kuliwa na bahari kutasababisha kukosekana kwa eneo la kilimo na hivyo kusababisha uhaba mkubwa wa chakula.

Alibainisha kuwa kuwapo kwa magonjwa ya mazao ya kilimo kama vile mpunga, mhogo na migomba ambacho ni chakula muhimu kwa wananchi, kunahitajika juhudi kubwa za kiutafiti ili kuzalisha mbegu mbadala na vifaa tiba na chanjo za magonjwa mbalimbali kupitia teknolojia ya kisasa ili kukabiliana na hali hiyo.

Awali, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk. Omar Dadi Shajak, alisema mafunzo hayo ni muhimu katika kufanya tathmini ya masuala yanayohusu matumizi ya teknolojia ya kisasa na kusaidia Zanzibar katika uandaaji wa sera na sheria ili kuweka mwongozo sahihi wa matumizi ya teknolojia ya kisasa.

Semina hiyo ya siku moja imeandaliwa kwa pamoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Tume ya Mipango na kudhaminiwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) na kuwashirikisha Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu wakuu wa SMZ.


**SIMBA CEMENT**
STRENGTH WITHIN

**RESIGNATION OF THE CHAIRMAN OF THE BOARD**

**TANGA CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY (DSE: TCPLC)**
**(INCORPORATED IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA) ("TANGA" OR "THE COMPANY")**

Shareholders are advised that Tanga Cement PLC announced today that the Chairman of the Board, Mr. Lawrence Masha, has resigned from his position with effect from 15 December 2022 having spent nine years on the Board of the Company, to be able to commit to a new opportunity.

In line with the Company's succession plan, the Deputy Chairman, Mr Patrick Rutabanzibwa, has accepted the appointment as the new Chairman of the Board with effect of the same date.

The Board wishes to thank Mr Masha for the significant contribution he has made over the years to the Company.

**On behalf of the Board.**

**Patrick Rutabanzibwa**
**Chairman of the Board**
**22 December 2022**

17207502



Mwonekano wa daraja la waenda kwa miguu lililoko Mbezi Luis Dar es Salaam, inadaiwa baadhi ya watu hawalitumii badala yake wanalazimisha kupenya katika uzio kuvuka upande wa pili wa Barabara ya Morogoro, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yatia saini mkataba kuunganisha Bandari Ziwa Nyasa, barabara za lami

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI imeanza kuziunganisha bandari za Ziwa Nyasa, Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya na barabara za lami kwa kutia saini mkataba wa ujenzi wa barabara tatu zenye urefu wa kilometa 32 ili zijengwe kwa kiwango cha lami.

Jana Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), ulitia saini na mkandarasi wa Kampuni ya PS Group ya nchini Uturuki, mkataba wa kujenga barabara tatu zenye urefu wa kilomita 32 zinazounganisha bandari za Kiwira na Itungi.

Mkataba huo ulitiwa saini kati ya Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Rogatus Mativila na Meneja Mkuu wa Kampuni ya PS Group na kushuhudiwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa.

Mtendaji Mkuu wa TANROADS, Mhandisi Mativila, alizitaja barabara zinazojengwa kuwa ni ya Ibanda-Kanjunjumele yenye urefu wa kilomita 22, barabara ya Kanjunjumele-Kiwira Port, yenye urefu wa kilomita sita na Kanjunjumele-Itungi Port yenye urefu wa kilomita nne.

Alisema barabara hizo kwa pamoja zitajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 38.3 fedha zinazotokana na vyanzo vya ndani vya mapato.

Alisema barabara hizo zitasaidia kuiunganisha mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma kupitia bandari za Itungi, Kiwira na Mbamba Bay hasa kwa kusafirisha mazao ya chakula na biashara, madini na shughuli zingine za kijamii.

"Barabara hii pia itatusaidia kusafirisha mazao ya misitu na uvuvi, lakini ni kiungo muhimu cha barabara yetu ya Mbeya-Kasumulu ambayo inaunganisha nchi yetu na nchi za Malawi, Msumbiji, Zambia na Afrika Kusini," alisema Mativila.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo utakamilika katika kipindi cha miezi 36 ambayo miezi 24 ni kwa ajili ya ujenzi na miezi 12 ni kwa ajili ya uangalizi kabla ya kukabidhiana rasmi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema barabara hiyo ni muhimu kwa uchumi wa wananchi wa Wilaya ya Kyela kwa kuwa itasaidia kuwaunganisha Ziwa Nyasa ambalo lina uchumi mkubwa.

Alisema barabara hizo zitachochea ongezeko la mizigo itakayokuwa inasafirishwa kwa kutumia meli zilizojengwa na serikali ambazo kwa muda mrefu ufanisi wake ulikuwa mdogo kutokana na ubovu wa barabara.

Aliwataka wananchi wa Wilaya ya Kyela kutoa ushirikiano kwa mkandarasi ili barabara hizo zijengwe na kukamilika kwa wakati na wao waanze kunufaika.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoitoa kwa wananchi hao alipokuwa ziarani mwezi Agosti mwaka huu.

"Wananchi wa Kyela mna bahati kubwa, ukiacha barabara hii kuna serikali pia imeboresha barabara ya Kikusya-Ipinda Matema kwa kuweka taa katika Mji wa Ipinda kwa hiyo mwendelee kuipa serikali ushirikiano," alisema Homera.

Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Mlaghila, aliiomba serikali kutoa maagizo maalumu kwa mkandarasi wa mradi huo ili wakati wa ujenzi wa barabara hizo aajiri vijana wa Wilaya ya Kyela kwanza kabla ya kuwafikiria wa maeneo mengine.

Pia aliomba ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopitiwa na mradi huo ufanyike mapema kabla ya kuanza kujengwa kwa mradi huo ili kuepusha migogoro.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Mbarawa, aliagiza TANROADS kusimamia vizuri mradi huo ili kuhakikisha unatekelezwa kwa viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba ili barabara hiyo idumu kwa muda mrefu.

Aliwataka wananchi wanaoishi jirani na mradi huo kuhakikisha wanalinda vifaa vya ujenzi ili visiibiwe pamoja na kuilinda miundombinu ya barabara hiyo ili isihujumiwe.

# Mahakamani wakituhumiwa wizi wa mali za mil. 184.1/-

**Na Grace Gurisha**

WAKURUGENZI wawili wa Kampuni ya Japan Tanzania Tours Ltd., Hamis Mkomwa na Toshiaki Aizawa, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam wakikabiliwa na tuhuma za wizi wa mali zenye thamani ya Sh. milioni 184.1.

Akisoma hati ya mashtaka Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rhoda Ngimilanga, kuwa washtakiwa wanatuhumiwa kwa makosa manne.

Mafuru alidai kati ya Septemba, 2019 na Oktoba, 2020 washtakiwa wakiwa eneo la maktaba, Ilala, jijini Dar es Salaam, wanatuhumiwa kuiba vifaa mbalimbali vya ofisi zikiwamo kompyuta tatu zenye thamani ya Sh. milioni 38.8, mali ya kampuni hiyo walioaminiwa kuvitunza kama watumishi wa kampuni hiyo.

Alidai, Februari 28, 2019, katika ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ilala, Mkomwa aliiba gari aina ya Toyota Land Cruiser lenye thamani ya Sh. milioni 30.8 aliyoaminiwa kuitunza na kufanya uhamisho wa gari hilo kuwa lake kupitia kampuni yake ya Ada Car Hire Ltd.

Mafuru alidai kuwa Aprili 10, 2019, Mkomwa akiwa ofisi za TRA Kinondoni anatuhumiwa kuiba gari aina ya Toyota Rav4 lenye thamani ya Sh. milioni 28.5, mali ya kampuni hiyo aliyoaminiwa kuitunza kama mtumishi na badala yake akafanya uhamisho wa gari hilo kwenda kwa Edgar Maganga.

Pia Mkomwa anadaiwa Machi 14, 2019 akiwa katika ofisi za TRA Ilala, aliiba gari aina Nissan Pickup, yenye thamani ya Sh. 57.28 mali ya kampuni hiyo aliyoaminiwa kuitunza kama mfanyakazi na badala yake akaifanya uhamisho kwenda kwa Tatsuo Kasegawa.

Inadaiwa kuwa Aprili 10, 2019, Mkomwa akiwa TRA Kinondoni, Dar es Salaam aliiba Toyota Rav4 lenye thamani ya Sh. milioni 15, mali ya kampuni hiyo na kufanya uhamisho wa gari hilo kwenda kwa Invocavity Nkya.

Mafuru alidai kuwa Aprili 11, 2019, Mkomwa akiwa katika ofisi hizo aliiba Toyota Harrier lenye thamani ya Sh. milioni 14.527, mali ya kampuni hiyo na kufanya uhamisho wa umiliki wake kwenda kwenye Kampuni Genki Carent Car Rental.

Ilidaiwa kuwa, Septemba 10, 2019, katika benki ya Stanbic, mshtakiwa Mkomwa aliiba Dola za Marekani 8,100 za kampuni hiyo aliyoaminiwa kuitunza kama mfanyakazi na kuzihamishia katika akaunti yake ya Ada Car Hire Ltd ya CRDB.

Alidai kuwa mshtakiwa huyo anatuhumiwa pia kuiba Dola za Marekani 3,303 na Dola 5682.60 kutoka kampuni ya Japan Tanzania Tours Ltd na kuzihamishia kwenda kwenye akaunti ya Kampuni yake ya Ada Car Hire Ltd., ya CRDB.

Baada ya kusomwa mashtaka hayo, upande wa mashtaka ulidai kuwa upelelezi haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa na ilipangwa Januari 10, 2023.

Hata hivyo, washtakiwa hao walipelekwa mahabusu baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana, Mkomwa alitakiwa kuwasilisha fedha za taslimu Sh. milioni 218 au wadhamini wawili watakaowasilisha nusu ya kiasi hicho cha fedha au hati ya mali isiyohamishika ya kiasi hicho na wadhamini wawili.

Mshtakiwa wa pili kuwasilisha mahakamani hapo fedha taslimu Sh. milioni 16 au hati ya mali isiyohamishika ya kiasi hicho cha fedha na wadhamini wawili.

TANGAZO


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

# TAARIFA KWA UMMA

## MWALIKO WA KUSHIRIKI KATIKA MKUTANO WA WADAU WA KUKUSANYA MAONI KUHUSU MAOMBI YA NAULI MPYA ZA ABIRIA KWA MELI YA MV. RAFIKI 2

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limepokea kutoka Kampuni ya Usafiri Songoro Marine maombi ya nauli mpya za abiria kwa meli ya MV. Rafiki 2 ifanyayo safari kati ya Mwanza na Bukoba.

Kwa mujibu wa kifungu cha 29 (2) (b) cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415, TASAC imeandaa Mkutano wa wadau wa huduma ya usafiri majini jijini Mwanza ili kukusanya maoni ya wadau kuhusu maombi ya nauli yaliyowasilishwa na Kampuni ya Songoro Marine.

Shirika linawaalika wadau wote kushiriki katika mkutano huo utakaofanyika siku ya Alhamis, tarehe 5 Januari, 2023 katika ukumbi wa mikutano uliopo ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji - Mwanza kuanzia saa 4 kamili asubuhi.

Aidha, wadau wanaweza kutuma maoni kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe **tariff@tasac.go.tz** au kwa kufika katika ofisi za TASAC – Mwanza au TASAC – Makao Makuu. Maoni pia yanaweza kutumwa kwa njia ya barua kwa anuani ifuatayo: Mkurugenzi Mkuu, TASAC, S.L.P 989, Dar es Salaam. Mwisho wa kupokea maoni ni tarehe 13 Januari, 2023.

Wadau wote mnaalikwa kushiriki.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC),**

**28 Disemba 2022.**

PSSSF Garden Avenue Tower Building 7th and 8th Floor, Plot No. 20/21, Garden Avenue/Ohio Street,
P. O. Box 989, Dar es Salaam - Tanzania, Tel: +255 222 127 314,
Email: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz, Website: www.tasac.go.tz

17208002



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA
TASAC

# TAARIFA KWA UMMA

## MWALIKO WA KUSHIRIKI KATIKA MKUTANO WA WADAU WA KUKUSANYA MAONI KUHUSU MAOMBI YA MABADILIKO YA TOZO ZA USAFIRISHAJI MIZIGO KWA MELI ZA MV. NEW VICTORIA HAPA KAZI TU, MV. NEW BUTIAMA HAPA KAZI TU NA MV. UMOJA

Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limepokea maombi ya mabadiliko ya nauli ya usafirishaji mizigo kwa meli za MV. New Victoria Hapa Kazi tu, MV. New Butiama Hapa Kazi tu na MV. Umoja zinazomilikiwa na kuendeshwa na Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL).

Kwa mujibu wa kifungu cha 29 (2) (b) cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415, TASAC imeandaa Mkutano wa wadau wa huduma ya usafiri majini jijini Mwanza ili kukusanya maoni ya wadau kuhusu maombi ya mabadiliko ya nauli yaliyowasilishwa na MSCL.

Shirika linawaalika wadau wote kushiriki katika Mkutano huo utakaofanyika siku ya Ijumaa, tarehe 6 Januari, 2023 katika ukumbi wa mikutano uliopo ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji - Mwanza kuanzia saa 4 kamili asubuhi.

Aidha, wadau wanaweza kutuma maoni kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe tariff@tasac.go.tz au kwa kufika katika ofisi za TASAC – Mwanza au TASAC – Makao Makuu. Maoni pia yanaweza kutumwa kwa njia ya barua kwa anuani ifuatayo: Mkurugenzi Mkuu, TASAC, S.L.P 989, Dar es Salaam. Mwisho wa kupokea maoni ni tarehe 13 Januari, 2023.

Wadau wote mnaalikwa kushiriki.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mkuu,**
**Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC),**

**28 Disemba 2022.**

PSSSF Garden Avenue Tower Building 7th and 8th Floor, Plot No. 20/21, Garden Avenue/Ohio Street,
P. O. Box 989, Dar es Salaam - Tanzania, Tel: +255 222 127 314,
Email: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz, Website: www.tasac.go.tz

17208102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni habari njema korosho kupata soko Uholanzi

**IMEFAHAMIKA** kuwa zaidi ya tani 26 za korosho zilizobanguliwa kutoka Tanzania zimepata soko nchini Uholanzi.

Korosho hizo ni zilizobanguliwa katika kiwanda cha Amama Farms kilichoko wilayani Tandahimba mkoani Mtwara.

Taarifa hiyo njema imetolewa na Meneja Mkuu wa Kiwanda cha Amama Farms kilichoko wilayani Tandahimba kinachojishughulisha na ubanguaji korosho.

Mwakalinda Yassin ambaye ni Meneja Mkuu wa kiwanda hicho, hakuficha hisia zake kwa kuishukuru serikali kwa kuwatufutia soko la korosho Bara la Ulaya.

Kilio cha wakulima cha kupata soko la uhakika sasa kinaweza kuwa kimesikika na hatimaye sasa kuuza korosho zao kwenye kiwanda hicho na kusafirishwa nje ya nchi.

Kiwanda hicho kimekuwa na wawekezaji mbalimbali kutoka nchi za Ulaya ambao wanahitaji korosho zilizobanguliwa kutoka Tanzania na kwamba sasa nchi imewekeza soko la korosho zilizobanguliwa.

Imeelezwa kuwa kuanzia mwezi Januari hadi kufikia mwezi Desemba kwa mwaka huu wa 2022, kiwanda hicho kimeuza korosho zilizobanguliwa kwenda nchi za Ulaya ikiwamo Uholanzi na Marekani zaidi ya tani 414 na kwa uhakika zimesifiwa kwa ubora mzuri.

Zaidi ya tani 26 zilizobanguliwa na kiwanda hicho zimeshapata soko Uholanzi na Marekani na ziko mbioni kwenda moja kwa moja kwenye nchi hizo kipindi hiki cha mwezi Desemba, mwaka huu.

Tanzania kuweza kubangua korosho zake ni jambo la kujivunia kutokana na siku za nyuma kusafirisha nje ya nchi korosho ghafi kwa ajili ya kuchakatwa na kubanguliwa jambo ambalo kwa sasa linafanyika hapa nchini tena wilayani Tandahimba.

Ni jambo la kuishukuru serikali kwa kutafuta soko hilo na kiwanda hicho kilipofikia kimeomba ushirikiano uendelee vyema ili Tanzania iweze kutangazwa kwa soko hili la korosho za kubanguliwa.

Kabla kiwanda hicho hakijaanza ubanguaji korosho, zilikuwa zikipelekwa katika nchi za Vietenam na India ili zikabanguliwe na baadaye isafirishwe kwenda Ulaya kuuzwa.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Francis Alfred, anasema malengo ya bodi hiyo ni kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini na pia kubangua.

Unapotegemea kuuza korosho ghafi za Tanzania, soko kuu ni nchi mbili pekee ambazo ni India na Vietnam na kama uhitaji ukikosekana katika nchi hizo korosho inakosa soko la uhakika.

Njia pekee ya kupata soko la uhakika wa korosho ya Tanzania ni kubangua na baadaye kupeleka nchi za nje kama wanavyofanya kiwanda hicho cha Amama Farms.

Akipongeza kwa hatua hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba, Kanali Patrick Sawala, anasema kitendo cha usafishaji wa korosho kutoka Tanzania wilayani Tandahimba mpaka nchi ya Uholanzi si tukio dogo ni jambo kubwa na ni fahari kwa Tanzania na Rais wake.

Bodi ya Korosho imefanya kazi kubwa ya kusimamia zao hilo na wakulima kupata tija na kilimo hicho ambacho kwa upande wa serikali imetoa pembejeo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kwa utoro huu serikali 'isipoe'

Na Sabato Kasika

**MOJA** ya matukio yanayochafua maendeleo ya elimu mwaka huu ni utoro wa baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, jambo linaloweza kuchangia kukwamisha maendeleo yao kielimu.

Karibu mwaka mzima kulikuwa kunaripotiwa utoro kutoka shule mbalimbali hasa za sekondari. Kwa mfano, Februari mwaka walikuwapo watoro 436 katika Halmashauri ya Mji wa Nanyamba mkoani Mtwara .

Hawa walitakiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu, lakini walikuwa bado hawajaripoti shuleni.

Utoro huo ulisababisha viongozi kutangaza msako wa wazazi wa wanafunzi hao, huku watendaji kuanzia ngazi ya vijiji na kata katika halmashauri hiyo wakishiriki msako huo.

Wakati Mtwara kukiwa hivyo, wanafunzi 405 wa Shule ya Msingi Kumkambati iliyopo Kijiji cha Mvugwe mkoani Kigoma wameshindwa kumaliza elimu ya msingi.

Sababu inayotajwa na Mwalimu Mkuu , Ndabilole Raphael, ni utoro sugu, mimba na ndoa za ututoni.

Ni katika mahafali ya 19 ya shule hiyo, tatizo linafichuliwa, akifafanua kuwa ni wanafunzi 163 pekee walioandikishwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi katika shule hiyo kati ya 568 walioanza darasa la kwanza mwaka 2016.

Kwa ujumla matukio ya utoro yapo mengi katika shule mbalimbali, lakini hili la wanafunzi 963 wa shule za sekondari mkoani Njombe, kutofanya mtihani wa kidato cha pili nalo mwiba wenye ncha kali.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni, katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na Ofisa Elimu Nelas Mulungu, akifafanua kuwa mojawapo ya sababu za kutofanya mtihani ni utoro.

Aidha, janga hilo limesababisha wanafunzi wa kiume 584 na wasichana 379 kutofanya mtihani, kitendo ambacho ni vyema kitafutiwe dawa ya kudumu ili elimu ipewe kipaumbele.

> **Maisha yanategemea sana maji, mimea na hewa ili kuishi. Vivyo hivyo maisha ya mimea yanategemea maji na hewa katika uhai wake.**

INashangaza wakati huu serikali inagharamia elimu kuanzia ya awali hadi kidato cha sita lakini kuna watu wanaopuuza kusomesha watoto, haipendezi. Aidha, karne ya 21 elimu haipaswi kuwekwa pembeni, badala yake ipewe msukumo mkubwa kutokana na umuhimu wake kwa maendeleo ya mtu mmoja na taifa kwa ujumla. Wazazi na walezi ni wadau wakubwa wa elimu, hivyo wangesimama kidete kwa kufuatulia kwa karibu maendeleo ya watoto wao shuleni, wanaweza kubaini nyendo zao kirahisi na kama ni mbaya wazitafutie ufumbuzi haraka. Vilevile ingependeza kama utoro huo utaishia mwaka huu wa 2023 na kuanza upya mwaka ujao kwa kuzingatia umuhimu wa elimu kuwa ndiyo ufunguo wa maisha.

Ikumbukwe kuwa, serikali imekuwa ikifanya mikakati mbalimbali ikiwamo kutoa elimu bure, kwa lengo la kutaka kila mtoto aipate elimu tena katika mazingira mazuri.

Kwa nini wanafunzi waendelee kuwa watoro wakati mazingira ya kupata elimu yamesharahisishwa, ikiwamo elimu bure kuanzia elimu ya msingi hadi kidato cha sita? Jamii inataka nini kifanyike ndipo ione umuhimu wa elimu?

Mtindo wa kuendelea kuendeleza utoro, ni sawa na kukwamisha juhudi za serikali za kutaka kila mtoto apate elimu ambazo zinaonekana wazi hasa baada ya kuamua kutoa elimu bila malipo.

Inasikitisha kuona kukiwa na jitihada hizo, halafu kunakuwapo na baadhi ya wanafunzi wa sekondari ambao wanaamua kuwa watoro au kuacha shule, kitendo cha kuendelea kumkumbatia adui ujinga.

Tunapoelekea kuhitimisha mwaka huu wa 2022, ni vyema wazazi na walezi ambao watoto wao ni watoro wakatafakari na kuchukua hatua sahihi zitakazosaidia kukabiliana na utoro huo na kuutokomeza.

Mwaka 2023 Tanzania yenye watoto wanaosoma iwe suala la kila mlezi au mzazi, iwapo kila mmoja kwa nafasi yake atawajibika kikamilifu kupambana nao kuanzia nyumbani hadi shuleni kwa kushirikiana na walimu na wadau wengine wa elimu.

# HABARI PICHA



Sehemu ya wananchi wilayani Kyela wakimsikiliza Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (hayupo pichani), katika hafla ya utiaji saini mkataba wa ujenzi wa barabara mkoani Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Kamanda wa Polisi mkoani Manyara, Kamishna Msaidizi, George Katabazi, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu gari la kampuni ya Machimula's Express lililokutwa na bunda 341 sawa na kilogramu 157.5 za dawa za kulevya zikisafirishwa kutoka Arusha kwenda Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma juzi. **PICHA: JALIWASON JASSON**




Madereva wa bajaj wakipita kwenye barabara ambayo ni rasmi kwa ajili ya mabasi bila kujali maandishi (kushoto) yanavyoelekeza, eneo la Mbezi Luis Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, akisisitiza jambo alipozungumza na wananchi wa Kyela (hawapo pichani) katika hafla ya utiaji saini wa mkataba wa ujenzi wa barabara ya Ibanda-Kajunjumele (KM 22), Kajunjumele hadi Kiwira Port (KM 6) na Kajunjumele hadi Itungi (KM 4), mkoani Mbeya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama Kuu kutoa hukumu rufani ya DPP dhidi vigogo CWT

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam inatarajia kutoa hukumu ya rufani iliyokatwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Nchini (DPP), kupinga adhabu ndogo iliyotolewa kwa aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Self (46) na Mwekahazina, Abubakari Allawi Februari 17, 2023.

Aidha, siku hiyo mahakama itatoa hukumu ya rufani iliyokatwa na Self na Allawi, wakiipinga Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam kuwatia hatiani katika makosa mawili ya matumizi mabaya ya madaraka.

Juni 28, 2022 Mahakama hiyo iliwahukumu vigogo hao wa CWT kifungo cha miezi sita gerezani baada ya kupatikana na hatia ya makosa hayo, mahakama hiyo ilitumia saa saba kutoa hukumu hiyo yenye kurasa 122.

Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate wakati anasoma hukumu hiyo alisema, kama baba wa familia ameguswa kwa mazingira ya baba kutokuwapo nyumbani, kwa hiyo anawahukumu kifungo cha miezi sita jela kwa kila mmoja na rufani iko wazi kwa pande zote mbili.

Kutokana na hukumu hiyo, pande zote hazikuridhika zikakata rufani katika Mahakama Kuu na kupangwa kusikilizwa mbele ya Jaji Ephery Kisanya na kutoa hukumu za rufani hizo Februari 17, 2023.

Katika hoja zao za msingi DPP alikata rufani hiyo kupinga hukumu ya vigogo hao kwa madai kuwa adhabu iliyotolewa na Mahakama ya Kisutu ni ndogo kinyume na sheria.

Pia vigogo hao wa CWT Seif na Allawi, walikata rufani kupinga adhabu iliyowatia hatiani kwa madai kuwa Mahakama ya Kisutu ilikosea kuwatia hatiani kwa sababu hawana hatia kwa makosa waliyoshtakiwa.

Hakimu Kabate alisema, baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi tisa na vielelezo 11 vya upande wa Jamhuri na utetezi wa washtakiwa, upande wa mashtaka umethibitisha mashtaka yao na Mahakama inawatia hatiani.

Alisema, amesilikiza maelezo ya kupunguziwa adhabu na yeye kama baba wa familia ameguswa kwa mazingira ya baba kutokuwapo nyumbani. Hivyo, anawahukumu kifungo cha miezi sita jela kwa kila mmoja pia warejeshe Sh. milioni 13.9 mali ya CWT.

Aidha, hakimu alisema katika hukumu yake alizingatia kwamba, washtakiwa hao waliongoza vyema chama hicho, hawakuwahi kuitisha migomo katika kipindi cha uongozi. Kwa hiyo, kuna mambo mazuri wamefanya.

Washtakiwa hao wanadaiwa kati ya Oktoba 3, 2018 na Novemba 6, 2018 katika ofisi za CWT Kinondoni, wakiwa waajiriwa wa chama hicho, walitumia mamlaka yao vibaya kwa kujipatia Sh. 13,930,693.

Shtaka la pili, siku na maeneo hayo, Seif na Allawi, kwa kutumia madaraka yao vibaya na kwa manufaa yao wenyewe wanadaiwa kuchepusha fedha Sh. milioni 13.9 ambazo ni mali ya CWT. Viongozi hao wanadaiwa kutumia fedha hizo kwa ajili ya safari ya kwenda Cape Verde, kuangalia mpira wa miguu.



Askofu Mkuu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Msafiri Mbilu (kushoto), akisalimiana na Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Muheza Mjini, John Ndimbo, alipowasili kanisani hapo na kufanya uzinduzi wa kitabu cha Mzee Ibrahim Joseph Shemdoe kuhusu maisha yake na utumishi ulioacha alama jana katika ukumbi wa Comfort wilayani hapo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mwanafunzi ashikiliwa kwa tuhuma za mauaji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MWANAFUNZI wa Shule ya Sekondari ya Bugayambelele, Erick Peter (19), ameingia matatani kwa tuhuma za kusababisha kifo cha mtoto wa miaka mitatu, Supa Mayela, baada ya kuruka ukuta na kumdondokea.

Tukio hilo limetokea katika maeneo ya Mtunduni, Kitongoji cha Mtakuja, mkoani Geita.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoa huo, Ally Kitundu, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 20, mwaka huu.

Kitundu alisema, mtoto huyo aliangukiwa na ukuta wa matofari ya saruji wenye urefu wa futi tatu na kupelekwa katika Kituo cha Afya Katoro na wakati akipewa matibabu alifariki dunia.

Alisema kabla ya tukio hilo, mtoto huyo alikuwa akicheza na watoto wenzake watatu, ndipo mwanafunzi huyo alipopita na kuruka ukuta huo na kusababisha kuporomoka na kumuangukia mtoto huyo.

Kaimu Kamanda huyo alisema, Jeshi la Polisi linamshikilia mwanafunzi huyo kwa tuhuma za mauaji ya mtoto huyo.

Aidha, aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao wacheza maeneo salama ili kuepusha vifo vya namna hiyo.

# Askofu aongoza uzinduzi wa kitabu Maisha ya Shemdoe

**Na Steven William,** MUHEZA

ASKOFU wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Msafiri Mbilu, ameongoza mamia ya watu katika uzinduzi wa kitabu cha Mzee Ibrahim Joseph Shemdoe (74), kinachohusu maisha yake.

Uzinduzi huo umefanyika jana wilayani hapo, mkoani Tanga na kujaza maelfu ya watu.

Akizungumza katika uzinduzi wa kitabu hicho, Ofisa Elimu wa Mji wa Mafinga, Steven Shemdoe, alisema, baba yake ameandika kitabu kinachohusu maisha yake na utumishi ulioacha alama nchini.

Alisema lengo la kuandika kitabu hicho ni kutazama kupanda wigo wa kuendeleza uandishi wa vitabu hapa nchini.

Alisema katika utendaji kazi wake, mzee huyo amemtegemea Mungu na kumfanya aandike kitabu cha maisha yake kutoka alikotoka mpaka kufikia sasa umri wa miaka 74.

Askofu Mkuu Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Msafiri Mbilu, alimpongeza mzee huyo kwa kuandika kitabu hicho ambacho kinaelezea maisha yake ya kumwabudu Mungu.

Aliwaomba wananchi wote kuendelea kumwombea mzee huyo kwa kuwa, yalikuwa maombi yao kwa miaka mingi kwa Mungu awaletee mzee huyo.

Naye Katibu Mkuu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Julius Madiga, alisema, kitabu hicho kitasaidia kujenga uelewa kwa watu ili kujipanga katika maisha yao.

Mwandishi wa kitabu hicho, Shemdoe alisema: Lengo la kitabu hicho ni kuelezea ukweli kuhusu kufahamu zaidi nini alichobeba katika maisha yake na utumishi wake.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la KKKT Usharika wa Muheza, John Ndimbo na Mchungaji Msaidizi, Jonathan Mwamboza kwa nyakati tofauti walisema: Kuna umuhimu wa kukisambaza kitabu hicho kwa wananchi wengine kwa ujumla bila kujali dini wala madhehebu wanayotoka ili waweze kuwa na mtazamo chanya.

**Askofu Mkuu Kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Msafiri Mbilu, alimpongeza mzee huyo kwa kuandika kitabu hicho ambacho kinaelezea maisha yake ya kumwabudu Mungu.**

HABARI KITAIFA

## Ng'ombe wa sherehe azaa akitaka kuchinjwa

**Na Steven William,** MUHEZA

KATIKA tukio lisilotarajiwa, ng'ombe aliyepangwa kuchinjwa katika sherehe ya ufunguzi wa Kituo cha Biashara cha Msekwa Park, wilayani Muheza, mkoani Tanga, amezaa mtoto wakati akikaribia kuchinjwa.

Ng'ombe huyo alipangwa maalum kwa ajili ya hafla ya ufunguzi wa kituo hicho kilichoko Chuo cha Uuguzi cha Elijerry, barabara kuu ya Muheza Mjini kwenda Amani.

Akizungumzia tukio hilo, Mkurugenzi wa Chuo hicho, Elizabeth Chigua, alisema ng'ombe huyo alinunuliwa kwa ajili ya kitoweo katika hafla hiyo iliyoambatana na Sikukuu ya Krismasi.

Chigua alisema hawakufahamu kuwa alikuwa na mimba walijua amenenepa kutokana na kuhifadhiwa kwenye zizi.

Alisema wakati watu wakijiandaa kumchinja, ghafla ng'ombe huyo alizaa mtoto na kusababisha shughuli ya kumchinja kusitishwa na kulazimika kutafuta kitoweo kingine.

Chigua alisema kwao ni ishara ya baraka mfugo huo kuzaa mtoto kabla ya kuchinjwa na sasa atabaki kulea mtoto wake ambaye amezaliwa na afya nzuri.

Wachungaji watatu wa Kanisa la Anglikana wilayani Muheza walioshuhudia tukio hilo, walisema kuwa hiyo ni baraka nzuri katika ufugaji.

Mchungaji Rafael Majama, Paul Luhinga na Mchungaji msaidizi Elia Singano, walimwombea ng'ombe huyo na kummwagia maji ya baraka.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi wa Chuo cha Uuguzi cha Elijerry, katika hotuba yake ya uzinduzi wa kituo cha biashara cha Msekwa Park, alisema wamejenga kituo cha biashara cha Msekwa Park kusaidia kutoa ajira.

Meneja wa Kituo hicho, Steven Mganga, alisema kituo hicho kina uwezo wa kutoa ajira kwa vijana wakazi wa Muheza.

Alisema kimekusudia kutoa huduma kwa wakazi wa Muheza na watalii kutoka nje ya nchi ambao wanatembelea katika vivutio vilivyoko Magoroto na Tarafa ya Amani.

# Sendiga awaonya walimu kufanya ngono na wanafunzi

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga, amewaonya baadhi ya walimu wasio waadilifu wanaojihusisha kufanya ngono na wanafunzi wao kuacha tabia hiyo mara moja kwa kuwa serikali itahakikisha inawachukulia hatua kali za kinidhamu na kisheria ili kuwakomesha.

Alisema hayo hivi karibuni wakati akizungumza kwenye kikao cha kupokea madarasa 191 yenye thamani ya Sh. bilioni 38, fedha iliyotolewa na Serikali Kuu kwa ajili ya kutatua tatizo la madawati katika mkoa huo.

Sendiga alisema tayari ana orodha ya shule zipatazo 19 ambazo walimu wake wameripotiwa kushiriki ngono na wanafunzi wao hadi wengine kuwapa ujauzito na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na kuahidi mwaka ujao wa 2023 kamwe hakitafumbiwa macho.

"Maofisa elimu sekondari mnazifahamu shule zenu ambazo kuna baadhi ya walimu hawana maadili...mmekaa kimya kwa hiyo mnabariki si ndio?... Hadi walimu wanahonga wazazi, kuna watoto watano wamezalishwa wapo vijijini taarifa ninazo.

Ukipelekewa watoto shuleni nyie ni wazazi...jikazeni acheni tamaa zingatieni maadili ya kazi yenu tofauti na hivyo mtafungwa... sitowaacha salama," alisisitiza.

Aliwaagiza wakuu wa wilaya za mkoa huo ifikapo Februari 2023, wanaondoa tatizo la upungufu wa madawati na madarasa ya awali na msingi, upungufu ni madawati 99,043.

Alisema Wilaya ya Kalambo ina upungufu mkubwa wa madawati kwa msingi na awali ni 54,040, Nkasi 17,667, Wilaya ya Sumbawanga 20,623 na Manispaa ni 6,713.

Awali, Katibu Tawala wa mkoa huo, Rashid Mchata, alisema ujenzi wa madarasa hayo 191 yatasaidia kuwezesha kutumiwa na wanafunzi 25,362 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mapema Januari 2023.

Alisema kupatikana kwa madarasa hayo kumesaidia kuwapunguzia mzigo wa kuchangia miundombinu hiyo wazazi na walezi ambao kipindi kama hiki siku za nyuma wangekuwa wakibanwa kufanya hivyo.



Mchungaji Msaidizi wa Kanisa la Anglikana Muheza, Elia Singano akimwagia maji ya baraka ng'ombe aliyepangiwa kuchinjwa na kufanywa kitoweo katika sherehe ya ufunguzi wa Kituo cha Biashara cha Msekwa Park. **PICHA: STEVE WILLIAM**

# Korosho ya Tanzania yapata soko Uholanzi

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

ZAIDI ya tani 26 za korosho zilizobanguliwa kutoka katika Kiwanda cha Amama Farms wilayani Tandahimba, mkoani Mtwara, zinasafirishwa kwenda nchini Uholanzi barani Ulaya baada ya kupata soko kwenye nchi hiyo.

Meneja Mkuu wa kiwanda hicho kinachojishughulisha na ubanguaji korosho, Mwakalinda Yassin, alisema wanaishukuru serikali kwa kuwatafutia soko la korosho bara ya Ulaya.

Alisema kiwanda hicho kimekuwa na wawekezaji mbalimbali kutoka nchi za Ulaya wanaohitaji korosho zilizobanguliwa kutoka Tanzania na kwa ujumla Tanzania imeweza soko la korosho zilizobanguliwa.

Alifafanua kuwa kuanzia mwezi Januari hadi kufikia mwezi Desemba mwaka huu, kiwanda hicho kimeuza korosho zilizobanguliwa kwenda nchi za Ulaya ikiwamo Uholanzi na Marekani zaidi ya tani za korosho 414 na kwamba korosho hizo zimesifiwa kwa ubora mzuri.

Alisema zaidi ya tani 26 korosho zilizobanguliwa na kiwanda hicho zimeshapata soko katika nchi za Uholanzi na Marekani na ziko mbioni kwenda moja kwa moja kwenye nchi hizo mwezi huu wa Desemba, mwaka huu.

Alisema kitendo cha ubanguaji wa korosho kufanyika Tanzania ni jambo la kujivunia kwa vile siku za nyuma ilikuwa ikitoa korosho ghafi kupeleka nje ya nchi kwa kuchakatwa na kubanguliwa jambo ambalo kwa sasa halipo.

"Tunaishukuru sana serikali kwa kuweza kututafutia soko hili na sisi kutufanya tuweze kufikia hapa tulipo, hivyo tunaomba tuendelee kushirikiana vyema ili tuendelee kuitangaza Tanzania katika soko hili la korosho za kubanguliwa," alisema Yassin.

Alisema soko la korosho zisizobanguliwa huko nyuma zilikuwa zikipelekwa nchi za Vietenam au India ili zikabanguliwe na baadaye zisafirishwe kwenda Ulaya kuuzwa.

Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Francis Alfred, alisema melengo ya Bodi ya Korosho, kwanza kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini na pili ni kubangua.

Alisema bodi hiyo ina sababu mbili kuu za kuwa na lengo la kubangua korosho, kwanza inapotegemea kuuza korosho ghafi za Tanzania inategemea nchi mbili pekee ambazo ni India na Vietenam na kama uhitaji ukikosekana kati ya nchi hizo mbili inakosa soko la uhakika.

"Ili tuweze kuiona njia nyeupe katika tasnia hii ya zao la korosho ni kuacha kuuza ghafi na ili tuweze kuiona njia iliyo nyeupe basi ni kuuza iliyobanguliwa hapo ndipo itakuwa na thamani kubwa sana," alisisitiza Alfred.

Alisema njia pekee ya kupata soko la uhakika la korosho ya Tanzania ni kubangua na kupeleka nchi za nje kama wanavyofanya kiwanda hicho cha Amama Farms na wanapaswa kupongezwa kwa hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Tandahimba, Kanali Patrick Sawala, alisema kitendo cha usafishaji wa korosho kutoka Tanzania wilayani Tandahimba mpaka Uholanzi sio tukio dogo na ni fahari kwa nchi na maono ya viongozi hasa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema anaipongeza serikali pamoja na Bodi ya Korosho kwa kazi kubwa wanayofanya katika kusimamia zao hilo vyema na wakulima kupata tija na kilimo hicho na kwa upande wa serikali imetoa pembejeo kwa wakulima.

# Waja na mapendekezo matano kukomesha ukeketaji

**Na Sabato Kasika**

KIKAO cha viongozi wa Kata ya Mzinga Dar es Salaam, kilichokutana kujadili mbinu za kukabili ukeketaji kimetoa mapendekezo matano ambayo kinaamini yanaweza kusaidia kukomesha vitendo hivyo katika kata hiyo.

Baadhi ya viongozi hao waliokutana juzi katika kikao hicho, ni wajumbe wa nyumba 10, polisi kata, wenyeviti wa mitaa, diwani, viongozi wa dini, wazee maarufu, mratibu elimu na ulinzi shirikishi.

Mapendekezo matano walioibuka nayo ni kila mtu kwa nafasi yake kuripoti viashiria vya ukeketaji, kuhakikisha mabinti wanaokimbia ukeketaji kutoka kwao, wanafika makao salama bila vikwazo na kumchukulia hatua atakayeshuhudia vitendo vya ukatili bila kutoa taarifa kwa wakati.

Viongozi hao pia walipendekeza kila mtu kwa nafasi yake aendelee kutoa elimu kuhusu madhara ya ukeketaji na kufanya ukaguzi wa kushtukiza katika misafara ya vijana wa kiume wanaoenda kutahiriwa.

Lengo la kufanya ukaguzi huo ni kutaka kubaini kama kuna watoto wa kike, waondolewe ili wasifanyiwe ukatili huo unaopingwa na serikali pamoja na wadau wa kupambana na vitendo vya ukatili.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Mzinga, Oliver Gabriel, alisema walifikia hatua ya kuitisha kikao hicho baada ya kuwapo kwa mabinti wawili waliokimbia kutoka kwao baada ya kuona viashiria vya kuketwa. "Mabinti hao kwa sasa wametunzwa katika vituo vya kulelea watoto vya Msongola na Chanika, huku juhudi zikifanyika za kuhakikisha wanakuwa salama kama tutawarudisha kuungana na wazazi wao," alisema Oliver.

Diwani wa Kata ya Mzinga, Job Issac, alisema amechoka kuona kinachoendelea katika kata yake na kuongeza kuwa hawezi kuvumilia vitendo hivyo.

"Nimekuwa nikipokea simu kutoka kwa wadau mbalimbali kuniomba nifanye kitu, ndiyo maana nimeamua niwaite niwaeleze kuwa sasa naingia kazini najua kuna wengine mnajiandaa kukeketa watoto msije kunilaumu," alisema Issac.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mzinga, Nyaikoba Ryoba, aliahidi kuyafanyia kazi mapendekezo ya kikao hicho kwa kuwa amepata elimu ya kutosha na kwamba hawezi kuongoza jamii inayovunja haki za binadamu.

Ryoba alisema ataelekeza watu wa ulinzi shirikishi watabadili mbinu, ili wanazunguke usiku na mchana na kukagua misafara ya vijana wanaoenda kutahiriwa wahakikishe hakuna mabinti miongoni mwao.

"Pia niwashukuru uongozi wa Kata ya Mzinga, Sauti ya Jamii Kipunguni na WILDAF Tanzania kwa kuandaa kikao hiki ambacho kimesaidia kutoa elimu kuhusu madhara ya ukeketaji," alisema Ryoba.

Ofisa Programu kutoka Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WILDAF) Tanzania, Rehema Meremo, alisema kupitia kitengo cha dharura cha shirika hilo, lipo tayari kufanya kazi na jamii ya Mzinga.

"Yeyote atakayeona vitendo vya ukatili apige simu haraka, WILDAF itatoa usafiri, kwa ajili ya uokoaji pale ambapo polisi wataelemewa. Lengo ni kuhakikisha ukeketaji unakoma," alisema Rehema.




Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Abas Kayanda, akimkabidhi bango linaloonesha zawadi ya kutimiziwa ndoto ya kumaliziwa ujenzi wa nyumba yake, Happyness Tarimo, baada ya kushinda kupitia matumizi ya huduma za Kidijitali za M-pesa kutoka kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka, hafla iliyofanyika jana mjini Moshi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waliolipwa fidia kupisha upanuzi mgodi Barrick watakiwa kuondoka

**Na Samson Chacha,** TARIME

SERIKALI kupitia Mkuu wa Wilaya ya Tarime, mkoani Mara, Kanali Michael Mtenjele, amewataka wananchi wa Kijiji cha Komarera, Tarafa ya Ingwe waliofanyiwa tathmini na kulipwa fidia za mali zao kuondoka katika maeneo yao ili kupisha upanuzi wa Mgodi wa Barrick North Mara.

Aidha, imeonya wanasiasa kuacha kuchochea wananchi.

Akizungumza na wakazi wa kijiji hicho mwishoni mwa wiki akiwa ameongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya na wafanyakazi wa mgodi huo, Kanali Mtenjele alisema: "Serikali inatoa tamko kwa wananchi wanaoishi eneo la Kijiji cha Komarera kuondoka katika maeneo hayo badala ya kuanzisha mgogoro usio na tija ili maeneo hayo yatumike katika shughuli za upanuzi wa mgodi."

"Tunasikitishwa na baadhi ya wanasiasa wanaojitafutia umaarufu kuja katika kijiji hiki na kuwadanganya wananchi kuwa malipo ya fidia waliyopewa na kupokea yalikuwa kidogo wakati wananchi mlikubaliana na mkafanyiwa tathmini na picha zikapigwa za satellite zikionyesha mali zenu zilizokuwapo katika

maeneo yenu zikiwamo nyumba za nyasi na mazao na mkakubaliana."

Aidha, alisema wananchi hao walipokea hundi za fidia na mtu anapopokea fidia hiyo anatakiwa kuachia eneo hilo kwa mwekezaji, kama waliona fedha ni kidogo wasingepokea fedha hizo.

Mtenjele alisema mgodi umeanza kusafisha eneo hilo lililokwisha lipiwa fidia kwa ajili ya upanuzi na baadhi ya wanasiasa wameanza kutuma kwenye mitandao ya kijamii kuwahimiza wananchi kukataa kuondoka katika maeneo wakati walikwisha lipwa fidia na kupokea fedha na kuzitumia.

"Tunawaonya wanasiasa kuacha kuwachochea wananchi na kuanzisha mgogoro ambao hauna tija kwao kwani malipo walishapokea na kutumia, wanatakiwa kuondoka katika maeneo hayo bila shuruti," alisema.

Kadhalika, alisema watu wanajenga nyumba na kupanda miti ya matunda kama utitiri kwa ajili ya kutegesha ili walipwe huku tathmini ilishafanyika siku nyingi na watu kulipwa fidia.

Alisisitiza kuwa jambo hilo halikubaliki na kuwataka kuwa na uhusiano mzuri na mgodi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na taifa pia.

Aliwataka wasiwasikilize wachochezi kwa sababu wakati wananchi walipokuwa wakifanyiwa tathmini hawakufika kuwashauri.

Naye Ofisa Uhusiano wa Mgodi wa Barrick North Mara, Zakayo Makobora, alisema mgodi unaungana na agizo la serikali kwa kuheshimu mikataba na makubaliano iliyofanywa ya kuwalipa fidia watu wote waliofanyiwa tathmini za mali zao katika eneo la Kijiji cha Komarera na wamelipwa fidia zao.

"Tumeanza zoezi la upanuzi wa eneo kwa ajili ya shughuli za mgodi tunaomba wananchi kutoa ushirikiano na mgodi ili kujiletea maendeleo," alisema.

## 'Tatizo kiuchumi huwaingiza watoto kwenye ndoa'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

TATIZO la kiuchumi katika baadhi ya familia mjini Njombe limetajwa kuwa moja ya sababu ya wasichana wadogo kujiingiza katika ndoa.

Mkurugenzi wa Shirika la Safina Women Association, Yunus Lwendo, alisema hayo wakati akizungumza na gazeti Nipashe kuwa wengi wanakua hawajakomaa.

"Wanakua hawajakomaa hata viungo wanapokwenda wakipata mimba wanapata shida akili inakua haijapevuka kwa ajili ya kutunza familia kwa hiyo unakuta kwamba anashindwa kutunza familia na inaweza kusababisha migogoro kwenye familia yule aliyemwoa anaona kama ameoa mtu mkubwa kumbe ameoa katoto kadogo ambako bado hakajaelewa vitu vizuri," alisema Lwendo.

Hata hivyo, alisema madaktari wanashauri ni vizuri binti aolewe akiwa viungo vyake vimekomaa ili aweze kuhimili matatizo ya uzazi.

"Anaweza kujifungua vizuri, lakini unakuta mwingine lazima afanyiwe upasuaji kwa sababu viungo vinakua havijakomaa vizuri," alisema Lwendo.

"Huyu binti akiona kwamba amemaliza la saba au kidato cha nne, lakini hana mwelekeo unakuta anaamua sasa basi kinachofuatia ni kuolewa tu," alisema.

Alisema ni vyema marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 yakafanyika haraka ili kusiwe na nafasi ya namna ya kuhalalisha ndoa za utotoni.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Herieth Magaji, alisema sio kwamba ndoa za utotoni hazipo isipokuwa zinafanyika kwa siri.

"Wanafanya kisiri siri kwa sababu wanajua ni kinyume na sheria na zinazoripotiwa sasa hivi hamna, sijapata, kiuhalisia wanafunzi wanaomaliza darasa la saba wale wanaofaulu ndio wanaendelea ila hawa waliofeli wazazi wengi hawana fedha ya kuwaendeleza, wengi wapo mtaani wapo tu," alisema Magaji.

"Wanaripoti isipokuwa wakiwa hawajaelewana wenyewe kwa wenyewe ndio utaona wanakuja wazazi kuripoti kwamba amembaka mtoto yupo chini ya miaka 18, ukiangalia chimbuko ni kwa sababu hawakumalizia mahari kwa hiyo nyingi zinazoripotiwa ni kwa ubakaji na zinafika mahakamani," alisema.

# Tanzania kuuza mazao ya parachichi China, Marekani

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

TANZANIA iko katika hatua za mwisho, kukamilisha makubaliano ya kibiashara ya kuuza mazao yake yanayotokana na parachichi kwenye nchi za China na Marekani.

Akiwa katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya TARI SELIAN iliyoko mkoani Arusha, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema kwa sasa kinachoendelea katika mazungumzo hayo ni vitu gani vya kufuatwa, ambavyo ni hatua muhimu katika masoko ya kimataifa.

"Tumepata soko la parachichi nchini Afrika ya Kusini, Hispania na hivi sasa tunakamilisha mazungumzo na nchi za China na Marekani, kwa ajili ya hatua muhimu ambazo tunazifuata sasa ili tuanze kupeleka parachichi nyingi zaidi katika mataifa hayo," alisema.

Kutokana na uwekezaji huo, Naibu Waziri Mavunde, alisisitiza kuwa mazao yote yatakayotolewa kwenda nje ya nchi, hayatakuwa na shaka na hakuna mtu ataitilia mashaka, kwa sababu Tanzania imekidhi viwango vya ubora vya usafi wa mazao duniani na imepata ithibati ya kusafirisha mazao nje, pasipokuwa na kitu kinaitwa 'notification'.

Mavunde, alisema serikali imejipanga kuikuza sekta ya kilimo kwa asilimia 10, ifikapo mwaka 2030.

"Hivi sasa sekta ya kilimo inakua kwa asilimia 4.8, ilani ya CCM inatuelekeza kuikuza sekta hii kwa asilimia 5.8 ifikapo mwaka 2025. Hayo ndiyo maeneo, matarajio na mategemeo yetu.

"Utafiti unaofanywa na taasisi zetu, unakwenda kujibu mambo mengi na kupitia utafiti tutakuwa na uwezo wa uzalishaji wa mbegu bora ambazo zinastahimili ukame, lakini vilevile zitaongeza mavuno kwa wakulima wetu.

"Ni jukumu la TARI kuhakikisha kwamba wanabuni teknolojia na mbinu bora za kuwafanya wakulima wetu kulima kwa tija na mwisho wa siku tuweze kufikia malengo ambayo tumejiwekea.

"Kwenye bajeti ya mwaka huu, tumewatengea TARI kutoka Sh. bilioni 11.7 ya mwaka uliopita, mpaka Sh. bilioni 40.7, lengo lake tunataka kuona fedha hizi zinakwenda kwenye utafiti na mwisho wa siku matokeo ya utafiti yamfikie mkulima na mkulima anufaike na utafiti ambao inaufanya, hasa kulima kwa tija."

Vilevile, aliongeza kuwa eneo la pili ni la uzalishaji mbegu, serikali imetenga fedha pia kutoka Sh. bilioni 10.5 kwenda Sh. bilioni 43 na tumewaelekeza ASA kushirikiana na sekta binafsi.

Alisema serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi, itaendelea kuhamasisha wadau kuongeza uzalishaji wa zao la parachichi kutoka tani 190,000 mwaka 2018 hadi kufikia tani 215,000 mwaka 2022/23.

Mara kwa mara, Taasisi ya Kilele ya Mazao yanayotokana na maua, mboga, matunda, viungo na mazao ya mizizi (TAHA), imenukuliwa ikisema uzalishaji wa parachichi nchini, kwa mwaka uliopita, ulifikia tani 11,237, na thamani yake ni sawa na dola za Marekani milioni 33.



Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Lenganasa Soipey (wa pili kulia) na Mjumbe wa Wilaya ya Monduli, Siria Saibuli (wa pili kushoto), wakiwa kwenye harambee na uzinduzi wa kwaya ya Sayuni KKKT katika mtaa wa Oloshonyokie Naisinyai na kufanikisha kupatikana Sh. milioni 12.5 na dume moja la ng'ombe, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mradi wa maji kumaliza kero wananchi vijiji vinne

**Na Hamida Kamchalla,** LUSHOTO

WANANCHI 6,239 kutoka vijiji vya Irente, Yoghoi, Ngulwi na Bombo wilayani Lushoto wanatarajiwa kunufaika na mradi wa maji na kuondokana na kero iliyokuwa ikiwasumbua kwa miaka mingi.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Wilaya ya Lushoto, Mhandisi Edwin Kayetan, alisema mradi huo utagharimu zaidi ya Sh. milioni 578.

Aliyasema hayo baada ya Meneja RUWASA Mkoa wa Tanga, Mhandisi Upendo Lugongo, kufanya ziara ya kukagua miradi ya maji wilayani humo.

Kayetan alisema mradi huo unahusisha vilula (vituo vya kuchotea maji) 17, ukarabati wa matangi mawili yenye ujazo wa lita 175,000 kila moja na lingine la lita 50. Pia ujenzi wa chanzo kipya na ulazaji wa bomba mita 13,500.

"Mradi wa Maji wa Irente-Yoghoi-Ngulwi-Bombo utanufaisha wananchi 6,239 ambapo hadi kukamilika kwake utagharimu Sh. milioni 578.1 na utakuwa na vilula 17, ukarabati wa matangi mawili ya lita 175,000 kwa kila moja na tangi lingine la lita 50," alisema.

Aliongeza: "Lakini ujenzi wa chanzo kipya na ulazaji wa bomba umbali wa mita 13,500 chini ya Mkandarasi Buzubona & Sons Company Ltd wa Karagwe, Kagera. Mkataba unaisha Januari mwakani".

Kayetan alisema kwenye mradi wa maji wa Funta katika Halmashauri ya Bumbuli wilayani Lushoto utakuwa na vilula 23, wakazi 4,782 watanufaika na utagharimu Sh. milioni 832.6 hadi kukamilika kwake.

Alisema pia utahusisha ujenzi wa tangi lenye ujazo wa lita 90,000, ujenzi wa chanzo kipya na ulazaji wa bomba mita 9,900, utajengwa na Koberg Construction ltd, mkataba unaisha Mei mwakani.

Katika ziara hiyo Mhandisi Lugongo alisema RUWASA wapo tayari kuendelea kuongeza mahitaji ya matangi kwenye Kata ya Ngulwi ili wananchi wawe na ari ya kuchangia gharama ya huduma ya maji na kufanya miradi iwe endelevu.

Lugongo alisisitiza juu ya utunzaji wa mazingira na kulinda vyanzo vya maji hasa katika Kata ya Funta ambapo maeneo yake mengi yameharibiwa kutokana na uchimbaji wa madini.

Alisema: "Nimeona katika kata hii maeneo mengi yameharibiwa kutokana na uchimbaji madini, hivyo naamini viongozi wa vitongoji, vijiji, kata na wilaya watakaa kuweza kuweka mikakati ya kulinda vyanzo vya maji na mtiririko wa maji yanakopita."

## Viwavijeshi wavamia vijiji, washambulia mashamba

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKULIMA wa Kata ya Kiru na vijiji vya jirani katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara wamesema limeibuka kundi la wadudu waharibifu wa mazao waitwao mbilizi ambao wanatishia uhai wa mazao.

Wakizungumza na waandishi wa habari, wananchi hao walisema wadudu hao wamekuwa wakishambulia mazao yao hali inayohatarisha usalama wa chakula.

Akizungumza na Nipashe aliyekuwa Mbunge wa Babati Vijijini, Vrajil Jituson, alisema wadudu hao ni wengi wapo katika Bonde la Kiru.

Aidha, alisema wakulima wakubwa wameishaanza kupiga dawa za visumbufu ili kuepusha madhara. Alisema wadudu hao wakipita kwenye mzao majani yanaanza kunyauka.

Jituson alieleza kuwa wameanza kupiga dawa ili kuwadhibiti wadudu hao na kwamba hawaisubiri serikali ila kuna haja ya kutoa taarifa katika mamlaka za serikali ili zijue na kuanza kuchukua hatua za kuwatokomeza wadudu hao.

Mkazi wa Kijiji cha Daghailoy, Janeth Isaya, alisema siyo mara ya kwanza kwa wadudu hao kushambulia mazao, kwamba wanajitokeza hasa mvua inapoanza kunyesha.

Alieleza kuwa mbilizi huwa wanaingia kwa makundi makubwa na kushambulia mimea ya aina zote bila kujali ni aina gani.

Alisema wadudu hao wakijitokeza mwaka unaofuata wakulima wanapata mazao ya kutosha kitu ambacho anadai huwashangaza wengi.

Kaimu Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Manyara, Samweli Dahaye, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu alikiri kuibuka kwa wadudu hao maeneo ya Kiru na Kijiji cha Daghailoy.


Alisema wadudu hao wanaitwa viwavijeshi vamizi ila wakulima wamezoea kuwaita mbilizi.

Dahaye alisema wadudu hao wanakuwa wanajazana kwenye mashamba kama vile inzi.

Mtaalamu huyo wa kilimo alisema wadudu hao pia hujificha kwenye udongo ila mvua ikinyesha ndio wanatoka, kwamba waliingia nchini miaka mitatu iliyopita.

Alisema njia pekee ya kuwaondoa wadudu hao ni wakulima kuchukua hatua za haraka kupiga dawa ambazo watashauriwa na wataalamu.

Alisema njia nyingine ya kuwadhibiti ni wakulima kukagua mashamba yao mara kwa mara na kupiga dawa kwenye kiini cha mche ili uweze kuendelea kustawi.



# Wanafunzi 7,000 washindwa kufanya mtihani wa taifa

**Na Anjela Mhando,** MOSHI

WANAFUNZI 7,600 wa darasa la saba katika Mkoa wa Kilimanjaro, wameshindwa kufanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka huu kutokana na utoro, mimba na ugonjwa.

Kwa mujibu wa ripoti ya elimu iliyokabidhiwa kwa Katibu Tawala wa Mkoa huo, Willy Machumu, wanafunzi hao ni kati ya wale walioanza darasa la kwanza kwanza mwaka 2016 na kuatarajiwa kufanya mitihani hiyo Novemba mwaka huu.

"Wanafunzi waliojiunga na elimu ya msingi mwaka 2016 katika mkoa wetu, walikuwa 42,740 na kati yao wanafunzi 41,117 ndio waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka jana. Ukitazama takwimu hizo kuna kitu utagundua kwamba kuna wanafunzi 7,648 wameshindwa kufanya mtihani huo," alisema. Aidha, katika matokeo yaliyotangazwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), wanafunzi 33,469 walioko mkoani Kilimanjaro, ndio waliofaulu kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2023.

Akizungumzia ufaulu wa wanafunzi kwa ngazi ya halmashauri, Machumu alisema Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, imeongoza kwa asilimia ya ufaulishaji wa wanafunzi, ukilinganisha na halmashauri nyingine sita za mkoa huo.

Katika taarifa hiyo, Manispaa ya Moshi, inafuatiwa nafasi ya pili na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi na nafasi ya mwisho ya ufaulu ikishikiliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Kutokana na takwimu hizo, Katibu Tawala huyo, ameiagiza Kamati ya Elimu kufanya mchanganuo zaidi ili kujua sababu zilizosababisha wanafunzi hao kushindwa kufanya mitihani hiyo.

Akizungumzia uboreshaji wa sekta ya elimu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mkoa wa Kilimanjaro, uliidhinishiwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sh. bilioni 353.38 kwa ajili ya mishahara, miradi ya maendeleo na matumizi mengineyo.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Mazingira Tanga, Mhandisi Geofrey Hilly, akisisitiza jambo kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, wakati wa ziara yake ya kutembelea miradi ya maji juzi, (kulia) ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tanga –UWASA, Dk. Ally Fungo. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Shughuli za kibinadamu katika chanzo cha maji kwamchefua RC

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SHUGHULI za kibinadamu zinazofanyika katika chanzo cha maji cha Mabayani kilichoko Jiji la Tanga, kumemchefua Mkuu wa Mkoa wa huo, Omari Mgumba, akiwaonya wananchi wa eneo hilo wanaondelea kukaidi amri kuacha kuijaribu serikali.

Mgumba aliagiza Serikali ya Mtaa wa Mabayani, kuwatangazia wananchi juu ya amri hiyo ya kutakiwa kusitisha shughuli hizo.

"Hili ni katazo na kila mmoja anapaswa kulizingatia. Wananchi wote wanaoishi karibu na vyanzo vya maji vilivyoko eneo la Mabayani acheni kufanya shughuli za binadamu kwenye vyanzo vya maji kama kilimo. Unaofanyika hapa sasa ni uharibifu wa mazingira na sio utunzaji wa mazingira, kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadaye.

"Nimekuja hapa kukagua na kutoa maagizo yangu, kwa sababu ya hali ya upatikanaji wa maji ilivyo sasa kwenye Mto Zigi na Bwawa la Mabayani. Ukame umesababisha vyanzo vingi vya maji kukauka na vingine kufa na hivyo kuathiri upatikanaji wa maji ya kutosha kwa wananchi wa Tanga Mjini."

Aidha, alisema vyanzo hivyo vimeharibika kutokana na shughuli hizo za kibinadamu ambazo kama zisipokemewa na kudhibitiwa hali inaweza kuwa mbaya zaidi kwa wananchi kuingia katika mgawo mkali wa maji.

"Nimejiridhisha kwamba Bwawa la Mabayani na Mto Zigi, sasa yana maji ya kutosha katika vyanzo hivyo. Natoa rai kwa wananchi acheni kufanya shughuli za binadamu karibu na vyanzo hivi. Nimefurahi kwa kuwa nimeona hata mradi wa maji unaotekelezwa na Tanga UWASA, umefikia asilimia 75," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Tanga UWASA, Dk. Ally Fungo, alimshukuru Mkuu wa Mkoa huo, kwa kutembelea na kukagua miradi yake hususani kwenye vyanzo vya maji vya Maabayani na Mto Zigi.

Alisema matatizo madogo yaliyojitokeza wamejitahidi kuyatatua na maji yameongezeka kwenye bwawa lao.

Dk. Fungo pamoja na mambo mengine aliwasihi wananchi wanaoishi karibu na bwawa hilo kuitunza miundombinu iliyoko eneo hilo, kwa kuwa ni faida kwa wananchi wote.

Alisema: "Lakini wananchi wa vijiji vilivyoko kwenye Bwawa la Mabayani wanashiriki kuhakikisha bwawa hilo lipo salama na vyanzo vinahifadhiwa na kwenye vyanzo vya Misitu ya Amani, kuna vikundi vya kutunza mazingira kuhakikisha vyanzo vinalindwa."

# Watoto sita wazaliwa mkesha wa Sikukuu ya Krismasi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WATOTO sita wamezaliwa wakati wa mkesha wa Sikukuu ya Krismasi, kati ya hao wanne walizaliwa katika Hospitali ya Mission Dareda na wawili Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara.

Akizungumza na Nipashe Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mission Dareda, Dk. Joseph Lori, alisema katika hospitali hiyo walizaliwa watoto wanne.

Dk. Lori alisema watoto wawili walikuwa wanaume na wengine wawili ni wanawake ambapo mtoto aliyezaliwa na uzito mkubwa kati ya hao alikuwa ni mwanaume na uzito wake ulikuwa kilogramu nne na mtoto aliyekuwa na uzito wa chini kati ya hao ni mwanamke ambaye alikuwa na kilogramu 2.8.

Aidha, Nipashe ilitaka kufahamu uzito huo wa kilogramu 2.8 unafaa ambapo Dk.Lori alisema uzito huo unafaa kwa kuwa uzito unaotakiwa kitaalamu ni kuanzia kilogramu 2.5.

Alisema watoto wanaozaliwa na uzito pungufu shida kubwa wanakuwa wanazaliwa kabla ya kufikisha siku zao.

"Shida nyingine inakuwa kondo la nyuma la mama anakopata chakula mtoto anakuwa hapati chakula cha kutosha," alisema Dk. Lori.

Alisema mtoto kuzaliwa akiwa na uzito pungufu unaweza kuwa unasababishwa na wanawake wanaokunywa pombe au wanaovuta sigara wakati wakiwa wajawazito.

Dk. Lori alieleza kuwa endapo mama mjamzito anaishi mazingira ambayo kuna moshi wa sigara ni hatari kwa afya yake.

Alisema ili mjamzito aepushe madhara hayo kwa mtoto ni vizuri aanze mapema kuhudhuria kliniki ili apate ushauri wa kitaalamu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali alisema katika hospitali hiyo walizaliwa watoto wawili wanaume mmoja alikuwa na uzito mkubwa wa kilogramu 3.7 na mwanaume mmoja ambaye alikuwa na uzito wa kilogramu 3.4.


Ukurasa 14

**2022 mwaka usio na matukio makubwa Tanzania**


Ukurasa 15

2022 mwaka Ndugai alipoandika historia ni kuwa Spika wa kwanza kuachia ngazi


Ukurasa 19

**Uingereza ilivyobadili viongozi kama 'mswaki'**

siasa
JUMATANO DESEMBA 28, 2022
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

# 2022 ni mwaka wa wamachinga biashara zao mijini bado kitendawili

**Na Nimi Mweta**

MOJAWAPO ya maeneo ambayo yametikisa na kuleta malalamiko, hofu na lawama mwaka 2022 ni suala la wafanyabiashara wadogo (wamachinga) maeneo mengi mijini.

Watanzania hawa, kama wananchi wengine wanatazamia kwa kumsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan, ili kuliona suala zima la kuwawezesha wafanyabiashara wadogo hao kufikia mazingira bora ya kukua na kustawi bila kukwazwa kwa taratibu ambazo si rafiki.

Kwa mtazamo huo, wafanyabiashara wadogo wanaona kuwa wametikiswa. Wamebomolewa vibanda, kufukuzwa kwenye maeneo ya kuuzia bidhaa, wengine wakitakiwa kuonekana usiku pekee na mchana wajipange wajue wanafanya nini. Wanapomsikia Rais Samia wanafikiria urasimishaji wao upo pale wanapofaulu na kuwa katika mazingira ya kuingia mfumo rasmi ambao hasa ni kuwa na anuani ya mahali pa kufanyia kazi penye uhakika, yaani panapofunguliwa na kufungwa si kubeba mzigo barabarani. Pia kuna mkataba wa kulipa kodi.

Siyo kurasimisha kwa kuweka vifaa vya kielektroniki kwa wabeba mizigo kichwani wanaosaka wateja mitaani na barabarani.

Mtazamo wa ustawishaji unalenga manufaa ya wafanyabiashara wadogo wajue kuwa nchi inawajali na kuwa, wakijaribu kitu fulani (kama biashara) kinakuwa na nafasi ya kufaulu kwa kiwango cha kuridhisha, licha ya kuwa siyo kila mmoja atafulu, biashara istawi.

Suala hapo linakuwa siyo kuchangia maendeleo bali kumudu maisha. Kwa maana mtu mmoja akifaulu katika biashara ndogo, kutembeza bidhaa au kupanga chini au kwenye vimeza vya kuweka na kuondoa bado si mfumo rasmi.

Kuwapachika mashine za kukata risiti kielektroniki (EFD) na kusema wako mfumo rasmi ni kupambana na rai ya awali ya kuwezesha biashara ndogo zistawi, wamudu maisha kwanza, si kodi.


Ndivyo wamachinga walivyosambaa kila mahali kwenye stendi ya Mbezi jijini Dar es Salaam. **PICHA SABATO KASIKA**

Mkanganyiko huo umekuwapo muda wote ambapo wafanyabiashara wasio na mahala rasmi ambako kuna anwani halisi wamekuwapo na vianzio vyake vinatoka mbali katika hisia na hali halisi. Binadamu na wanyama wana mifumo ya ufahamu ambayo msingi wake ni kuwinda na kuwindwa. Hivyo, katika maisha na takriban chochote kinachofanyika, kuna mvutano unaoendana na hisia hizo. Kinyume chake ni hisia za kuchunga, kulinda na kulea, au katika suala hili ni ile jitihada ya kustawisha, kwa hitaji la kijamii kuwa wafaulu katika maisha kama sehemu ya mshikamano na kuwapo matumaini. Wawindaji hawajitumi kwa hilo.

Kutafuta kodi kwa nguvu zote kutoka katika kundi hili la wanyonge ambao kuweza kumudu maisha ni mashaka matupu ni sehemu ya hulka ya kuwinda, ila inajihalalisha kijamii au kiitikadi kama yenye dhamira ya kuongeza mapato, ili jamii ipate zahanati, shule.

Ni mtazamo wa kinafiki ambao huanza kuiangalia jamii kwa mahitaji ya jumla na si ya watu binafsi, kwa kuanza na familia. Ni kama kumuuliza mtu 'huruma ni nini' ajibu kuwa ni kuhakikisha kila mtoto anasoma, badala ya kusema anapata chakula, mahali pa kulala na shule ili apate elimu.

Ni hali ambayo imelisumbua Jiji la Dar es Salaam na kwingine kwani mandhari ya jiji yanatakiwa yapendeze, watu waegeshe magari na kuingia dukani na siyo wakute 'kibajaji' cha biashara kimetinga na kuziba wasiweze kuegesha hata kupita ni taabu. Hivyo, wafanyabiashara wadogo wanakuwa wasumbufu kwa wakazi wengi wa jiji na ikaamuliwa kuwa, angalau wabaki katika masoko rasmi pekee.

Hilo tayari wafanyabiashara ndogondogo wameanza kulizoea, baada ya mamia au maelfu kati yao kukwama katika shughuli hiyo, kwani masoko si sawa na kupanga biashara katika barabara zote hasa viunga vya miji. Katikati ya jiji tayari walishaondolewa labda kwa maeneo tengefu ya masoko

INAENDELEA UK. 20

# 2022 mwaka usio na matukio makubwa Tanzania

## •Ni mwendokasi wa maendeleo, kutegeana kisiasa

Na Mwandishi Wetu



Rais Samia Suluhu Hassan, akishuhudia Bwawa la Mwalimu Nyerere moja ya miradi mikubwa ya kimkakati, likijazwa maji hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

MWAKA unaomalizika wa 2022 ulikuwa wenye kila la kufurahisha hapa nchini ukilinganisha na yaliyokuwa yanaendelea katika mataifa mengine. Ahueni ya mwaka huu inatokana na ukweli kuwa 2021 na hata 2020 ulikuwa na unafuu na kupungua kwa UVIKO -19.

Pengine siyo kwamba watu hawakufariki kwa maradhi hayo lakini huwezi kulinganisha na idadi ya waliopoteza maisha kwingineko duniani.

Kwa suala hilo kuna jambo la kuongeza tafakari kuwa kwenye mwisho wa mwaka huu wakati dunia kwa jumla inaanza kuusahau UVIKO-19, nchini China sasa unapamba moto.

Tatizo limeendelea kuwapo hata baada ya kukwama kwa sera ya 'zero COVID,' inayohusisha kufungia watu ndani na kutoa vibali maalum baada ya kupima ili kudhibiti maradhi hayo.

**MIRADI KIMIKAKATI**

Mwaka 2022 Watanzania wanashuhudia ukamilishwaji na mwendelezo wa miradi na mikakati iliyoanzishwa wakati wa awamu ya tano ambako Rais Samia Suluhu Hassan, aliahidi kila ambacho serikali ilikianzisha hakitaachwa na awamu ya sita.

Kuanzia 2021 na hata 2022 zilitafutwa nyenzo nyingine kwa mfano tozo katika kupelekeana fedha kwa njia ya simu, ingawa viwango vilivuka mpaka katika bajeti ya 2022 ikabidi virekebishwe visilete madhara kibenki na kisera.

Kwa jumla jitihada zilizobaki za kujenga miundombinu, reli ya kisasa SGR, kukamilisha bwawa la umeme la Julius Nyerere ambalo sasa limeanza kujazwa maji, viko pia vituo vya afya na shule mpya pamoja na madarasa mengi zaidi yanajengwa kwa kasi.

Yako maeneo ambayo kasi inashangaza, kwa mfano kukamilisha kufikisha umeme vijiji vyote hadi kufikia mwisho 2025.

Eneo ambalo kwa upande fulani lilikuwa na mwendo halisi wa kutatua matatizo halafu mikwamo ya wazi inayotokana na baadhi ya maelekezo ya awamu ya tano, ni mdahalo kuhusu mfumo wa siasa na hasa kuvizuia vyama vya siasa kuendesha shughuli zake kwa mwaka wa saba sasa.

Ni suala ambalo serikali imesikika ikiahidi kuwa inakaribia kutoa rasimu ya kukubali mapendekezo ya kikosi kazi cha kuboresha demokrasia, hasa suala la mikutano ya hadhara ya vyama inayoruhusiwa kikatiba ndilo eneo nyeti zaidi.

kwa ujumla jambo hilo, mwaka 2022 ulianza kwa kiongozi wa CHADEMA Freeman Mbowe na wenzake watatu kukutwa na mahakama kuwa wana kesi ya kujibu, ambayo bila shaka ingechukua muda mrefu na kuendelea kudumaza shughuli za siasa, kujenga uhasama zaidi, hadi kufikia 2025 wakati wa uchaguzi mkuu, hiyo ilikuwa Februari 2022 .

Mwezi Machi mwaka huu, Mkurugenzi wa Mashtaka Sylvester Mwakitalu, akatangaza kuwa hana nia ya kuendelea na kesi hiyo na kwa maana hiyo Mbowe akaachiwa huru.

Ni katika kufikia maridhiano na uhimilivu wa kisiasa Mbowe anafika Ikulu akiteta na Rais Samia, kukawa na matumaini ya maelewano.

Suala la wabunge 19 wa viti maalum waliofukuzwa CHADEMA, baada ya Mbowe kuteta na Rais Samia, mwenyekiti huyo aliashiria katika hotuba Iringa aliposhirika hafla ya Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA) kuwa ingefaa suala hilo liachwe. Ingekuwa ni hatua ya kwanza ya maelewano ila ikakwama Baraza Kuu, jambo likaachwa pembeni na sasa kesi inaendelea mahakamani ukibaki kuwa mkwamo unaodumu.

Baada ya mkwamo huo wa vielelezo vya maelewano mkakati wenyewe wa maelewano ukabakia, kikaundwa Kikosi Kazi cha kuweka sawa mfumo wa kidemokrasia wa kuendesha vyama vya siasa. Inawezekana kweli zipo kanuni zitarekebishwa lakini kama ilivyo katika urekebishaji wa sheria ya vyombo vya habari, si rahisi kutazamia kuwa serikali ijivue uwezo wa kuingilia kati, kuonya, kudhibiti au kuzuia.

Ndani ya ukanda wa Afrika Mashariki 2022 ni mwaka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ilipojiunga na Jumuiya, kuwezesha suala la amani mashariki ya nchi hiyo liwe la kikanda.

Nchi kadhaa zinataka kufanya biashara halali na DRC ambayo inasimamiwa na mifumo kama umoja wa forodha, hati ya kusafiria ya kijumuiya, soko la pamoja na sasa Soko Huria la Afrika ambalo limeridhiwa kwa viwango tofauti.

> Mwezi Machi mwaka huu, Mkurugenzi wa Mashtaka Sylvester Mwakitalu, akatangaza kuwa hana nia ya kuendelea na kesi hiyo na kwa maana hiyo Mbowe akaachiwa huru.

Kuendelea kwa vikosi vya waasi kudhibiti eneo hilo na kuchota madini huku haki za binadamu zinavunjwa ni mkakati ambao muda wake umepita. Licha ya M23 kujizatiti kwa mapambano kikamilifu sambamba na juhudi za kupata amani zinazoendelea Nairobi na Angola.

Eneo jingine ambako limeonekana mbele ya dunia nzima ni jinsi Rais Samia alivyomudu kuteka hisia za watu na kuonyesha mbinu mbadala za maendeleo, nje ya kuendeleza miradi mikubwa.

Amefikisha uwezekano wa makubaliano kwa miradi kama Bandari ya Bagamoyo kuanza tena kutangaza zabuni za ujenzi wake, mradi wa kuchakata gesi asilia mkoani Lindi ambao kimsingi una uwezekano wa kubadili sura ya nchi kimapato na kukamilisha itifaki ya kuanza kuchimba njia ya bomba la mafuta kutoka kaskazini ya Uganda kwenda Tanga.

Bomba la mafuta kwenda Zambia sasa linapata kasi mpya ya kusafirisha gesi kutoka Dar es Saalam, halafu kuna bomba la gesi kutoka Dar es Salaam kwenda Mombasa limeshaafikiwa. Ni diplomasia ya uchumi ya kasi na mageuzi.

Tukio ambalo lilimpambanua Rais Samia heshima kwa haiba yake ne kujituma ni kushiriki filamu ya 'Tanzania: The Royal Tour' Inaelekea kuwa ilifaulu kuchochea utalii, pamoja na hatua nyingine za diplomasia ya uchumi zilizofanya Tanzania ing'are katika mageuzi ya uchumi mwaka uliopita.

Rais Samia anakuwa kiongozi mkuu wa kwanza kutoka nje aliyekaribishwa China baada ya mkutano mkuu wa Chama cha Kikomunisti kilichomthibitisha Rais Xi Jinping katika nafasi hiyo akiitumikia nchi yake kama kiongozi wa maisha.

Alipoingia madarakani mwaka 2013 Tanzania ilikuwa ndiyo nchi ya kwanza kuitembelea nje, kama ambavyo Rais Barack Obama alipoingai madarakani mapema 2009 kiongozi wa kwanza kutoka Afrika aliyepewa nafasi ya kumwona Ikulu ya Washington alikuwa Rais Jakaya Kikwete, hivyo Rais Samia anajenga katika misingi iliyokuwa imara.

# 2022 mwaka Ndugai alipoandika historia ni kuwa Spika wa kwanza kuachia ngazi

**Na Sabato Kasika**

SIKU tatu zimebakia kuhitimisha mwaka 2022, tunawatakia heri na baraka tele wasomaji wetu, tukiwasihi waendelee kuwa nasi mwakani.

Kwa ujumla 2022, yalikuwapo matukio mengi katika uwanja wa siasa tangu ulipoanza na sasa unapoelekea ukingoni, miongoni mwa mambo makubwa yaliyojiri ni la Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai, kutangaza kujiuzulu nafasi hiyo ikiwa ni siku chache za kusambaa kwa video ambayo alinukuliwa akisema ipo siku nchi itauzwa kutokana na madeni.

Alijiuzulu Januari 6 kwa kuandika barua kwa Katibu Mkuu wa CCM, na kwamba uamuzi huo ulikuwa ni wa binafsi na hiari, kwa kuzingatia maslahi ya nchi, serikali na chama.

Kabla ya kuchukua uamuzi huo, kulikuwa na shinikizo kubwa kutoka kwa makada wa CCM wa mikoa mbalimbali waliotaka aachie ngazi kutokana na kwenda kinyume na serikali, kwa kutoka hadharani na kupinga hatua ya kukopa fedha nje akidai itasababisha nchi kupigwa mnada.

**KIKOSI KAZI KAZINI**

Januari 11, mwaka huu, kikosi kazi kilichoagizwa kiundwe na Rais Samia Suluhu Hassan kwa Msajili wa Vyama vya Siasa, kinanza kazi.

Ni kupitia na kuchambua maoni na mapendekezo yote yaliyotolewa na washiriki wa mkutano wa wadau Desemba mwaka jana kuhusu mwenendo wa demokrasia.

Majukumu ya kikosi kazi hicho yalikuwa ni kuchambua hotuba ya kufungua, kufunga, maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika mkutano wa wadau na kuainisha masuala muhimu ya kufanyiwa kazi.

Miongoni mwake ilikuwa ni kuandaa mpango kazi wenye masuala tisa ambayo ni kuchambua na kuandaa maoni na mapendekezo kuhusu suala la mikutano ya hadhara na mikutano ya ndani ya vyama vya siasa.

Kuandaa taarifa ya awali ya kikosi kazi iliyowasilishwa kwa Rais Samia, kukaribisha maoni ya wadau, kutoa maoni kwa serikali kuhusu utungaji wa kanuni za kuratibu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa.

Mengine ni kuzungumza na wadau mbalimbali wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar, ili kupata maoni yao, kuchambua maoni ya wadau na kuandaa ripoti ya kikosi kazi.

Machi 21 kikosi kazi kiliwasilisha kwa Rais Samia Suluhu Hassan, lakini naye akataka mapendekezo ya kikosi hicho kifanyie kazi maboresho yote yaliokubaliana ili baadaye waone kama kuna haja kurekebisha katiba ya nchi.

**LISU Vs RAIS**

Tukio jingine kubwa lililojiri mwaka huu, ni Rais Samia Suluhu Hassan, kukutana na kufanya mazungumzo mafupi na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu.

Rais alikutana na kiongozi huyo wa upinzani jijini Brussels nchini Ubelgiji Februari 16, ni baada ya Rais kukubali maombi yake ya kukutana naye na kuzungumza masuala mbalimbali yenye maslahi na ustawi wa taifa.

**MBOWE HURU**

Machi 4, mwaka huu, CHADEMA ililipuka ni baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka, kumfutia kesi ya ugaidi Freeman Mbowe, Mwenyekiti wa CHADEMA ambaye alikuwa anashikiliwa na wenzake watatu dhidi ya mashtaka mbalimbali yakiwamo kupanga njama na kufanya vitendo vya kigaidi.

Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali, Sylvester Mwakitalu, anawasilisha hati ya kutokuwa na nia ya kuendelea na kesi hizo, katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, hatua ambayo inampa uhuru Mbowe na wenzake watatu.

Ni baada ya mahakama kusikiliza hoja iliyoletwa na wakili mwandamizi wa serikali akisema Mkurugenzi wa Mashtaka hana nia ya kuendelea na kesi hiyo, upande wa pili wakaridhia.

Shauri hilo lililokuwa linawakabili washtakiwa Khalfani Bwire, Adam Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Freeman Mbowe, ambao awali kesi yao ilitokea kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ambayo haikuwa na mamlaka ya kusikiliza kisheria.

**WABUNGE 19 'OUT'**

Mei 11, Kamati Kuu ya CHADEMA inapiga kura na kuwafukuza wanachama 19 akiwamo Halima Mdee waliokuwa wanatuhumiwa kwa utovu wa nidhamu kwa kosa la kuapishwa kuwa wabunge bila ruhusa ya chama chao.

Baada ya uamuzi huo wa kuwafukuza katika chama, Julai 22 walifungua kesi ya kupinga kufukuzwa uanachama ambayo inataendelea kusikilizwa Machi mwaka kesho katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Dar es Salaam.

Pamoja na Halima Mdee, wengine waliovuliwa uanachama ni Esther Matiko, Grace Tendega, Cecilia Pareso, Ester Bulaya, Agnesta Lambart, Nusrati Hanje, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Asia Mohammed, Felister Njau, Nagenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Stella Fiao, Anatropia Theonest, Salome Makamba na Conchesta Rwamlaza.

**RAIS, CHADEMA WAKUTANA**

Mei 20, Rais Samia anaandika historia kukutana na viongozi waandamizi CHADEMA, Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma na kuongoza kikao cha majadiliano akiwa na Mwenyekiti Freeman Mbowe.

Wengine wanaoshiriki ni Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Saidi Issa Mohamed, Katibu Mkuu wa John Mnyika na baadhi ya wajumbe wa Kamati Kuu na Sekretarieti ya CHADEMA

**VURUGU NCCR**

Mei 21, vurugu zinatikisa makao makuu ya NCCR- Mageuzi, baada ya Halmashauri Kuu kumsimamisha Mwenyekiti wa chama hicho, James Mbatia na Makamu wake upande wa Bara, Angelina Rutairwa.

Kikao hicho cha Halmashauri Kuu kinakutana, katika ukumbi wa Jeshi la Wokovu ulioko Kurasini Dar es Salaam na kutangaza kuwasimamisha viongozi hao wawili.

Baada ya mkutano huo, Mjumbe wa Halmashauri Kuu, Joseph Selasin, Katibu Mkuu wa Chama hicho, Martha Chiomba, wakiambatana na walinzi, wanafika kufunga ofisi za chama hicho makao makuu na kutangaza kuwa hakuna shughuli zitakazoendelea katika ofisi hizo hadi baadaye.

Hata hivyo, baada ya ofisi hizo kufungwa, baadhi ya wanachama wanaodaiwa kuwa upande wa Mbatia, walifika katika ofisi hizo wakitaka kuzifungua, kitendo ambacho kilisababisha vurugu kwa muda.

Mgogoro ndani ya chama hicho, ulifikia hatua ya kumtumia Mbatia kumvua uongozi Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Angelina Rutairwa, katika Mkutano Mkuu uliofanyika Septemba 24, jijini Dodoma.

**MABADILIKO KATIBA**

Oktoba 21, Rais Samia anapokea ripoti ya kikosi kazi kuhusu uratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kutoka kwa mwenyekiti wake Prof. Rwekaza Mukandala katika hafla iliyofanyika Ikulu Dar es Salaam.

Moja ya mapendekezo yanayotolewa na kikosi hicho, ni kuruhusiwa kufanyika kwa mikutano ya hadhara kwa mujibu wa Katiba na Sheria na kuzingatia asilimia 40 ya jinsi katika vyombo vya maamuzi vya vyama vya siasa.

Kikapendekeza pia utaratibu mpya wa kupata wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, utendaji wa tume uruhusiwe kuhojiwa kwenye Mahakama ya juu na isilazimike kufuata amri ya mtu yeyote, idara yoyote ya serikali, chama

**VIGOGO CCM CHALI**

Januari mosi mwaka huu, CCM inatoa ratiba ya uchaguzi wa viongozi wa chama hicho na jumuiya zake kuanzia ngazi shina hadi taifa na kuhitimisha uchaguzi huo Novemba mwaka huu, huku baadhi ya vigogo wakianguka.

Moja ya vigogo walishindwa kufurukuta katika uchaguzi huo, ni aliyekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, Dk. Edmund Mndolwa aliyebwagwa na Fadhil Maganya.

Katika uchaguzi huo uliofanyika Novemba 25, mwenyekiti wa sasa Maganya anakuwa mshindi kwa kupata kura 578 kati ya kura 835 zilizopigwa, huku Dk. Mndolwa akiambulia kura 16.

Baada ya uchaguzi wa Jumuiya ya Wazazi, ulifuata mwingine wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT), uliofanyika Novemba 28, ambapo Mary Chatanda aliibuka na ushindi wa kishindo.

Chatanda anachuana vikali na aliyekuwa mwenyekiti wa umoja huo, Dk. Gaudentia Kabaka, lakini akafanikiwa kupindua meza kwa kujizolea kura 527, huku Dk. Kabaka akishindwa kutetea nafasi hiyo na kuambulia kura 219.



Job Ndugai

MWAKA 2022 UNAPOYOYOMA

# Vita Urusi, Ukraine, kifo Malkia Elizabeth mambo yaliyoutikisa

## •Ni kipindi mapinduzi yalizizima upya Afrika



Ndivyo ilivyokuwa siku ya mazishi ya kitaifa ya  Malkia Elizabeth jijini London. **PICHA: BBC**

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI mwaka 2022 ukielekea ukingoni, yapo matukio kadhaa yakukumbukwa, ambayo yameacha alama na yataendelea kubaki kwenye kumbukumbu ya nyanja ya kisiasa kwa miongo kadhaa.

Zipo nchi ambazo zilishuhudiwa kutokea mapinduzi ya kijeshi hasa ukanda wa Afrika Magharibi, uchaguzi mkuu Kenya na Angola, huku medani za kimataifa kifo cha Malkia Elizabeth wa Uingereza kikiweka rekodi ya tukio lililoshuhudiwa zaidi kwenye vyombo vya habari duniani.

Barani Afrika minyonyoro ya mapinduzi haikukatika bado majenerali wanaendelea kutumia mtutu kujipa madaraka kisiasa. Shoo inaanza na Luteni Kanali Paul-Henri Damiba.

Akitumia silaha Januari, mwaka huu, kuiingia madarakani nchini Burkina Faso naye akang'olewa kwa bunduki miezi michache tangu ashikilie madaraka ya kuongoza nchi hiyo.

Anaanza kumwondoa Rais Roch Chrisitian Kabore, aliyekuwa mamlakani, huku wachambuzi wa siasa za kimataifa wakisema milio ya risasi ikisikika ujue 'kimenuka' ikulu.

Na ndivyo ilivyokwa kabla ya mapinduzi kumwondoa Kabore, milio ya risasi ilirindima Januari, mwaka huu, ikisikika usiku kucha karibu na ikulu na kwenye kambi ya jeshi katika mji mkuu wa nchi hiyo, Ouagadougou.

Oktoba, mwaka huu ikawa zamu yake Luteni Damiba, baada ya Kapteni Ibrahim Traore wa Jeshi la Burkina Faso, kutangaza katika televisheni ya taifa, amempindua kiongozi huyo wa kijeshi.

Kapteni Traore, anaeleza sababu ya kuidhinisha mapinduzi hayo kuwa ni kutokana na kushindwa kwa Luteni Damiba kukabiliana na waasi.

### GUINEA-BISSAU

Pia Rais wa Guinea-Bissau, Umaro Sissoco Embalo, 2022 haikumwacha salama licha ya kutangaza kunusurika katika jaribio la mapinduzi ambalo lilisababisha vifo vya watu wengi na kusema kwa sasa hali imedhibitiwa.

Anawaambia waandishi wa habari kwamba alikabiliwa na milio ya risasi na silaha nzito kwa takriban saa tano, akiwa na mshauri wa kijeshi, waziri na walinzi wawili katika mji mkuu, Bissau, wakati wa njama ya kumuua na baraza zima la mawaziri, ikipangwa na jeshi hilo.

Rais Emballo anasema washambuliaji wangeweza kuzungumza naye kabla ya matukio hayo ya umwagaji damu ambayo yamesababisha vifo na majeruhi kadhaa.

Guinea-Bissau inayokabiliwa na mapinduzi inachafuliwa na vitendo vya rushwa na magendo ya dawa ya kulevya na rais aligusia hilo bila kuwataja waliojaribu kuipindua serikali yake.

### UCHAGUZI KENYA

Ni kinyang'anyiro kilichomhusisha mgombea wa Azimio la Umoja na William Ruto na Baba Raila Odinga.

Baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika Agosti 9, nchini Kenya na matokeo kutangazwa, Ruto alishinda lakini Raila aliyapinga mahakamani akikataa ushindi wa mpinzani wake.

Hata hivyo, mwezi mmoja tangu mahakama ya juu, iingilie kati, Ruto akatangazwa kuwa Rais mteule wa tano wa Kenya, baada ya ushindi wake kuthibitishwa na Mahakama ya Juu.

Uamuzi huo wa pamoja, ni kutoka kwa majaji saba, akiwamo, Martha Koome, Philomena Mwilu; Mohammed Ibrahim; Smokin Wanjala, Njoki Ndung'u; Isaack Lenaola na William Ouko, wakisema Raila Odinga na walioopinga matokeo walishindwa kuthibitisha madai dhidi ya ushindi wa Ruto.

Licha ya kuungwa mkono na Rais aliyekuwa anamaliza muhula wake Uhuru Kenyatta, matokeo ya uchaguzi huo uliosimamiwa na Tume ya Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), chini ya Mwenyekiti Wafula Chebukati, Odinga aliangukia pua na sasa Ruto ni Rais, baada ya kula kiapo Septemba 13.

### ANGOLA

Agosti 24 uchaguzi mkuu unafanyika Angola, na matokeo yakatangazwa Agosti 29, na kutangaza Movement for the Liberation of Angola (MPLA), kuwa mshindi kwa kupata asilimia 51.17 ya kura na kumpata Rais Joao Lourenco muhula wa pili, upinzani ukakataa matokeo.

MPLA, kimekuwa chama pekee kinachotawala nchi hiyo tangu ilipojinyakulia uhuru kutoka kwa Ureno mwaka 1975, lakini kimekuwa na matokeo mabaya zaidi ya kura za mwaka huu, chini ya ushindi wake wa asilimia 61 kwenye chaguzi zilizotangulia.

### VITA URUSI Vs UKRAINE

Nchini Urusi baada ya Rais Vladimir Putin, kuidhinisha jeshi la nchi hiyo kuivamia Ukraine katika operesheni maalumu, Februari 24, vita vilianza na kushuhudiwa idadi kubwa ya wakimbizi wakielekea nchi jirani.

Waziri wa Mambo ya Nje Russia, Sergei Lavrov, anasema licha ya operesheni hiyo kuanza, Rais Putin haweza kukataa wito wa kuzungumza na mwenzake wa Ukraine Volodymyr Zelenskiy kujadili masuala anayoyaita ni muhimu.

"Hatupangi kuishambulia nchi zingine mbali na Ukraine," Lavrov anaahidi.

Baada ya kuanza kwa vita hivyo, Zanzibar ilijikuta ina watalii kutoka Ukraine takribani 1,000 wakiwa hawajui hatima yao ya kuwa ugenini baadaye wakaamua kuendelea kuishi Zanzibar.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki, Mevlut Cavusoglu, ambaye alishiriki mazungumzo ya amani baina ya Urusi na Ukraine anasema, lengo la mkutano huo ni kuandaa mazungumzo kati ya marais wa mataifa hayo mawili ambayo yataongozwa na Rais wa Uturuki.

Umoja wa Mataifa (UN), unasema idadi ya wakimbizi kutokana na vita nchini Ukraine, imefika 2,000,000 huku nusu yake ikiwa ni watoto, aidha Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), likisema watoto 37 waliuawa Ukraine na 50 wakajeruhiwa.

Shirika la Kimataifa la Uhamiaji, (IOM) linabainisha kuwa watu milioni 2.3 walikimbia Ukraine kati yao 112,000 wanatoka nchi za dunia ya tatu.

Rais wa Senegal, Macky Sall, ambaye ni Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), akizungumza na Rais Putin, kutafuta usitishaji wa kudumu wa mapigano nchini Ukraine, anamweleza namna Afrika inavyoathirika zaidi kutokana na bidhaa kadhaa kama za chakula kukosekana na bei yake kupaa.

### BURIAN MALKIA

Malkia Elizabeth II wa Uingereza, amefariki dunia, Septemba 8, mwaka huu, akiwa na umri wa miaka 96. Anaacha kumbukumbu ya kuwa kiongozi aliyekaa kwenye ufalme kwa muda mrefu zaidi nchini humo na kuipitisha Uingereza katika nyakati ngumu na nyepesi kwenye kipindi chote cha utawala wake wa miaka 70.

Kilipotangazwa kifo chake, Malkia Elizabeth II kulikuwa na hisia tofauti mitandaoni yakiwamo mambo takribani 30 ya kipekee, yaliyomfanya awe wa pekee, kutoka mwonekano hadi maisha akitekeleza mambo mengi bila idhini wala kibali, ikiwamo kuendesha gari kwa spidi yeyote.

Pia inakadiriwa duniani kote watu bilioni 4.1 bilioni walishuhudia mazishi yake hususan kupitia televisheni. Kadhalika wageni mahsusi 2,000 wakiwamo viongozi 500 waliwasili Uingereza kwa maziko.

Pia ndiye pekee kwa miongoni kadhaa kutwaa mamlaka akiwa binti mdogo, miaka 25, alipokuwa kwenye ziara ya matembezini nchini Kenya, akiwa na mumewe, Prince Philip.

Historia ya kiti chake kwa miongo saba, ilianzia nchini Kenya, muda mfupi baada ya kupewa taarifa kutoka London, kwamba baba yake, Mfalme George VI amefariki dunia mwaka 1952 na kulazimika kurejea haraka nchini Uingereza, ili kutwaa mamlaka ya kifalme.

Wabunifu kadhaa walifanya kazi ya ubunifu kwa mavazi ya wa Malkia, akiwamo Sir Norman Bishop Hartnell, ambaye tangu mwaka 1940 alipata waranti ya kazi hiyo kwenye familia ya kifalme, huku mwaka 1957 akiwa rasmi ndiye mvalishaji mkuu wa Malkia Elizabeth II. Mbunifu huyu aliyezaliwa mwaka 1901 alifariki 1979.

# Migogoro wakulima, wafugaji janga linalohitaji kukoma sasa

**Na Sabato Kasika**



Baadhi ya wafugaji waliovamia Hifadhi ya Bonde la Mto Kilombero. **PICHA: MAKTABA**

MIGOGORO ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji imekuwa ikijirudia kila mwaka na kusababisha baadhi ya mali za watu kuharibiwa, kuumizana na hata wakati mwingine kuwapo kwa umawagaji damu.

Hayo yote yanatokana na kutokuwapo kwa maeneo maalum kwa ajili ya shughuli za ufugaji na kusababisha mifugo kuingia kwenye maeneo ya wakulima kitendo ambacho huzusha migogoro hiyo.

Wapo baadhi ya wakulima ambao wamewahi kufikia hatua ya kukata mifugo kwa mapanga, kama njia ya kulipiza kisasi baada ya wafugaji kuingiza mifugo hiyo katika mashamba ya wakulima na kusababisha uharibifu.

Wakati tunaelekea kuhitimisha mwaka 2022, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amekutana na viongozi wa serikali ya mkoani Morogoro katika kikao kilichotokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, yanayohusu kusimamia kwa karibu sekta ya mifugo, ili kutatua changamoto hizo.

Pamoja na mengi ambayo Waziri Mkuu aliongea katika kikao hicho, inasikitisha kusikia kuwa kumekuwapo na vitendo vya rushwa miongoni mwa viongozi ambao pia wamekuwa wakichochea migogoro hiyo.

Lakini akafafanua kuwa polisi wenyewe sasa hivi wameanza kudhibitiwa na wananchi na kwamba ikifikia hapo hiyo haina tija, chombo cha ulinzi na usalama kinadhibitiwa na raia.

Ninadhani inapofikia hapo, ina maana kuna jambo haliko sawa kama alivyosema Waziri Mkuu kuhusu rushwa miongoni mwa viongozi wanaopewa chochote na kuruhusu wafugaji kuingia katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Kwa mtindo huo, ni wazi migogoro ya ardhi inayosababisha uhasama kati ya wafugaji na wakulima haitakwisha, hivyo ingependekeza viongozi wanaoamini kuwa kauli ya Waziri Mkuu imewagusa, basi wabadilike.

Mwaka 2023 uwe ni wa kuanza ukurasa mpya wa kuelewana na kuishi kama ndugu, badala ya uhasana unaosababishwa na migogoro ya ardhi. Utashi wa kisiasa unaotumiwa na serikali upewe nafasi kumaliza migogoro hiyo.

Ikumbukwe kwamba, mikoa 11 ya Morogoro, Iringa, Pwani, Lindi, Arusha, Manyara, Kagera, Katavi, Tabora, Tanga na Mwanza inatajwa kuongoza katika migogoro hiyo. Ingependeza kama haitaongezeka.

Njia nzuri ya kuifanya mikoa isiongezeke au migogoro iishe kabisa, ni kila kiongozi kuwajibika kwa kusimamia haki, usalama na kutoa elimu kwa jamii ambayo kwa sasa imekuwa na roho ya kikatili.

Kwa mujibu wa ripoti ya Global Peace Index (GPI) inayotolewa na taasisi ya uchumi na amani (IEP) yenye makao yake makuu mjini Sydney nchini Australia, Tanzania inaongoza kwa amani Afrika Mashariki.

Tanzania imeshika nafasi ya saba 7 kwa kuwa nchi yenye amani kwa nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara na duniani, ikiwa imeshuka kutoka nafasi ya 51 mwaka 2018 hadi nafasi ya 54 mwaka 2019 kati ya nchi 163.

Ni vyema amani hiyo isivurugwe na watu wachache wanaopenda rushwa na kusababisha wakulima na wafugaji ambao kwa miaka mingi wamekuwa wakiishi pamoja bila ugomvi hado miaka ya hivi karibuni.

Kimsingi, mkuu wa nchi anapoonyesha kutoridhishwa na maeneo fulani, ni wajibu wa viongozi au wasaidizi wake kuweka mipango ambayo itasaidia kudhibiti viashiria vyote vya uvunjifu wa amani kati ya makundi hayo mawili.

> “Ninadhani inapofikia hapo, ina maana kuna jambo haliko sawa kama alivyosema Waziri Mkuu kuhusu rushwa miongoni mwa viongozi wanaopewa chochote na kuruhusu wafugaji kuingia...

Leo migogoro ya ardhi inatajwa kushamiri kwenye mikoa 11, lakini ninaamini kuwa inaweza kupanuka hadi mikoa mingine iwapo hakutakuwa na mipango madhubuti ya kudhibiti viashiria hivyo mapema.

Kauli ya Waziri Mkuu itoshe kuwashtua viongozi ambao wanatajwa kujihusisha na rushwa na kuruhusu mifugo kuingia katika maeneo ambayo hairuhusiwi kuingia au kuvamia mashamba ya wakulima.

**MAAGIZO YA RAIS**

Katika hotuba yake baada ya kulifungua rasmi geti la handaki lililojengwa kuchepusha maji, ili kupisha ujenzi wa bwawa la Nyerere lililoko Rufiji mkoani Pwani, aliagiza kushughulikiwa kwa familia 12 za viongozi waliovamia na kuchepusha maji Bonde la Ihefu.

Rais Samia aliwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuondoa mifugo yote iliyoingizwa katika Bonde la Ihefu kinyume na utaratibu na kwamba ile itakayohamia maeneo ya vijiji katika bonde hilo, uwezo wa vijiji utaangaliwa.

Rais Samia pia aliagiza kwamba, wanaposhughulikia migogoro hiyo, wakafanye kazi zao kwa mujibu sheria kwa kuzingatia weledi na haki za binadamu.

“Tuna uzoefu wa mapigano ya wakulima na wafugaji hasa mkoani Morogoro na katika wilaya moja nadhani Kilosa mkuu wa wilaya alipoulizwa kwa nini wako wengi wanakufa kutokana na haya mapigano jibu lake ng'ombe wengi ni wa wakubwa nashindwa kuwagusa sasa niwaambie hakuna mkubwa atakayetuharibia mradi huu,” Rais.

Rais anaagiza wakuu wa wilaya na mkoa wakafanye kazi na kwamba watakaoogopa wakubwa waseme washughulikiwe. Wale wanaochepusha maji wazuiwe Mto Rufiji ili maji yapite mkondo wake wa asili.

# 2022 ni vilio, mayowe Congo, balaa wakimbizi kila kona

## •Swali gumu, mbona M23 wanazidi kuwa jeuri?



Mamia ya Wakongo wakikimbia mapigano kati ya vikosi vya serikali na waasi wa M-23 huko Goma, mwezi uliopita. **PICHA ZOTE: AP**

**Na Gaudensia Mngumi**

ZIKIWA zimesalia siku tatu kuanza mwaka mpya wa 2023 , njaa na kipindupindu vinawakabili maelfu ya Wakongo waliokimbia mashambulizi ya waasi wa M23 huko Kivu Kaskazini.

Hali ni mbaya wakimbizi maelfu waliowakimbia waasi wa M23 walioteka maeneo mengi katika miezi ya hivi karibuni, wanalala mashambani, juu ya mawe ya lava iliyokauka baada ya volkano kulipuka miaka ya nyuma kwenye milima ya Nyiragongo karibu na Goma.

Wachache wenye bahati wanalala kwenye sakafu za shule na makanisa, lakini wengi wanalala ndani ya vibanda vya maturubai. Njaa imekithiri na hali duni ya usafi imesababisha mlipuko wa kasi wa kipindupindu.

"Siwezi kusherehekea Krismasi sina chakula," anasema Olive Pandezi (35), akiwa na rozari mkononi huko Kanyaruchinya, eneo la mlima karibu na Goma lililojaa watu waliohamishwa. Ni kwa mujibu wa Al Jazeera.

Mambo ni magumu licha ya kwamba mwaka huu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) imejiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ili pamoja na mambo mengine, kuwepo na utatuzi wa pamoja wa mgogoro wa kivita baina ya waasi wenye silaha wa M23 na Jeshi la Kongo (FARDC).

Mwaka mzima wa kuwa mwanachama wa EAC, vita inaendelea katika jimbo la Kivu Kaskazini na mapigano hayo yamesababisha watu wengi kuhama makazi yao huku takriban raia 262,000 wakikimbia makazi yao tangu Machi mwaka huu muda mfupi baada ya kuwa mwanachama, wakati mapigano yalipoanza. Unasema Mtandao wa the UN Office for the Coordination of Humanitarian Affairs -OCHA.

Tatizo kubwa ni vita inayochochewa na waasi hao, inayoleta shida kwani ulinzi wa raia ni kazi ngumu na inakadiriwa kuwa watoto 20,000 wanahitaji msaada wa ulinzi haraka, ambao haufahamiki utawafikia.

Ingawa kufikia utatuzi wa misaada ya kibinadamu mashirika yanaendelea kutoa misaada kwa watu walioathiriwa na migogoro na waliokimbia makazi yao, likiwamo la Mpango wa Chakula Duniani WFP lililowasilisha mgao wa chakula kwa siku 15 kwa takriban raia 82,000 waliokimbia makazi yao katika eneo la Nyiragongo, inasema OCHA.

Ili kuwadhibiti waasi na kuinusu DRC zinahitajika dola milioni 76.3 na kwa sasa ufadhili umepatikana kwa asilimia 42, kwa mujibu wa shirika hilo.

Kivu Kaskazini, kama majimbo mengine Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), inakabiliwa na ongezeko kubwa la mashambulizi yanayolenga raia kutoka kwa makundi yenye silaha.

Hadi mwaka una malizika kuna zaidi ya wakimbizi wa ndani milioni 1.6 (IDPs) katika Kivu Kaskazini na taifa hilo lina karibu IDPs milioni 5.7 kwa jumla nchini DRC, inaongeza.

Aidha, zaidi ya Wakongo 8,000 wameomba hifadhi ya ukimbizi katika nchi jirani ya Uganda tangu mwisho wa Oktoba. Mtiririko huo unaendelea na unaonyesha kuwa, kinachoendelea DRC ni jambo la kutafakariwa upya mwakani na kupata ufumbuzi.

**NANI MFADHILI M23**

Hata sasa mwaka unavyomalizika mfadhili wa M23 anadaiwa kuwa ni Rwanda nayo inakanusha. Lakini swali la kujiuliza linabakia kuwa wanapata wapi silaha nzito na vifaa vya kijeshi vya kisasa, fedha za kuendesha mapigano, mavazi na mishahara ya askari hao.

Wiki iliyopita Ufaransa imelaani waziwazi kile inachokiita kuunga mkono kwa Rwanda. Waasi wa M23 wanaopigana Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ambao wanadhaniwa kuua takriban raia 131 mwishoni mwa Novemba, inasema Redio ya Ufaransa RFI.

Taarifa ya Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa Anne-Claire Legendre anasema: "Tunalaani uungaji mkono wa Rwanda kwa kundi la M23 na tunaomba mchakato wa kufikia amani wa Rwanda na Nairobi utekelezwe kikamilifu."

RFI inaongeza kuwa vuguvugu la Machi 23 au M23 ni uasi wa Watutsi ulioasisiwa mwaka 2012 ambao walichukua silaha kwa mara nyingine tena mwishoni mwa mwaka jana na kuweka kambi kwenye maeneo makubwa ya Kaskazini mwa Goma, mji mkuu wa mkoa wa Kivu Kaskazini Mashariki mwa DRC na kusababisha vita visivyoisha.

Aidha, ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyotolewa wiki iliyopita RFI, inasema: Waasi wa M23 waliua takriban raia 131 ikiwa ni pamoja na wanawake 17 na watoto 12, mauaji yaliyofanyika Novemba, ambayo watu walipigwa risasi kiholela au kuuawa kwa kuchomwa visu katika vijiji viwili mashariki mwa DRC.

Viongozi wa Kongo, wataalam wa Umoja wa Mataifa, na wanadiplomasia wa Marekani wanasema vuguvugu la M23 linaungwa mkono na Rwanda, lakini Rais wa Rwanda Paul Kagame, anakataa uhusiano wowote na kundi hilo.

Akizungumza hivi karibuni Kagame anasema: "Tatizo hilo halikutengenezwa na Rwanda, na si tatizo la Rwanda, ni shida ya Wakongo wenyewe."

Rwanda pia, imeondolewa katika kikosi cha kulinda amani cha kikanda, ambapo Burundi na Kenya tayari zimetuma wanajeshi wakati Uganda iko mbioni kutuma vikosi.

**MSIMAMO WA M23**

Kwa mara nyingine kundi la waasi la M23 limeendeleza mchezo wa kombolela wa 'kujificha' na 'kuibuka' kushambulia katika mkakati uliowawezesha kuteka maeneo mengi Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, wameahidi kujiondoa kwenye maeneo waliyoyateka, ni kwa mujibu wa Al Jazeera.

Katika taarifa yao siku ya Ijumaa iliyopita, waasi hao walitangaza kwamba, watajiondoa kwenye ngoma mji wa Kibumba ulioko takriban kilomita 20 kutoka Goma, kitovu cha kibiashara cha zaidi ya watu 1,000,000 ambao M23 waliuteka kwa muda, wakati wa mkutano wao mkuu wa kwanza, uasi ulipoanza mwaka 2012.



Wanajeshi wa Kenya na Kongo wakilinda Uwanja wa Ndege wa Goma, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kabla ya ujio wa msuluhishi Rais wa zamani wa Kenya, Uhuru Kenyatta.

# Uingereza ilivyobadili viongozi kama 'mswaki'

## •Johnson, Liz Truss wakionyeshwa mlango



Boris Johnson aling'oka Julai 2022.



Liz Truss alikaa madarakani siku 44 pekee



Rishi Sunak Waziri Mkuu wa Uingereza, aliyeanza kazi Oktoba mwaka huu.
**PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

Ni mwaka wa Uingereza, unaweza kusema. Ni katika kipindi cha mwaka mmoja imebadilisha viongozi - mawaziri wakuu watatu na kujikuta ikihangaika bila kujua wapi inapoelekea.

Ilikuwa 'Sabasaba' au Julai 7, 2022, 'Waziri Mkuu wa Uingereza aliyezozaniwa Boris Johnson, anapotangaza kujiuzulu rasmi wadhifa huo na kumaliza mgogoro wa kisiasa usio wa kawaida juu ya mustakabali wake.

Muda mfupi baada ya kujiuzulu uongozi wa chama chake cha Conservative, unagongomelea msumari unashindiliwa kwa kutaka kuwe na mabadiliko yanayofaa ya serikali na mchakato mwingine unaanza.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Johnson anajiuzulu kama kiongozi wa Chama cha Conservative baada ya kupoteza uungwaji mkono na mawaziri na wabunge wake ambao walimchukulia kama mtu mdanganyifu na asiyemaanisha mambo aliyokuwa akiyazungumzia.

Julai 2019, Johnson alichukua rasmi mikoba ya Theresa May, Waziri Mkuu aliyejiuzulu baada ya kutokea uasi ndani ya baraza lake la mawaziri na kupingwa na karibu kila mtu.

Waziri Mkuu huyo mstaafu alikuwa Meya wa zamani wa Jiji la London aliyekuwa anahamasisha Brexit, au Uingereza kujitoa kwenye Umoja wa Ulaya na kuhakikisha kuwa inapigwa kura ya maoni ili kuifahamu hatima ya taifa hilo na hilo lilifanikiwa na Uingereza kujiondoa EU.

Hata hivyo ilipotimia miaka minne Julai 22, Johnson alimwachia kijiti Liss Truss ambaye naye aliongoza nchi kwa takribani mwezi mmoja na wiki mbili na kuwekwa pembeni.

Elizabeth au Liz Truss ni Waziri Mkuu aliyehudumu kwa muda mfupi zaidi Uingereza pengine na duniani. Akishika nafasi hiyo siku 44.

Kwa mujibu wa BBC Truss - ambaye aliingia madarakani siku 44 anakuwa Waziri Mkuu aliyeongoza kwa muda mfupi zaidi katika historia ya Uingereza. Uongozi wa Chama cha Conservative unaitisha uchaguzi mara moja kufuatia hotuba ya Truss ya kujiuzulu.

Katika hotuba yake, Truss anasema aliingia "ofisini wakati wa machafuko makubwa ya kiuchumi na kimataifa", huku vita vikiendelea nchini Ukraine na gharama za maisha zikiongezeka.

Septemba 5, 2022 ndiyo siku alipopata nafasi ya kuiongoza Uingereza baada ya kushinda uongozi wa Chama cha Conservative na kumwondoa Boris Johnson, aliyekuwa anakabiliwa na tuhuma za kufanya misururu ya karamu wakati wa karantini ya COVID-19 nchini humo na kulidanganya bunge.

Septemba 8, siku chache baada ya Lizz kuchukua nchi Malkia wa Uingereza Elizabeth wa II, anaaga dunia.

Oktoba 20 Liss Truss anajiuzulu baada ya kutumikia ofisi yake kwa siku 44. Ukielezwa kuwa ni muda mfupi kuliko kampeni za uongozi alizofanya kumrithi, Johnson.

Liz Truss, ambaye amekuwa madarakani kwa muda mfupi zaidi alidaiwa kuwa 'mharibifu zaidi' kwa mpango wake wa kupunguza kodi kwa matajiri. Waingereza walikabiliwa na hali ngumu kuanzia mfumuko wa bei kwa asilimia 10 ukiwa ni wa juu zaidi katika kundi la nchi tajiri duniani G7 na wa juu zaidi kwa miaka 40, uliopunguza nguvu zao za ununuzi wa bidhaa na Pauni kudhoofika.

NI RISHI SUNAK

Kijiti cha uongozi kwa kipindi cha mwaka mmoja kikamwangukia tena Rishi Sunak, ambaye sasa ni Waziri Mkuu wa 57 wa Uingereza baada ya kualikwa kuunda serikali na Mfalme Charles, anayekalia kiti cha ufalme baada ya kifo cha mama yake Elizabeth wa II.

Oktoba 25, 2022 ndiyo siku Sunak anapotangazwa kuwa ni Waziri Mkuu wa tatu wa Uingereza kwa mwaka huu.

Aidha, anatajwa kuwa anakuwa Waziri Mkuu mdogo zaidi katika karne mbili, aliyewahi kuiongoza Uingereza .

Katika kinyang'anyiro cha kwanza Sunak anaelezwa kuwa alishindwa kuwashawishi wajumbe kumchagua kuwa kiongozi wa Conservative, badala yake walimpigia kura Liz Truss kuwa Waziri Mkuu mnamo Septemba na pia kiongozi wa chama hicho.

**MAMBO MAGUMU**

Sunak analazimika kufanya mambo magumu kama kupunguza matumizi ya umma, kuangalia upya kodi ili kuleta fedha mpya katika hazina ya serikali inayokabiliwa na gharama ya deni lake ambalo limekuwa kubwa. Kutatua tatizo la shida ya nishati. Rishi Sunak, Kansela wa zamani wa Hazina, anaelezwa kuwa anafaa kwa kazi hiyo.

Matatizo ya sasa ya uchumi wa Uingereza yanahusiana na Brexit? Ni swali linaloulizwa. Inawezekana kwa kiasi fulani mambo yanatiwa chumvi na janga la CORONA-19 , tatizo la nishati linaongezeka mara 10 zaidi na kibaya zaidi ni vita vya Ukraine na Urusi ambao ni chanzo chakushuka kwa uchumi wa dunia ikiwamo Uingereza.

Aidha, kitisho cha athari za mabadiliko ya tabianchi nacho hakiwezi kuwekwa pembeni kwenye nishati na pia kusimama yenyewe kama uyoga bila kuwa na wadau wengine wa Ulaya.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba yote hayo yanaikuta Uingereza katika mshtuko uliotokana na kudhoofishwa na Brexit. Kuondoka kwa Uingereza katika Umoja wa Ulaya kumezidisha uhaba wa wafanyakazi, uhaba wa vitu na ugumu wa biashara kutokana na ongezeko la gharama na kodi.

# 2022 ni mwaka wa wamachinga biashara zao mijini bado kitendawili

INATOKA UK. 13

kama ilivyo sasa kwa yale ambayo 'yamesafishwa' mwaka huu unaomalizika. Zoezi hilo ingebidi liishie hapo.

Viongozi wanadai kukwazwa na hali hiyo kwani hawalipi kodi, hawachangii maendeleo na hilo kwao ni kosa kubwa. Kwa kuwa ustawi wao na kufaulu kimaisha na familia zao, jambo hilo haliko ndani yao, hawalifahamu, wanajua kodi peke yake. Kumbe ziko njia tofauti za kulipa kodi, kwani mtu huyo anayeuza vitu kando ya mtaro wa kupitisha maji machafu akipata Shilingi 5,000 akanunua kilo moja ya mchele na kilo moja ya unga atakuwa amelipa kodi mara mbili, akijaza vocha analipa kodi, hata akipanda daladala anachangia shughuli inayoleta kodi. Kimsingi hakuna asiyelipa kodi, ila zinatofautiana; za moja kwa moja zinazolenga waajiriwa au wafanyabiashara wenye maskani ya biashara yenye anuani sahihi, na zile za kupitia bidhaa. Hivyo, hoja ya kutolipa kodi ina ugumu kuielezea.

Ukiangalia mtiririko wa hulka serikali kuu na za mitaa kwa mujibu wa tafiti mbalimbali katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea, kilicho wazi ni kuwa serikali kuu ina uwezo zaidi wa hulka ya kuchunga au kulea watu wa tabaka la chini waweze kumudu maisha. Wale wa serikali za mitaa muda wote wanaona maeneo hayo kama mawindo, hivyo kuna wakati walikuwa wanawanyang'anya kinamama hata masufuria na kuondoka na chakula hicho huku wakiwaacha wanapiga mayowe.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwa kwenye soko la wamachinga la Mbauda jijini Arusha.
**PICHA: MAKTABA**

Ni moja ya sababu ambazo zilimwezesha kiongozi mkuu wa awamu ya tano kuwa mkombozi, kwa kulazimisha hulka ya kuwalea. Ila wanapotakiwa wahamie katika masoko, kuwasukumia EFD ni kama kwenda kinyume na utaratibu wa kuwalea na kujali ustawi.

Mara kadhaa, mamlaka za usimamizi au uendeshaji wa sekta fulani hasa pale wadau kadhaa wanapolitaka jambo hilo, wanatunga sera ambazo zinapingana na azma ya utawala. Wanatangaza dhamira kama kujaribisha hali ya hewa na hata kujiandaa kikamilifu kutekeleza suala husika, hadi vyombo vya dola vipate hisia kuwa jambo hilo linawachukiza watu na kuondoa imani au 'bashasha' kwa viongozi miongoni mwa watu wa kawaida.

Moja kati ya hatua kama hizo ilikuwa ni tangazo kuwa maduka ya dawa yasiwapo karibu na hospitali, muhimu yakae umbali wa mita 500 kutoka hospitali ili kuzuia wizi wa dawa. Ukiangalia hapo hakuna mantiki, halafu ukiuliza unaambiwa kuwa dawa ni ghali zaidi katika dirisha hospitalini kuliko dukani mtaani, ndiyo unapata picha kuwa kuna ushindani wa kuuza dawa ambako za wizara au maofisa huko zinadoda, za dukani zinanunuliwa kwanza.

Ukiangalia baadhi ya taarifa za serikali za mitaa kwa mujibu wa ripoti ya kila mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu (CAG), mara nyingi ziko fedha nyingi zinazokusanywa halafu hazipelekwi benki. Kwa kuwa, wafanyabiashara hawana anwani na matazamio ya ulipaji kodi yanayoeleweka. Hivyo, kulazimisha EFD zitumike hakutakuwa na tija.

> Ni moja ya sababu ambazo zilimwezesha kiongozi mkuu wa awamu ya tano kuwa mkombozi, kwa kulazimisha hulka ya kuwalea. Ila wanapotakiwa wahamie katika masoko, kuwasukumia EFD ni kama kwenda kinyume na utaratibu wa kuwalea na kujali ustawi.

## CHEMSHABONGO NA -00 37 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. kinyume cha kaka
5. Baba
7. shughuli ya kusafirisha watu
8. ikiwa, endapo
10.jimbo kubwa Marekani
12.kadiria
13.Ottawa ni mji wake mkuu
14.Ubinadamu
16.mwanzo au asili ya kitu

Chini:
1. Supamaketi
2. zao la nyuki
3. mji mkuu wa Syria
4. afezia
5. fungu
6. kifupi cha neno Bibi
9. magonjwa
11.nyumba ya ibada
15.hutoa nuru

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | ■ | 5 | 6 | |
| 7 | | | | | | | ■ |
| 8 | | | | ■ | | ■ | 9 |
| 10 | | | | 11 | | ■ | |
| 12 | | | | | ■ | ■ | |
| | ■ | 13 | | | | | |
| 14 | 15 | | ■ | | ■ | ■ | |
| ■ | 16 | | | | | ■ | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ | ■ | |

Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

KABULI
UKALILI
KIBALI
ULAFI
IWAPO
AGWA, BALAA
SHAUA, BIA
KUKU, AKILI
BABA, ULAFI
LILIWALA, ILI
NDOA, IBA, AGA
PWANI, KASA
AUA, BIA

maoni SMS: 0787 00 97 94

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | ■ | ■ |
| | | | | | | | ■ |
| | | | | | | ■ | N |
| | | | | | ■ | ■ | D |
| ■ | | ■ | | | | | O |
| | ■ | | ■ | | | | A |
| | ■ | | | | | | ■ |
| | | | | | ■ | | ■ |
| | ■ | ■ | | ■ | | | |

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | U | M | U | ■ | M | B | U |
| O | B | A | M | A | ■ | ■ | G |
| K | A | M | A | T | I | ■ | U |
| A | Y | A | ■ | I | N | D | A |
| ■ | A | L | M | A | S | I | ■ |
| A | ■ | I | ■ | ■ | H | A | U |
| D | U | A | ■ | M | A | N | A |
| H | ■ | ■ | ■ | J | ■ | A | ■ |
| A | B | I | R | I | A | ■ | ■ |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | W | A | N | Z | A | ■ | K |
| O | ■ | M | ■ | A | D | H | A |
| T | A | B | A | K | A | ■ | M |
| A | F | I | S | A | ■ | ■ | B |
| ■ | Y | A | I | ■ | U | Z | A |
| ■ | A | ■ | L | U | L | U | ■ |
| J | ■ | K | I | L | E | L | E |
| U | J | I | ■ | N | Z | I | ■ |
| A | ■ | U | R | A | I | A | ■ |



# Polisi yaanza kupima madereva kilevi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya, limeanza operesheni ya kupima viwango vya ulevi madereva wote wa vyombo vya moto ili kuwadhibiti na kuwachukulia hatua za kisheria kwa wale watakaobainika ili kuepukana na ajali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP), Benjamin Kuzaga, alisema hayo jana alipozungumza na Nipashe juu ya mikakati ya polisi katika kukabaliana na ajali msimu huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Alisema miongoni mwa hatua walizoanza kuchukua ni kuweka askari wa kutoka katika vizuizi na maeneo mengine ili kupima madereva wote kujua viwango vya ulevi wa pombe. Alisema watakaobainika watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

"Unapofika mwisho wa mwaka, baadhi ya madereva wanajisahau sana. Wengine wanakunywa pombe kupindukia na kuendesha vyombo vya moto jambo ambalo ni hatari sana kwa usalama wao na watu wengine.

"Hatua hii ya kuwapima viwango vya ulevi itasaidia kuwa na nidhamu kidogo maana polisi wametawanyika kila eneo hapa mkoani Mbeya. Ukibainika umekunywa pombe, gari linachukuliwa na wewe mwenyewe unaenda kutoa maelezo kwenye vyombo vya sheria," alisema Kuzaga.

Aliongeza kuwa polisi wa kikosi cha usalama barabarani watasimamia maeneo yote ya vivuko barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) na kuhakikisha madereva wanawaruhusu watu kuvuka.

Tumeweka askari wetu kwenye vivuko vyote vya barabara kuu jukumu lao ni kuruhusu magari kupita au watembea kwa miguu kuvuka ambapo kumeandaliwa utaratibu maalum," alisema ACP Kuzaga.

Baadhi ya watembea kwa miguu wamesema kwa sasa wanapata kero kubwa wanapohitaji kuvuka barabara kutokana na madereva wengi kutowaruhusu kuvuka kwa wakati, hali inayosababisha msongamano wa watu.

Betwel Asukukile, Mkazi wa Esso jijini Mbeya, alisema hatua ya Jeshi la Polisi kuwa kwenye vivuko itasaidia madereva kuwaheshimu watembea kwa miguu wakiwamo watu wenye mahitaji maalum.

# Baba na mtoto wafa katika ajali ya gari

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

WATU watatu wa familia moja ambao ni mmiliki wa Shule ya Msingi ya Mtwara Heritage, Ipyana Kyomo (59) na mwanawe Irene Kyomo (14) na mtumishi wa nyumbani Christina Lucas (20), wamefariki dunia papo hapo katika ajali ya gari.

Ajali hiyo iliyotokea eneo la Ntokela, Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, pia imesababisha watu wengine wanne kujeruhiwa baada ya gari dogo walilokuwa wakisafiria kuangukiwa na lori lililokuwa limebeba mafuta aina ya dizeli.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Benjamin Kuzaga, alisema jana kuwa ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 07:30 mchana katika barabara kuu ya Mbeya-Kyela.

Alisema gari lenye namba za usajili T 745 DPZ/T.258 DRJ aina ya Faw Tank, lililokuwa limepakia mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Malawi, likiendeshwa na Jimmy Benasusi (51) Mkazi wa Tabata, liliangukia gari dogo namba T 103 DPZ Toyota Vanguard, lililokuwa linatoka Kyela kwenda Mtwara, ikiendeshwa na Kyomo na kusababisha vifo dereva huyo (Kyomo), mwanawe Irene, mwanafunzi wa kidato cha pili na Christina, mtumishi wa nyumbani.

Kamanda Kuzaga aliwataja waliojeruhiwa katika ajali hiyo kuwa ni Eunice Nyiti (51) mwalimu mkoani Mtwara, Idrisa Mwende (30) fundi magari, Vanesta Amasha (12) na Elizabeth Mrope, rafiki wa familia ya Kyomo mkoani Mtwara.

"Waliopata ajali ni familia moja na rafiki yao mmoja. Majeruhi watatu wamepelekwa Hospitali ya Misheni Igogwe kwa matibabu na miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe ya Makandana iliyoko mjini Tukuyu," alisema ACP Kuzaga.

Alifafanua kuwa chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa lori kuendesha gari kwa mwendokasi huku akiwa amelewa. Alisema hatua za awali zimefanyika ikiwamo kumpima kiwango cha ulevi na kukutwa na milligram 216 za ulevi.

Tayari taratibu za mazishi ya Ipyana Kyomo, mwanawe Irene zimeanza kufanyika katika eneo la Forest Mpya jijini Mbeya.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Injinia Rogatius Mativila (kulia), akitia saini mkataba wa ujenzi wa barabara tatu zinazounganisha barabara kuu na Bandari ya Ziwa Nyasa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Prime System Group ya nchini Uturuki, Mhandisi Umit Pal. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Kanisa TAG lakemea ndoa za jinsia moja

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KANISA la Tanzania Assemblies of God (TAG) Jerusalem Temple, Soko Matola jijini Mbeya, limekemea ndoa za jinsia moja ambazo zimeanza kushamiri nchini.

Kutokana na hali hiyo, kanisa hilo limeiomba serikali kutokukubali misaada inayotolewa kwa sharti la kuruhusu ndoa za aina hiyo ili kuendana na matakwa ya Mwenyezi Mungu.

Askofu wa Kanisa hilo, Adson Mwajunga, alitoa kauli hiyo kwenye Ibada ya Sikukuu ya Krismasi iliyofanyika Jumapili iliyopita.

Mwajunga alisema kuruhusu ndoa ya jinsia moja ni upotevu mbele za Mungu na kuishauri serikali kutokuruhusu misaada inayotolewa ambayo ina mlengo wa kuruhusu ndoa za namna hiyo huku akisisitiza kuwa hakuna maandiko matakatifu ambayo yanaruhusu ndoa hizo.

"Naiomba serikali yetu na viongozi wetu, wasikubali kupokea misaada ambayo itakuwa na masharti ya kuruhusu ushoga nchini kwetu. Ni bora tukafa na umaskini wetu kuliko kuruhusu hizo ndoa," alisema Mwajunga.

Alisema maandiko matakatifu, ikiwamo Biblia, yanatambua ndoa ya jinsia mbili tofauti kwa maana ya mwanamke na mwanamume na kwamba ndoa za jinsia moja si ndoa bali ni laana mbele ya Mwenyezi Mungu.

Roman Kessy, ambaye ni Mzee wa Kanisa hilo, alisema watu wote wanaojihusisha na ndoa ya jinsia moja siku zao za kuishi zinahesabika na kwamba kitendo wanachokifanya ni laana huku akitolea mfano wa Sodoma na Gomora.

"Mwenyezi Mungu haruhusu vitu vya aina hii na hawa wote wanaoshiriki hizi ndoa na kuruhusu ni wale ambao hawajamwona Mungu na Mungu anaweza kufanya lolote juu yao," alisema Kessy.

Naye Emma Mwabukusi, aliwataka wanawake kote nchini na duniani kote kukataa ndoa za jinsia moja na kukemea vikali huku akisema kufanya hivyo ni kupingana na agizo la Mungu na kuwaomba kuzaliwa upya na Kristo kwa kutubu dhambi zao.



# Bosi Mahakama asisitiza matumizi TEHAMA

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama, Prof. Elisante Ole Gabriel, amewataka watendaji kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuharakisha utekelezaji wa kesi bila upendeleo.

Prof. Ole Gabriel alisema hayo jana wakati akifungua mkutano wa maofisa TEHAMA kutoka mikoa mbalimbali nchini uliofanyika jijini hapo.

Alisema mifumo hiyo ikikaa vizuri itasaidia kupunguza upungufu uliojitokeza katika utendaji kwa mwaka wa mahakama uliopita.

"Naomba mboreshe mifumo yenu tunahitaji kuona TEHAMA inapewa nafasi katika utendaji kazi za mahakama za kila siku,"alisema Ole Gabriel.

Alisema siku hiyo ni muhimu kwa ajili kupeana baadhi ya mambo na hii ni heshima ya kipekee kabisa kwa sababu Mahakama inakwenda kubadilika katika matumizi ya TEHAMA.

"Mpango mkakati unatekelezwa vizuri na lazima tuwapongeze kwa kazi nzuri mnayoifanya kwa upande wa TEHAMA," alisema.

Aidha, aliwataka kuhakikisha wanaimarisha uwazi, uwajibikaji na matumizi ya TEHAMA ndiyo maana wamewaita ili kuelezana ukweli katika kuongeza wateja wa Mahakama ili dira iwe ni kufikiria kwa kasi kubwa zaidi.

"Msukumo tulio nao ni kwenda kwenye mfumo wa mtandao na hadi sasa asilimia 99 ya mashauri yanafunguliwa kwa njia ya mtandao ili kuwarahisishia wananchi upatikanaji wa huduma.

"Asilimia 70 ya mashauri yanatoka kwenye mahakama za mwanzo, hivyo wamulikeni ili kubaini changamoto na ziweze kutatuliwa.

Naibu Msajili Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Sylvia Lushasi, alisema hivi sasa kuna kituo cha huduma kwa wateja kinachofanya kazi saa 24 na kinaruhusu Watanzania wenye kero yoyote wapige simu na watahudumiwa.

"Pia tumefungua laini ya kupiga simu bure na tuna laini nyingine ya kushughulikia ndoa na mirathi pekee," alisema.

Mikakati iliyoko, alisema ni kuboresha miundombinu ya TEHAMA na matumizi ya mahakama mtandao, hivyo watawekeza zaidi kwenye eneo hilo.

"Kwa sasa tuko kwenye hatua za mwisho za majaribio ya matumizi ya mfumo wa akili bandia ambao utakuwa ukitafsiri mambo mbalimbali ya kuandika nakala za hukumu na hii haitaji mtu aje kuandika hukumu inaandika yenyewe. Tunawategemea zaidi ninyi maofisa TEHAMA," alisema.

Ili kufikia azma hiyo, aliwataka maofisa TEHAMA kubadilika kifikiria na kuendana na kasi ya utendaji wa mahakama na wasipobadilika wataachwa nyuma.



Mchuuzi wa nazi ambaye jina lake halikupatikana akiwahudumia wateja wake eneo la One way jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mkurugenzi asema wanafunzi wote watapata nafasi kidato cha kwanza

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, amewataka viongozi wa mitaa, kata, wazazi na walezi kuhakikisha wanashirikiana ili watoto wote waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza na wale walioandikishwa kuanza darasa la kwanza mwakani, waanze masomo kwa wakati.

Mafuru alisema hayo wakati akikabidhi madarasa 29 ya Shule ya Sekondari ya Ng'ong'ona jijini hapo kwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, yaliyojengwa na kusimamiwa na jiji kwa fedha za UVIKO-19 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan. Alisema viongozi hao kwa kushirikiana na wazazi na walezi wahakikishe watoto wote wapelekwe shuleni na kuanza masomo kwa kuwa madarasa yapo ya kutosha na hakuna sababu ya kuwaacha nyumbani.

Fedha zilizotolewa na serikali, alisema zimesaidia kutatua kero ambazo zilikuwapo kwenye sekta ya elimu, hivyo wazazi na walezi wanatakiwa kushirikiana kuhakikisha watoto wote wanaostahili kuanza masomo wasiachwe kwa visingizio vya uhaba wa madarasa.

"Rais wetu Samia Suluhu Hassan, ametatua tatizo ambalo kwa muda mrefu lilionekana kwa upande wa elimu kama ni changamoto ya kukosa madarasa ya kutosha kwa watoto wetu. Hivi sasa majengo karibu nchi nzima yamejengwa, hivyo hatuna sababu ya kuwaacha watoto wakizurura na kukaa majumbani," alisema.

Naye Shekimweri aliwataka madiwani, walimu wakuu, wakuu wa shule, maofisa elimu kata kuhakikisha wanawahamasisha wazazi na walezi wenye watoto wote waliofaulu hakuna anayebaki kwa vizingizio vya uhaba wa madarasa.

Shekimweri alisema hatarajii uhamasishaji wa kuwataka watoto hao kuanza masomo uanze baada ya kufungua shule, bali zoezi hilo la kuwahimiza wapelekwe mapema wanatakiwa kulianza hivi sasa kabla hawajafungua.

"Hakuna maana ya ujenzi wa madarasa ambao Rais wetu mpendwa ameamua fedha za UVIKO - 19 zitatue changamoto za elimu kwa kujenga majengo ya madarasa, halafu watoto wote waliofaulu wasipelekwe kusoma. Hii kwa kweli haiwezekani hata kidogo.

"Viongozi wote kwa pamoja na wazazi na walezi tunatakiwa kumuunga mkono Rais kutokana na jitihada zake za kuhakikisha taifa linawapata wasomi watakaoitumikia nchi hii kwa uzalendo kutokana na elimu watakayoipata," alisema.

Aidha, alisema kwa mwaka 2023 zaidi ya watoto 12,000 wamefaulu kidato cha kwanza na ni matumaini kuwa waliochaguliwa hakuna atakayekosa nafasi kutokana na uwapo wa vyumba vya kutosha vya madarasa.

# Vijana 11,280 wafikiwa na taasisi mwaka 2022

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

TAASISI ya Vijana Mkoa wa Dodoma (DOYODO) imewafikia zaidi ya vijana 11,280 kupitia miradi mbalimbali ya kijamii kwa kipindi cha mwaka 2022.

Mkurugenzi wa taasisi hiyo, Rajabu Nhunga, alisema hayo jana wakati akizungumza na mwandishi wa habari hii kuhusu mafanikio ya taasisi hiyo katika kuwahudumia vijana mkoani hapa.

Alibainisha kuwa taasisi hiyo inafanya kazi na makundi ya vijana kutoka maeneo mbalimbali yaliyoko mkoani hapa.

Kadhalika, Nhunga alisema DOYODO inaendelea kuanzisha na kuvijengea uwezo vikundi vya vijana shuleni kuhusu afua za afya ya uzazi.

Alisema kuwa vikundi hivyo vimewezeshwa elimu ya stadi za maisha ambapo shule 40 zimefikiwa na zaidi ya wanafunzi 5,650 wamejengewa uwezo huo.

Pia alisema DOYODO, imefanikiwa kutekeleza miradi ya afya ya uzazi, uchumi pamoja na kuhamasisha vijana kushiriki kwenye ngazi za maamuzi.

Sambamba na hilo, alisema taasisi hiyo imewezesha mashirika ya vijana 20 kutoka wilaya za Dodoma, Bahi, Chamwino na Mpwapwa kushiriki katika mafunzo mbalimbali ambayo yanalenga kuboresha uwezo wao kwenye eneo la uendeshaji wa mashirika yao na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ya vijana nchini.

Alisema taasisi hiyo ikiwa mjumbe mwakilishi wa vijana katika Kamati ya Kuthibiti UKIMWI Jiji la Dodoma (CMAC), imefanikiwa kutoa elimu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI (VVU).

Alisema zaidi ya vijana 2,320 ambao wako kwenye mazingira hatarishi ya kupata maambukizi ya VVU, wamejengewa uwezo wa kujikinga.



## Viongozi wa dini watakiwa kutoa elimu ya malezi

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA Mdhamini wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Pemba, Hafidh Ameir Shoka, amewataka viongozi wa dini kuwaelimisha wananchi hasa wa vijijini juu ya malezi ya watoto kwa kuzingatia misingi ya dini zao.

Alisema hayo jana kisiwani humo wakati akifungua mkutano wa viongozi wa dini juu ya uwasilishaji wa utekelezaji wa kazi zao za kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka huu pamoja na mikakati yao ya kipindi cha Januari hadi Machi mwakani.

Alisema ni jambo linalotia aibu kwa Zanzibar ambayo watu wake kwa asilimia kubwa wapo katika misingi ya dini lakini vitendo vya udhalilishaji kila kukicha vimekuwa vikiripotiwa kwa wingi.

Alisema ni lazima kuongeza nguvu kwenye mapambano hayo kwa kuwahamasisha wazazi na walezi, kuwaelimisha watoto tangu wakiwa wadogo katika makuzi yao ili iwe rahisi kuwajenga katika misingi imara.

Aidha, aliwataka viongozi hao wa dini kusaidia kurejesha maadili yaliyoambatana na upendo na huruma ambayo kwa sasa yametoweka yanayochangia kasi ya udhalilishaji wa kijinsia.

Viongozi hao wa dini walisema pamoja na mafanikio wanayoyapata katika utoaji wa elimu ya udhalilishaji lakini bado wanakabiliwa na matatizo mbalimbali yanayowafanya kukosa ufanisi mzuri wa kazi zao.

**Alisema ni jambo linalotia aibu kwa Zanzibar ambayo watu wake kwa asilimia kubwa wapo katika misingi ya dini lakini vitendo vya udhalilishaji kila kukicha vimekuwa vikiripotiwa kwa wingi.**

# Taasisi yaandaa chakula kwa watoto yatima sikukuu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAASISI ya Holding Hands Foundation imewaandalia chakula cha mchana watoto yatima wa vijiji vya Mkoa wa Kaskazini Unguja ili watoto hao wafurahi wakati wa msimu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Akizungumza juzi na waandishi wa habari Mkokotoni mkoani humo, baada ya hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema jukumu la kuwalea na kuwatunza watoto yatima ni la jamii wala siyo la ndugu au jamaa wa watoto hao.

Alisema watoto yatima wanahitaji malezi mazuri kama watoto wengine ili kutojihisi wanyonge au kukosa furaha kutokana na kuondokewa na wazazi wao.

"Jamii na viongozi wa ngazi mbalimbali wana jukumu la kuhakikisha watoto yatima wanaishi katika mazingira mazuri na kitendo cha kuondokewa na wazazi wao isiwe sababu ya wao kuwa wanyonge na kukosa furaha," alisema.

Alisema watoto wote wanahitaji kupatiwa haki zao za msingi ikiwamo haki ya kuishi, elimu, afya na kulindwa na vitendo vyote vya uvunjifu wa haki za binadamu ikiwamo vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Pia aliipongeza taasisi hiyo kwa kuwajali watoto yatima akisema watoto hao kupoteza wazazi wao haina maana kuwa watakosa wazazi wengine wa kuwahudumia na kujali haki zao.

Aidha, aliwataka watoto hao kuendelea kuwa na tabia nzuri na watakapobaini kuna mtu anataka kuwafanyia mambo yasiofaa watoe taarifa kwa walezi wao.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Florance Riwa, alisema malengo ya taasisi hiyo ni kusaidia watu wenye mahitaji maalum wakiwamo wajane, watu wenye ulemavu na kuwapatia bima ya afya watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Malengo mengine ni kugawa taulo za kike kwa wasichana shuleni na kutoa msaada wa kisheria kwa wanawake.

Alisema kutokana na juhudi wanazozitumia katika kuitumikia jamii ya watu wenye mahitaji maalum wamefanikiwa kupata washirika wenzao kutoka taasisi isiyo ya kiserikali ya nchini Bosnia ambao wapo nao pamoja kuhakikisha kuwa wanawafikia walengwa kwa ukaribu zaidi.



Mkurugenzi wa Jumuiya ya Wajane Zanzibar, Tabia Makame (kulia), akimfariji Fatma Juma mtoto wa marehemu Zakia Muhammed ambaye ni mwanachama wa jumuiya hiyo aliyefariki dunia juzi Mkoa wa Kaskazini Unguja.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Sheria kuanzisha Mamlaka ya Mapato Zanzibar yapitishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha na Uchumi, imesema kupitishwa kwa Sheria ya Kuundwa kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) itasaidia kuwapo kwa mifumo ambayo itawatambua walipa kodi wote nchini kwa kuwa na kanzi data maalumu.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Sabiba Filfil Thani katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akitoa maoni yake kufuatia Baraza la Wawakilishi kupitisha sheria mpya ya kuundwa kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar na kufutwa kwa Bodi ya Mapato ZRB.

Alisema hadi sasa hakuna takwimu halisi za walipa kodi wakubwa ambapo matokeo yake baadhi ya wafanyabiashara wenye sifa ya kulipa kodi hawalipi inavyostahiki.

Aidha, aliitaka Wizara ya Fedha kuhakikisha mifumo ya kodi yote inatumika rasmi kwa walipakodi ili kudhibiti mianya ambayo huikosesha serikali mapato yake muhimu kwa ajili ya maendeleo.

"Kamati ya Fedha na Uchumi ya Baraza la Wawakilishi imefurahishwa kuwasilishwa kwa sheria ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar ambayo matarajio yetu makubwa chombo hicho kitafanya kazi zake kwa ubunifu mkubwa kuhakikisha mapato ya nchi yanaimarika," alisema.


Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliitaka serikali kufanya ukaguzi wa fedha wa taasisi hiyo ili kuona matumizi, ukusanyaji wa kodi unakwenda katika malengo yaliyokusudiwa.

Mwakilishi wa Bubwini, Mtumwa Peya Yussuf alisema: "Tunaiomba serikali kuhakikisha mamlaka mpya ya kodi inayoundwa kunakuwapo na utaratibu wa ukaguzi wa hesabu zake ili kuona matumizi halisi ya fedha pamoja na makusanyo yake ikiwa ni hatua ya kuwapo kwa uwazi wa fedha."

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Ali Suleiman Ameir, alisema kuundwa kwa Mamlaka ya Kodi Zanzibar kutakwenda sambamba na mikakati ya kuanzishwa kwa mifumo ya kuwatambua walipakodi wote na kuingizwa katika daftari kwa kusajiliwa.

Aidha, alisema mamlaka mpya itakuwa na uwezo wa kufanya marekebisho mbalimbali ya kodi kwa mujibu wa sheria na kwenda na wakati ulioko sasa.

Kamishna wa Mamlaka Kodi Zanzibar, Yussuf Mwenda, alisema wamejipanga kwenda sambamba na sheria ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato ambayo ni kuongeza ufanisi wa kasi ya ukusanyaji wa kodi nchini.





# Polisi yatangaza msako wa wavamizi

**Na Richard Makore,** MWANZA

JESHI la Polisi mkoani Mara limeahidi kuwasaka na kuwakamata watu wanaotoka kijiji cha Mekariro wilayani Bunda, wanaovamia mashamba ya wananchi wa kijiji cha Remungorori wilayani Serengeti wakiwa na silaha za jadi zikiwamo upinde, mikuki na mapanga kwa lengo la kuwanyang'anya ardhi.

Kwa takribani miaka sita sasa, watu hao wamedaiwa kufanya fujo kwa kuvamia mashamba ya wananchi wa kijiji cha Remng'orori ambacho wanapakana nacho.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Longnus Tibishibwamu, alisema wahalifu hao wamekuwapo muda mrefu wakitishia wenzao kwa silaha za jadi na kwamba watawasaka na kuwakamata wote.

Kamanda Tibishibwamu alisema vijiji hivyo havina mgogoro wa kudumu, badala yake kumejitokeza kundi la watu wanaotaka kuvamia ardhi ya kijiji cha Remng'orori kwa ajili ya kuweka makazi na kilimo.

Alisema vijiji hivyo vina mipaka ya kiutawala inayojulikana na kwamba viongozi wa serikali walishakutana na wananchi wa pande zote mbili wakakubaliana kila mtu alime eneo lake alilokuwa akimiliki.

Kamanda aliongeza kuwa wakuu wa wilaya za Bunda na Serengeti walishakutana na wananchi wa pande zote mbili, lakini anashangaa wahalifu kuendelea kuwapo.

"Hawa ni wahalifu kama wahalifu wengine na tutawasaka na kuhakikisha tunawakamata ili tuwafikishe mbele ya sheria," alisema.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu kuhusu uhalifu huo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Remng'orori wilayani Serengeti, ambacho wananchi wake wanaendelea kuvamiwa na kushambuliwa, Msamba King'anyi, alisema wameshindwa kufanya shughuli za kilimo kutokana na kuhofia usalama wao.

Alikiri wananchi wake kuvamiwa na kikundi cha watu wanaotoka Kijiji cha Mekamariro wilayani Bunda wanaotaka kupora kwa nguvu mashamba yao.

Alisema awali kulikuwa na mgogoro wa vijiji vitatu, lakini serikali iliumaliza kwa kugawa ardhi kwa pande zote zilizokuwa na malalamiko.

Alisema katika mgawanyo huo, Kijiji cha Remng'orori kilipewa ekari 1,179, Sirori Simba ambacho kiko wilaya ya Butiama kilipata ekari 1,176 na Mekamariro kilichoko Bunda, kiligawiwa ekari 1,180.

King'anyi alisema baada ya mgogoro huo kumalizwa na serikali, wameibuka tena watu wengine kutoka kijiji hicho cha Mekamariro na kulivamia eneo lingine ambalo ni la Remng'ororori pia na kuanza kujenga nyumba za kudumu pamoja na kilimo.

Alilalamika kuwa viongozi wa kijiji chake wanapotoa taarifa kuhusu uvamizi huo, wamekuwa wakikamatwa wao badala ya wavamizi.

Aliongeza kuwa mwaka 1918 uvamizi kama huo ulitokea katika kijiji chake na kusababisha vifo vya watu wawili katika eneo hilo.

Baadhi ya wananchi wanasema chanzo cha uhalifu huo ni kutaka kuchukua kwa nguvu ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji.



Mkaguzi wa Hesabu wa Vyama vya Ushirika mkoani Shinyanga, Rodrick Kilemile (kulia), akitoa taarifa ya upatikanaji wa hati yenye shaka kwa Chama Kikuu cha Ushirika wilayani Kahama (KACU), (katikati) ni Meneja wa KACU, Abdul Ali na Mjumbe Kayungiro Mwenge. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mkaguzi ushirika agundua madudu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Kikuu cha Ushirika Wilaya ya Kahama (KACU), kimepata hati yenye shaka baada ya kufanyika ukaguzi wa hesabu kwa mwaka 2021/22.

Ukaguzi huo ulifanywa na mkaguzi wa hesabu wa vyama vya ushirika mkoani Shinyanga.

Mkaguzi wa Hesabu wa Ushirika mkoani Shinyanga, Rodrick Kilemile, aliyasema hayo katika mkutano mkuu wa 27 wa KACU na kusema kati ya hoja 10 za mwaka wa fedha 2021/22 ilijibiwa hoja moja, tatu ziko katika utekelezaji na sita hazijatekelezwa.

Alisema wakati wa ukaguzi wa hesabu wa mwaka wa fedha 2021/2022 katika chama hicho, waliomba kupata nyaraka za uthibitisho wa uhalali wa deni la Sh. milioni 70 kutoka Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), lakini hawakuzipata.

Kilemile alisema katika mwaka huo kuna magari mawili aina ya Toyota Land Cruiser yanayofanana yalinunuliwa kwa Sh. milioni 165, lakini moja likinunuliwa Sh. milioni 85 na lingine Sh. milioni 80 hatua ambayo imezua shaka aina moja ya magari kununuliwa kwa bei tofauti.

Aliongeza kuwa chama hicho kimekuwa kikitumia fedha nyingi ikilinganishwa na mapato wanayokusanya kila mwaka.

Alisema mwaka wa fedha uliopita walikusanya Sh. milioni 470.4, lakini walitumia Sh. milioni 655.9 na kuwataka kuendelea kujibu hoja zilizobaki ili kutopata hati yenye shaka.

Akijibu malalamiko hayo mbele ya wajumbe katika mkutano huo, Mwenyekiti wa KACU, Hamisi Majogoro, alikana kutambua deni la NSSF.

Wakati huo huo, KACU kimesema kitaacha kununua zao la pamba kutoka kwa wakulima kwa kuwa kinapata hasara kwa kila mwaka na hivyo kushindwa kulipa madeni yaliyokopa katika taasisi za kifedha ikiwamo Benki ya Maendeleo ya

## Daraja lajengwa kunusuru wanafunzi kuzama

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wanaosoma Shule ya Msingi Bubale katika Kata ya Masengwa wilayani Shinyanga, wameondokona na hatari ya kusombwa na maji wakati wakienda shule kupitia Mto Bulango ulioko kijijini hapo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Bubale, Phantom Nkonoki, alisema hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ilipotembelea kijijini hapo kuangalia kero mbalimbali zinazowakabili wanafunzi hao.

Alishukuru serikali kwa kuwajengea daraja la kuvuta katika mto huo, kwa kuwa kabla ya kupata miundombinu hiyo wakati wa mvua wanafunzi walikuwa wanashindwa kwenda shule kuhofia kusombwa na maji wakati wakivuka.

"Mto huu kabla ya kujengwa daraja ilikuwa ngumu kupita, siyo kwa watoto pekee wanaokwenda shule bali hata sisi watu wazima ilikuwa shughuli na tulikuwa tunashindwa hata kufanya shughuli za kiuchumi hadi maji yapungue ndipo tupite," alisema Nkonoki.

Mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, Juma Masesa, alisema kabla ya kujengwa daraja hilo walikuwa wakiwazuia watoto wao kwenda shule mpaka maji yaishe au kupungua.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Masengwa, wilayani Shinyanga, Hussein Majaliwa, alisema wana shule mbili za msingi katika eneo hilo na kwamba sehemu moja imepata ufumbuzi na sasa imebaki moja ambayo ni shule ya Ikonda.

# Biden aidhinisha msaada wa dharura New York

**NEW YORK, Marekani**

RAIS wa Marekani, Joe Biden, ameidhinisha kupelekwa kwa msaada wa dharura katika jimbo la New York ambalo limekubwa na dhoruba kali ya theluji iliosababisha vifo vya zaidi ya watu 37 huku maelfu wakiachwa bila nishati ya umeme.

Mamlaka nchini humo ilisema jana kuwa, kikosi cha dharura cha uokoaji kimejitahidi kuokoa wakazi walioathiriwa kutokana na kile kilichotajwa kama dhoruba ya theluji ya karne ambayo imetatiza mwenendo mzima wa usafiri katika majimbo tisa.

Mamlaka katika jimbo la New York ilieleza hali hiyo kuwa mbaya zaidi hasa katika eneo la Buffalo huku miili ikigunduliwa kwenye magari na kwenye kingo za theluji, huku waokoaji wakikagua magari ili kutafuta waliofariki au walio hai.

Gavana wa New York, Katheleen Hochul, alisema wanatazamia dhoruba hiyo itarejea tena, baada ya kushuhudia barafu yenye urefu wa nchi sita hadi 12 upande wa kusini wa Kaunti ya Erie na kusini mwa eneo hilo walipata theluji yenye urefu wa nchi 30 hadi 40 usiku wa kuamkia jana.

Gavana wa kaunti ya Erie, eneo ambalo hali mbaya zaidi ya hewa ilishuhudiwa, Mark Poloncarz, alisema idadi ya vifo imeongezeka kutokana na dhoruba hiyo ya theluji hadi vifo 12 kwa usiku wa kuamkia jana.

"Ofisi ya idara ya afya Erie imethibitisha vifo 25 katika kaunti yote ya Erie, idadi hiyo inajumuishwa na ile ya mji wa Buffalo," alisema Poloncarz.

Aliongeza kuwa wapo baadhi ambao wanaweza kupatikana Buffalo ambao idara ya afya haijawathibitisha na kwamba wako katika mchakato huo wa kuwathibitisha.

"Kwa sasa hatuna taarifa kuhusu maeneo, jinsia au namna ya kifo, tunatarajia kuwa na taarifa hizo hivi karibuni," alisema Poloncarz.

Hata hivyo, inabainishwa kwamba dhoruba ya theluji kali, upepo unaovuma kwa kasi huku halijoto ikiwa chini ya sifuri vililazimisha kufutwa kwa zaidi ya safari 15,000 za ndege za Marekani katika siku za hivi karibuni, zikiwamo zaidi ya 3,800 mwanzoni mwa wiki.

Pia inaelezwa kuwa barabara nyingi ikiwamo zile zenye shughuli mbalimbali zilifungwa kutokana na kufunikwa kwa barafu.

Aidha, madereva wameonywa kutoendesha magari yao barabarani pamoja na kwamba nchi ipo katika kipindi ambacho matumizi ya barabara yapo juu kutokana na watu wengi kusafiri.

Inaelezwa kuwa kikosi cha ulinzi cha taifa pamoja na timu zingine za uokoaji wameokoa mamia ya watu kutoka katika magari yaliyofunikwa na theluji na nyumba ambazo hazina umeme, huku mamlaka ikisema kwamba watu zaidi huenda wamenasa kwenye theluji.

Karibu watu milioni 1.7 Jumamosi walikosa huduma ya umeme huku wakipigwa na baridi kali.

Idadi hiyo imepungua kwa kiasi kikubwa ingawaje bado kulikuwa na takriban wateja 50,000 wakiwa hawana huduma hiyo Jumatatu huko pwani ya mashariki mwa Marekani.

***DW***



Sehemu ya barabara ikiwa imefunikwa kwa theluji Marekani. **PICHA: DW**

## China kutamatisha karantini ya Covid 2013

**BEIJING, China**

MAOFISA nchini China wamesema taifa hilo litaondoa karantini kwa wasafiri kuanzia Januari 8, 2023, na kwamba hatua hiyo inaashiria mabadiliko makubwa ya mwisho kutoka kwa sera ya 'zero covid' ya nchi hiyo.

Kwa mujibu wa ripoti ya BBC iliyochapishwa jana, hiyo itafungua tena nchi hiyo kwa wale walio na visa vya kazi, kusoma au wanaotaka kutembelea familia, baada ya mipaka kufungwa kwa takribani miaka mitatu.

Pia inaelezwa kuwa hatua hiyo imekuja wakati China inapambana na kuenea kwa virusi hivyo kwa sababu ya vizuizi kuondolewa.

Ripoti zinasema hospitali zimezidiwa na wazee wanakufa na kwamba idadi ya kweli, hesabu za kila siku na vifo haijulikani kwa sasa kwa sababu maofisa wameacha kutoa data ya UVIKO-19.

Beijing ilikuwa imeripoti takribani maambukizo mapya 4,000 ya ugonjwa huo kila siku wiki iliyopita na vifo vichache, huku ikisema itaacha kabisa kuchapisha nambari za kesi.

Kwa mujibu wa Reuters, kampuni ya data ya afya ya Uingereza Airfinity ilikadiria China ilikuwa ikipata maambukizi zaidi ya milioni moja na vifo 5,000 kwa siku.

Sera inayoitwa 'zero Covid' ilitajwa kudhoofisha uchumi na kuwafanya raia kuchoka kwa vizuizi na vipimo vya mara kwa mara nchini humo.

Chuki dhidi ya sera hiyo ililipuka na kwa kufanyika maandamano adimu ya umma dhidi ya Rais Xi Jinping Novemba mwaka huu, ambayo yalisababisha viongozi kutupilia mbali sheria za UVIKO-19 wiki chache baadaye.

***BBC***

## Ukraine yapanga mkutano wa amani 2013

**KYIV, Ukraine**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Dmytro Kuleba, amesema kwamba serikali yake ina lengo la kuandaa mkutano wa amani mwishoni mwa Februari mwaka 2013, kwenye Umoja wa Mataifa (UN).

Kwa mujibu wa ripoti ya VOA, iliyochapishwa jana, Katibu Mkuu wa UN Antonio Guterres, anatarajiwa kuwa mpatanishi, wakati wa maadhimisho ya vita vya Russia.

Kuleba aliiambia Associated Press kwamba Russia itaalikwa kwenye mkutano huo ikiwa nchi hiyo itakabiliwa kwanza na mashtaka ya uhalifu wa vita mbele ya mahakama.

Pia alisema kwamba aliridhishwa na matokeo ya ziara ya Rais Volodymyr Zelenskiy nchini Marekani wiki iliyopita, huku akifichua msaada mkubwa wa kiulinzi ambao Ukraine itapatiwa na Marekani.

"Serikali ya Marekani imeandaa mpango maalum wa kufanya makombora ya kujihami ambayo ni msaada wa Marekani, ambayo yatakuwa tayari kufanya kazi nchini Ukraine kwa miezi sita," alisema.

Aliongeza kwamba Ukraine itafanya lolote liwezekanalo kushinda vita mwaka ujao, akieleza kuwa diplomasia kila mara ina mchango mkubwa.

***VOA***

## Rais wa zamani Korea Kusini aachiwa huru

**SEOUL, Korea Kusini**

RAIS wa zamani wa Korea Kusini, Lee Myung-bak, aliyehukumiwa kifungo cha miaka 17, ameachiliwa huru kwa msamaha wa Rais. Baada ya Park Geun-hye kupewa msamaha wa rais mnamo mwaka 2021.

Inaelezwa kuwa kiongozi huyo wa zamani alihukumiwa 2020 kwa ufisadi na ubadhirifu, baada ya kupatikana na hatia ya kupokea mamilioni ya dola kama hongo, ili kubadilisha uamuzi kwa msamaha wa mkuu wa zamani wa Samsung.

Rais huyo wa zamani alisema msamaha huo wa kirais unamwondoa sehemu mbaya, kwani pamoja na kufutwa kwa kifungo chake, atapata na marupurupu yake.

Pia ilibainishwa kuwa Lee Myung-bak alifutiwa adhabu kwasababu za kiafya na kwamba alikaa gerezani miaka miwili pekee.

***RFI***

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

Ipo **Yombo Dovya,** Makangarawe Mtaa njia panda ya Mwinyi. Inafaa kwa Biashara pamoja na Makazi ya kuishi. Ina vyumba 6 na varanda 2. **Bei ni shilingi Milioni 75.**

**Kwa mawasiliano piga simu 0782 251 471.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha DODOMA MJINI**
**Mkoa DODOMA**
**Shauri la MADAI Na.269/2022**
**Jina la Mdai EMMANUEL SAMSON NALUGWA**
**Jina la MDAIWA GODFREY NDERINGO MOWO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**KWA; ... GODFREY NDERINGO MOWO**
Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba
**MADAI YA TSH. 20,000,000/=**
Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 05/01/2023 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelzo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini. Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 16/12/2022

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MATHIAS RAPHAEL MTEGA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T.851 CDH.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI MBE/MBE/RB/489009/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA JIJI MBEYA.**
**30/11/2022**
**tafadhali taja;**
**Kumb.Na.MBRL/10869/13/JRM**
**Kwa yeyote anayehusika,**
**SHERIA YA USAJILI WA ARDHI [SURA 334]**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KIWANJA NAMBA 355 KITALU A.IVUMWE JIJI LA MBEYA.**

Barua y toleo [letter of offer]ya kiwanja,Kiwanja Na.355 kitalu 'A' IVUMWE Jiji la Mbeya.
Mmiliki aliyeandikishwa;M/SMUNICIPAL COUNCIL HOUSING COOP.SOCIETY/MARGRETH MWANKENJA wa S.L.P 149, MBEYA.
Muombaji MAGRETHKIBONA MWANKENJA wa S.L.P 1246 MBEYA.
ARDHI; Kiwanja Na; 355 kitalu 'A' IVUMWE Jiji la MBEYA.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba barua ya toleo[letter of offer]pamoja na risiti orijino ya kiwanja iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa nakala halisi ya barua ya toleo[letter of offer] ya kiwanja tajwa hapo juu, iwapo hakuna kipingamizi chochote kitakacho jitokeza ndani ya muda wa mwez mmoja[siku 30]tokea tarehe ya taarifa hii.

Barua ya toleo [letter of offer] ya kiwanja halisi ikionekana irudishwe katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya S.L.P 149, Mbeya.

Imetolewa na,

**Dickley.E.Nyato**
**AFISA MTEULE**
**HALMASHAURI YA JIJI LA MBEYA**

---

**TANFIN CONSULTANT EA LTD**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**KAMPUNI YA TANFIN CONSULTANT EA LTD KWA MAMLAKA ILIYOPEWA NA MKOMBOZI SOKO KUU SACCOS – KONDOA INATANGAZA NNADA WA HADHARA UTAKAOFANYIKA TAREHE 30/12/2022 KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI KATIKA ENEO LA OFISI YA MKOMBI SOKO KUU SACCOS. MNADA HUU NI WA KUUZA PIKIPIKI, VIFAA VYA OFISINI KAMA PHOTOCOPY MACHINE, COPYUTA N.K PAMOJA NA THAMANI ZA NYUMBANI (TV, FRIJI N.K) MALI ZA OFISI NA WADAIWA SUGU**

**WOTE MNAKARIBISHWA**
**MAWASILIANO**
**0717417520, 0627704403.**

---

**DEUDEDIT JUVENARY KABUNDUNGURU T/A FREEDOM PASS TANZANIA LIMITED**

## MNADA WA HADHARA

KWA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA FILGONA RANGA DUKO SIKU YA TAREHE 16 JANUARY 2023 KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI.

ORODHA YA MALI ZITAKAZOUZWA NI KAMA IFUATAVYO HAPA CHINI

| Lot number | Maelelezo ya mali inayouzwa na kwa amri ya mahakama |
|---|---|
| 1 | TATA LP 909 Chasis No MAT 382042J7R03136, Engine no 497TC93PYS841445 yenye namba ya usajili T867DMU |
| 2 | TATA LP Chasis No MAT382042JR06708,Engine No 497tc93ERY815561 yenye namba ya usajili T526DNP |
| 3 | TATA LP Chasis No MAT382042JR06708,Engine No 497TC9ECR809720 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14 na ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwishailipa
3. Gharama ya kukagua na kuona magari ni ya mnunuzi pamoja na kuhamisha umiliki ni ya mnunuzi.
4. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa yeyote akatayejaribu kuharibu mnada huu
5. Kwa mawasiliano zaidi piga namba **0620811284**

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ABIHORERA RASHIDI BORA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 170 BKN.** Chassis namba **KE7KEFPKO30380.** Engine namba 162FMJPKO030380. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/490134/2022.**

---

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**LUCY ROBERT JONAS,** AMEPOTEZA PASSPORT YAKE YENYE NAMBA **TAE365681** ILIYOTOLEWA TAREHE **08/10/2020** NA IDARA YA UHAMIAJI DAR ES SALAAM. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/CHA/RB/483902/2022.**

---

**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF LANDS, HOUSING AND HUMAN SETTLEMENT DEVELOPMENT**
**REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT, (CAP 117)**

**DEED POLL**



The documents presented for registration on the 19-12-2022 at 3:00 herewith the original of the above mentioned documents registration having under folio/s 1981 and serials and serial/s 94812022 knowledge receipt of the enclosures here to.
**URES:**

SIGNED AND DELIVERED BY SAID
WINFRIDA GATAWA MAGANILA
Who is known to me personally identified to me by....
The letter being known to me personally.
This 19 day of 12...2022.

**BEFOR ME:** Name ... Signature ... Postal Address ... Date ... Qualification: COMMISSIONER FOR OATHS.

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

BURUDANI



# GIGY MONEY ACHEFUKWA

Msanii Gigy Money ameonekana kuchefukwa akidai siyo kila anayekwenda kuomba ushauri kwa mtu hajui la kufanya, bali ni kusikia maoni yao tu ya kuyapima.

Kwenye mtandao wake wa kijamii wa Instagram, Gigy alisema yeye hana rafiki wa kike na hataki mazoea nao kwa sana.

"Wadada mimi sio bongo movie wala bongo fleva, mimi ni Gigy Money sina muda na maisha ya mtu, pia sipendi mtu mnafiki maishani mwangu. Na sitaki mazoea na msanii wa mamuvi, nimesema sitaki mazoea ... sio mdogo wa mtu mimi wala sio ndugu wa mtu ... haya mafumbo msipo yaelewa nitakuja na faili la ukweli mtupu, sio kila mtu anaogopa jina sijui hela, kwanza maisha yangu tu wengi hamjayaishiii acheni uzee uje vizuri mimi sipendi ugombanishi kiukweli kabisa nikikupenda nakupenda na moyo wangu wote, na nikikuchukia ni huo huo moyo, siyo kila kitu ni bifu au ugomvi jina langu lifike mahala liwatoke kwenye vichwa na vinywa vyenu ndugu wasanii," alilalama dada huyo ikionyesha kabisa kuna mtu amemkera.

## HARMONIZE AFURAHIA KUPEWA NAMBA 10



BAADA ya Meneja wa Diamond Platnumz, Sallam SK, kutoa orodha ya wasanii 10 bora kwa mwaka 2022, huku Harmonize akiwamo, msanii huyo wa bongo fleva ameibuka na kumpa tano kiongozi huyo.

Harmonize ameonekana kufurahia kuwekwa kwenye orodha ya wasanii hao, licha ya kuwekwa kwenye namba 10.

Kupitia insta stori yake, msanii huyo alimshukuru kwa kusema 'Asante Kipara no Mara waah 10, Messi.'

Majuzi, Sallam SK alitoa orodha ya wasanii wake bora kwa mwaka 2022, ambapo Diamomd Platnumz alishika namba moja, huku Zuchu akifuatia.

Mbosso, kwa mujibu wa meneja huyo ameshika nafasi ya tatu na ya nne ilikwenda na Marioo, Rayvanny akiwa kwenye namba tano.

Jay Melody aliwekwa kwenye namba sita huku msanii mkongwe, Ali Kiba alitupwa nafasi ya saba, Nandy alikamata namba nane, nafasi ya tisa ikaendea kwa Lavalava.

## LAVALAVA AFUNGUKA DONGO LA DULLA MAKABILA



MSANII Lavalava amesema haoni baya lolote ambalo, Dulla Makabila ameimba kuhusu yeye kwenye wimbo wake wa 'Pita Huku', akiongeza huyo ni rafiki yake na ni mtu mwenye utani sana.

Kwenye kipande cha watu wabaya 'wachawi' baada ya kutaja mabaya yao ikiwamo kuwarudisha watu nyuma kimaendeleo, kuna kipande alisema "uchawi ndiyo chanzo cha umaskini unapita kwenye pembe hivi milango huioni na uchawi mkaupeleka usafini, yaani hata Lavalava aimbe vipi haonekani, we mchawi pita huku..."

Lavalava alisema Dula siku zote kabla hajaimba au kutoa wimbo humpigia, na hata wimbo huu pia alifanya hivyo, ingawa yeye hajapata wasaa wa kuusikiliza.

"Wimbo wenyewe sijapata nafasi ya kuusikiliza, najua yule ni mtu wa masihara sana, akisema kitu kinakuwa na utani ndani yake na mambo kama haya watu kuna wakati wanahitaji wafurahi, usifuatishe sana kinachozungumzwa. Mimi sijausikia wimbo huo, lakini watu wanasema ni mkali sana kama kweli uko hivyo basi ni kazi nzuri tu," alisema Lavalava.

# KMC FC YALIA NA MWAMUZI KUSAJILI WAPYA WATATU

**Shufaa Lyimo na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, akililalamika mwamuzi wa mechi yao dhidi ya Simba aliwanyima penalti, ameongeza anahitaji kusajili wachezaji wapya wasiopungua watatu ili kuimarisha kikosi chake kinachoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hitimana alisema anahitaji kusajili mshambuliaji, beki wa kati na kiungo ili kuiongezea nguvu timu hiyo.

Kocha huyo alisema tayari mapendekezo hayo ameshayafikisha kwa viongozi wa timu na ana imani watayafanyia kazi ili wawe imara na kufanya vizuri katika mechi zilizosalia za Ligi Kuu na mashindano ya Kombe la FA.

Alisema baadhi ya wachezaji wake ni majeruhi wa muda mrefu na kutokana na hali hiyo anahitaji kupata wachezaji wapya watakaoziba pengo hilo.

"Tumecheza michezo 18 ya ligi, tumeona madhaifu yetu na wapi tunatakiwa kuongeza nguvu, tayari nimekabidhi mapendekezo kwa kutaja nafasi ninazohitaji kusajili kwa lengo la kuisaidia timu kufanya vizuri," alisema Hitimana.

Aliongeza wanahitaji kuimarisha kikosi kwa ajili ya kukabiliana na ushindani mkubwa wa ligi uliopo.

"Hatutafanya mabadiliko makubwa kwa sababu ukiangalia katika baadhi ya mechi tumefanikiwa kutengeneza nafasi nyingi za wazi lakini tunashindwa kumalizia, nina imani kubwa tukipata mshambuliaji mwingine tutamaliza tatizo hili," alisema kocha huyo.

Aliongeza bado malengo ya KMC ni kumaliza msimu katika nafasi tano za juu, na hilo haliwezi kukamilika kama hawataboresha kikosi chao.

Mrundi huyo alisema pia amesikitishwa na kitendo cha mwamuzi, Omary Mdoe, kuwanyima penalti katika mechi ya juzi ambayo ilimalizika kwa kufungwa mabao 3-1. "Nimesikitika, tulipaswa kupata penalti isipokuwa mwamuzi hakututendea haki," alisema Hitimana.

Alilitaka Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kualiangalia zaidi suala la waamuzi kwa sababu mara nyingi wanaonekana kudaiwa kuzibeba timu kubwa.

KMC FC inashika nafasi ya tisa ikiwa imecheza michezo 18, wameshinda mechi tano, sare saba na wamepoteza michezo sita, kibindoni wana pointi 22.



Kikosi cha Kirengo FC kinachotarajia kukutana na Mafundi FC ya Obwere katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Umoja Cup Rorya itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Maji Sota, Rorya mkoani Mara. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Umoja Cup Rorya kumekucha

**Na Mwandishi Wetu, RORYA**

MABINGWA watetezi, Kirengo FC itakutana na Mafundi wa Obwere katika mechi ya nusu fainali ya kwanza ya mashindano yanayofanyika kila mwaka ya Umoja Cup itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Maji Sota, mkoani Mara.

Mashindano hayo yalianza kwa kushirikisha timu 20 na zilizobakia Kirengo FC, Mafundi FC, KMT ya Sota na Kabwana FC ya Shirati mjini.

Kirengo ilitinga nusu fainali baada ya kuwafunga Masonga mabao 3-0 na Mafundi waliwatoa Rifa ya Michire kwa magoli 4-3.

Hata hivyo, Kirengo anashuka dimbani bila wachezaji wake wanne waliofungiwa kucheza michuano hiyo kwa mwaka huu kutokana na kosa la utovu wa nidhamu, nyota hao ni Oribg'o Sido, Kitembe Kwara, Lazaro Lazaro na Riziki Abega.

Nusu fainali ya pili ya michuano hiyo itachezwa kesho kwa kuikutanisha KMT dhidi ya Kabwana fc.

Msimamizi wa mashindano na Meneja wa Umoja Cup, Daniel Maina, alisema mashindano ya mwaka huu yalichelewa kuanza kutokana na mdhamini wao kukutana na changamoto mbalimbali.

Wakati huo huo, mwenyeji wa michuano hiyo, Wanamaji FC ya Sota, ilifutiwa matokeo na kuondolewa mashindano hayo baada ya kumtumia, Abega, ambaye amefungiwa.



## Nyota waendelea kuondoka Geita

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumpoteza, George Mpole aliyekwenda FC Lupopo na Saido Ntibazonkiza aliyetua Simba katika usajili wa dirisha dogo, Geita Gold FC imepoteza mchezaji mwingine wa kikosi cha kwanza, Adeyum Suleiman, ambaye amejiunga na Dodoma Jiji.

Taarifa iliyotolewa na Dodoma Jiji FC imesema kwa sasa beki huyo mwenye uwezo wa kucheza nafasi zote za pembeni ni mali yao.

"Beki huyu anacheza maeneo ya pembeni, ni mbavu ya mpira. Anaitwa Adeyum Suleiman sasa ni mkulima wa zabibu" taarifa ya klabu hiyo iliandika.

Habari zilizopatikana jijini zinasema Adeyum amevunja mkataba na Geita Gold ili kupata changamoto mpya.

Adeyum ambaye ni mchezaji wa zamani wa Yanga, amejiunga na Dodoma Jiji ikiwa imepita siku moja tangu ikubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Singida Big Stars katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri.

## Timu tisa kuwania umalkia mapinduzi

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya netiboli ya kuwania Kombe la Mapinduzi yamepangwa kufanyika kuanzia Januari 4 hadi 11, mwakani kwenye Uwanja wa Gymkhana Zanzibar, imefahamika kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Netiboli Zanzibar (CHANEZA), Said Mansab alisema, mashindano hayo yatashirikisha timu tisa kutoka Pemba na Unguja.

"Maandalizi kuelekea katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanaendelea vizuri, kila timu imejipanga kikamilifu, timu saba zinatoka Unguja na mbili ni za kutoka Pemba," alisema Mansab.

Katibu huyo alisema CHANEZA imeshindwa kutoa mwaliko kwa timu kutoka Tanzania Bara kutokana na uhaba wa wadhamini.

Aliongeza viwango vya wachezaji wa mchezo huo kwa sasa Zanzibar vimepanda na wanatarajia kuwa na mashindano yenye ubora mkubwa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### JOAO ANUKIA CHELSEA

CHELSEA inajipanga kufanya mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Atletico Madrid, Joao Felix kwa mkopo katika dirisha la Januari lakini kukiwa na kipengele cha kumpa Mreno huyo mwenye umri wa miaka 23 mkataba wa kudumu kwenye majira ya joto ***(Telegraph).***

### RONALDO AANDALIWA VIPIMO

KLABU ya Al Nassr ya Saudi Arabia inaandaa zoezi la vipimo kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo, ambaye ana umri wa miaka 37 kabla ya kukamilisha uhamisho wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 75 kwa muda wa mwaka mmoja. ***(CBS Sports)***

### MUDRYK ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imewasilisha ofa ya thamani ya pauni milioni 55 kwa winga wa Shakhtar Donetsk na Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhaylo Mudryk, ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Telegraph)***

### BELLINGHAM SOKONI

KIUNGO wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham (19), anaendelea kuwa nyota anayewindwa na Liverpool ingawa bado kuna mchuano dhidi ya Manchester United ambayo pia inamhitaji Cody Gakpo wa PSV. ***(Mail)***

### MOYES: RICE HAONDOKI

KOCHA Mkuu wa West Ham, David Moyes, amesema klabu hiyo haitakubali kuona kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Declan Rice, mwenye umri wa miaka 23 anaondoka katika majira ya joto. ***(Mail)***

### RAYA ANUKIA AJAX

AJAX imeanza kufanya mawasiliano na golikipa wa Brentford na Timu ya Taifa ya Hispania, David Raya, ambaye ana umri wa miaka 27 kwa ajili ya uhamisho wa dirisha dogo la Januari. ***(AS - in Spanish)***

### BARCA: DE JONG HAUZWI

BARCELONA imeweka wazi haiko tayari kumuuza kiungo wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Frenkie de Jong, ambaye anatakiwa na Manchester United katika majira ya joto. ***(Sport - in Spanish)***

### ELANGA AGOMBEWA EPL

EVERTON ni moja ya timu za Ligi Kuu England zilizoingia katika vita ya kuwania huduma ya winga wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Sweden, Anthony Elanga, mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail)***

### LEAO ATOA MSIMAMO

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao (23), amesema anatamani kupata nafasi ya kucheza katika Ligi Kuu England hapo baadaye lakini kwa sasa "nguvu na akili yake kwa asilimia 100% ameziweka kwa AC Milan". ***(RDP Africa, via Talksport)***

### DURAN AKARIBIA BENFICA

BRENTFORD, Fulham na Aston Villa zimewasilisha ofa kwa ajili ya kumsajili mshambuliaji wa Chicago Fire na Timu ya Taifa ya Colombia, Jhon Duran, lakini Benfica inaonekana iko kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumnasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 19. ***Calciomercato - in Italian)***

### BADIASHILE KUTUA CHELSEA

CHELSEA iko katika hatua nzuri ya mazungumzo ya kumsajili beki wa kati wa Monaco na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Benoit Badiashile, na tayari imeshawasilisha rasmi ofa kumnasa nyota huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GAKPO, LIVERPOOL SASA KIMEELEWEKA

●●● Mshambuliaji huyo ajiandaa kwenda England kufanya vipimo vya...

**EINDHOVEN, Uholanzi**

LIVERPOOL imefikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Cody Gakpo akitokea PSV Eindhoven, taarifa ya klabu hiyo ya Uholanzi imesema.

Gakpo, ambaye ana umri wa miaka 23 alionyesha kiwango kizuri katika fainali za Kombe la Dunia zilizomalizika huko Qatar, akifunga mabao matatu na kuisaidia Uholanzi kufika hatua ya robo fainali.

Imeelezwa ada ya winga huyo inatarajiwa kuwa kati ya euro milioni 40 na 50.

PSV imesema Gakpo atasafiri kwenda England kukamilisha mchakato wa uhamisho na iliongeza usajili wake unatarajiwa kuvunja rekodi ya uhamisho ndani ya klabu hiyo.

Liverpool tayari imeshakamilisha usajili wa washambuliaji, Luis Diaz na Diogo Jota, ambao wamepewa mikataba mirefu.

Manchester United nayo ilihusishwa na usajili wa Gakpo.

"Uongozi wa PSV umekamilisha mazungumzo katika siku ya jana (juzi) na imetoa ruhusa kwa Gakpo kusafiri kuelekea England," taarifa rasmi ya klabu hiyo ya Eredivisie ilisema.

Gakpo alikuwa na kiwango kizuri katika msimu huu, amefunga mabao tisa na kutengeneza nafasi nyingine za kufunga 12 kwenye mechi 14 alizoichezea PSV.

Pia nyota huyo amefunga magoli matatu na asisti mbili kwenye mechi tano za Ligi ya Europa.

Katika fainali za Kombe la Dunia, amefunga katika kila mechi kwenye hatua ya makundi ambapo walicheza dhidi ya Senegal, Ecuador na Qatar.

Wakati huo huo Liverpool imepata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Aston Villa katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa juzi na kukifanya kikosi cha Jurgen Klopp kupanda hadi katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi hiyo.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 429,
MECHI KALI
LEEDS
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 7.63
X | 5.27
2 | 1.32
PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# RONALDO KUFANYIWA VIPIMO SAUDI ARABIA



**RIYADH, Saudi Arabia**

KLABU ya Al-Nassr imeandaa mchakato wa vipimo vya afya kwa mshambuliaji, Cristiano Ronaldo ikiwa ni maandalizi ya kukamilisha usajili wa mwaka mmoja wenye thamani ya paundi milioni 173, na nyota huyo wa Ureno atapewa nafasi ya kuchagua kocha ambaye ataungana naye kwenye timu hiyo ya Saudi Arabia.

Mkataba wa Ronaldo na Manchester United ulivunjika mwezi uliopita baada ya kufanya mahojiano ambayo yaliyobainisha kufanyiwa vitendo vya ubaguzi na Kocha wa klabu hiyo, Erik ten Hag.

Tangu wakati huo, mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 37 alianza kujipanga kusaka timu nyingine, na sasa inaonekana anakaribia kujiunga na klabu ya Mashariki ya Kati.

Al-Nassr inaendelea kujiimarisha katika kukamilisha uhamisho huo wa kumnasa Ronaldo, na tayari imeshaandaa malazi kwa nyota huyo pamoja na washauri wake, CBS Sports ilisema.

Inaonekana uhamisho huo unaweza kukamilika katika dirisha dogo la Januari baada ya pande hizo mbili kufikia makubaliano kwenye maslahi.

Wakati mshambuliaji huyo anatarajiwa kuwa nyota wa kwanza mkubwa kucheza soka Saudi Arabia, inaelezwa pia Ronaldo atafaidika kwa kupata dili mbalimbali za nje ya uwanja endapo atasajiliwa na Al-Nassr.

Kwa sasa Al-Nassr iko chini ya Rudi Garcia, ambaye aliwahi pia kuzifundisha Lille, Roma na Marseille wakati alipokuwa Ulaya.

# Kane afananishwa na mashine

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Tottenham, Harry Kane ni "mashine" na ni nyota anayetarajiwa kuwa "namba moja duniani", amesema mchezaji mwenzake, Pierre-Emile Hojbjerg.

Kane hajaonyesha uchovu wowote uliotokana na mashindano ya Kombe la Dunia akifunga kwa kichwa katika mechi ya Ligi Kuu England iliyomalizika kwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Brentford.

Ni mechi ya kwanza kwa nahodha huyo wa Timu ya Taifa England tangu alipofunga penalti moja na kukosa nyingine katika mechi ya hatua ya robo fainali iliyomaliza kwa Ufaransa kushinda mabao 2-1.

"Kutothamini ubora wake ni kosa kubwa," alisema Hojbjerg, ambaye alifunga bao la kusawazisha.

"Yeye ni mashine. Ana uwezo mzuri na anastahili kuwa mchezaji namba moja duniani kwa sasa.

"Kosa kubwa katika kandanda ni kutilia shaka kiwango cha Harry Kane."

Kane ameingia katika rekodi ya nyota wa England waliofunga mabao mengi, akipachika wavuni magoli 53 kwenye michezo 80 aliyoichezea timu hiyo.



,669,290

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/12/22 | 17:00 | Troyes vs Nantes | 2.34 | 3.48 | 2.78 |
| 02. 28/12/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Kasimpasa | 2.78 | 3.53 | 2.31 |
| 03. 28/12/22 | 22:00 | Portimonense vs Casa Pia Atletico | 2.36 | 3.14 | 2.99 |
| 04. 28/12/22 | 22:45 | St Johnstone vs Hearts | 2.85 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 28/12/22 | 22:45 | Livingston vs St Mirren | 2.32 | 3.38 | 2.88 |
| 06. 29/12/22 | 17:00 | Giresunspor vs Gaziantep BB | 2.47 | 3.34 | 2.69 |
| 07. 29/12/22 | 19:00 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.36 | 3.15 | 3.05 |
| 08. 29/12/22 | 21:15 | Betis vs Athletic Bilbao | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 29/12/22 | 22:00 | GD Estoril vs Boavista | 2.27 | 3.13 | 3.18 |
| 10. 29/12/22 | 22:45 | Blackburn vs Middlesbrough | 2.53 | 3.22 | 2.68 |
| 11. 29/12/22 | 22:45 | Wigan vs Sunderland | 2.69 | 3.19 | 2.54 |
| 12. 29/12/22 | 23:00 | Nice vs Lens | 3.14 | 2.89 | 2.43 |
| 13. 30/12/22 | 11:45 | Western United vs Brisbane Roar | 2.49 | 3.24 | 2.74 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 28/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:10 | 2456 | Alshoulla vs Al Jabalain | 2.57 | 2.81 | 2.81 |
| 15:25 | 1881 | AL Hazm vs AL Ain | 1.24 | 5.03 | 10.65 |
| 15:45 | 2680 | Enppi Club vs El Daklyeh | 2.27 | 3.08 | 3.23 |
| 16:00 | 3202 | JS Bordj Menaiel vs USM Annaba | 1.58 | 3.40 | 5.83 |
| 16:00 | 5919 | PWD Bamenda vs Cotonsport | 3.55 | 2.85 | 2.28 |
| 16:30 | 1704 | RC Arbaa vs CR Belouizdad | 3.35 | 3.15 | 2.21 |
| 17:00 | 1237 | ATK Mohun Bagan vs FC Goa | 2.32 | 3.46 | 2.63 |
| 17:00 | 2290 | AC Ajaccio vs Angers | 1.98 | 3.28 | 3.78 |
| 17:00 | 3102 | Istanbulspor vs Kasimpasa | 2.68 | 3.53 | 2.39 |
| 17:00 | 5097 | Troyes vs Nantes | 2.36 | 3.49 | 2.75 |
| 17:00 | 5560 | Alanyaspor vs Kayserispor | 2.09 | 3.59 | 3.14 |
| 17:35 | 5442 | Hajer Club vs Al Orubah | 2.33 | 2.90 | 3.40 |
| 18:00 | 2139 | Farco FC vs Coca Cola | 4.58 | 2.64 | 2.09 |
| 18:00 | 2394 | Talaea El Gaish vs Haras EL Hodood | 1.81 | 3.29 | 4.59 |
| 18:00 | 4808 | Levadiakos vs Ionikos Nikea FC | 2.26 | 3.04 | 3.29 |
| 18:00 | 5627 | Maghreb Tetouan vs Hassania Agadir | 3.16 | 2.77 | 2.36 |
| 19:00 | 1650 | US Biskra vs USM Alger | 2.31 | 2.78 | 3.26 |
| 19:00 | 3759 | AJ Auxerre vs Monaco | 4.18 | 3.83 | 1.74 |
| 19:00 | 4314 | Olympiakos vs Asteras Tripolis | 1.30 | 4.47 | 11.93 |
| 20:00 | 1395 | Porto B vs Sporting Farense | 2.61 | 3.20 | 2.56 |
| 20:00 | 2857 | Fatih Karagumruk vs Trabzonspor | 3.49 | 3.59 | 1.96 |
| 20:00 | 3617 | Ceramica Cleopatra vs Al Ahly Cairo | 5.59 | 3.94 | 1.56 |
| 20:15 | 3709 | Union Touarga vs CRS Salmi | 2.83 | 2.59 | 2.78 |
| 20:30 | 4676 | Volos vs AEK Athens | 6.96 | 3.83 | 1.49 |
| 21:00 | 1789 | Clermont Foot vs Lille | 4.17 | 3.67 | 1.78 |
| 21:00 | 4223 | Atromitos vs PAOK | 4.77 | 3.53 | 1.72 |
| 21:00 | 4321 | Faulkland SC vs Portmore United | 4.70 | 3.00 | 1.90 |
| 21:00 | 4510 | Dunbeholden FC vs Waterhouse FC | 3.10 | 2.90 | 2.49 |
| 22:00 | 5961 | Portimonense vs Casa Pia Atletico | 2.36 | 3.14 | 2.99 |
| 22:30 | 1647 | Panathinaikos vs OFI Crete | 1.31 | 4.68 | 9.96 |
| 22:30 | 4191 | Mouloudia Oujda vs Olympique Khouribga | 2.76 | 2.71 | 2.71 |
| 22:45 | 2322 | Livingston vs St Mirren | 2.42 | 3.24 | 2.84 |
| 22:45 | 4070 | Dundee Utd vs Ross County | 1.95 | 3.39 | 3.74 |
| 22:45 | 4487 | Rangers vs Motherwell | 1.22 | 6.18 | 10.97 |
| 22:45 | 4490 | St Johnstone vs Hearts | 3.02 | 3.27 | 2.28 |
| 22:45 | 5529 | Kilmarnock vs Aberdeen | 2.98 | 3.28 | 2.30 |
| 23:00 | 1088 | Humble Lions FC vs Tivoli Gardens | 2.26 | 2.88 | 3.22 |
| 23:00 | 1195 | Paris St Germain vs Strasbourg | 1.24 | 5.93 | 9.88 |
| 23:00 | 1936 | Brest vs Lyon | 3.54 | 3.59 | 1.95 |
| 23:00 | 2347 | Leeds vs Manchester City | 7.63 | 5.27 | 1.32 |
| 23:00 | 4038 | Hibernian vs Celtic | 6.77 | 4.88 | 1.38 |
| 23:15 | 1627 | Molynes vs Mount Pleasant FC | 6.42 | 3.79 | 1.47 |
| 23:15 | 5936 | Montego Bay Utd vs Chapelton Maroons FC | 1.99 | 3.30 | 3.75 |

ALHAMISI - 29/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 00:15 | 5263 | Porto vs FC Arouca | 1.12 | 7.56 | 18.90 |
| 19:00 | 1705 | Lorient vs Montpellier | 1.99 | 3.54 | 3.44 |
| 21:15 | 1693 | Betis vs Athletic Bilbao | 2.65 | 3.25 | 2.60 |
| 23:00 | 2168 | Nice vs Lens | 3.14 | 2.89 | 2.43 |
| 23:00 | 4541 | Marseille vs Toulouse | 1.50 | 4.39 | 5.59 |
| 23:30 | 2189 | Atletico Madrid vs Elche | 1.26 | 5.40 | 11.00 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MFAUME, PIALALI HAKUNA MSHINDI, KURUDIWA TENA

**Na Saada Akida**

PAMBANO la usiku wa mabingwa kati ya bondia, Mfaume Mfaume dhidi ya Idd Pialali lilishindwa kumalizika na kupata mshindi kama ilivyotarajiwa.

Kwa mujibu wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), pambano hilo lililokuwa la raundi 10 katika uzito wa Super Walter lilivunjika katika raundi ya kwanza kutokana na mabondia hao kugongana vichwa vilivyopelekea Pialali kupasuka usoni.

Hata hivyo, promota amepewa nafasi ya kuandaa pambano lingine kwa sababu pambano la juzi lililofanyika jijini Arusha halikupata mshindi.

Katibu Mkuu wa TPBRC, Yahaya Poli, alitangaza pambano hilo halina mshindi baada ya kujiridhisha wazi mabondia hao wote waligongana vichwa na kuamua kulivunja pambano.

Pialali alisema tukio lililotokea katika pambano hilo halikuwa matarajio yake huku akisisitiza atakuwa tayari kwa ajili ya pambano la marudiano.

Naye Mfaume alisema matokeo yalitokea siyo jambo alilolitarajia na anajipanga kwa ajili ya kukutana na mabondia kutoka nje ya nchi.

Mabondia wengine walifanikiwa kushinda katika pambano hilo la Usiku wa Mabingwa ni Karim Mandonga aliyemchapa Alibaba Tarimo wakati Hassan Ndonga akimdunda kwa KO ya raundi ya kwanza, Yamikani Mkandawire huku Shabani Ndaro wa Arusha akimtuliza Shabani Kaoneka kwa pointi.

Halima Vunjabei yeye alimtwanga kwa TKO Zawadi Kutaka wakati Yohana alimchapa Yamikani Mkandawire kutoka Malawi na Osama Allabi akimchakaza Salim Omary kwa pointi.




Bondia Karim Mandonga (kushoto), akipigana na Ally Baba katika pambano la Usiku wa Mabingwa lililofanyika jijini Arusha juzi usiku. Mandonga aliibuka mshindi katika pambano hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## HATIMAYE FEITOTO

INATOKA UK. 32

malengo yetu ingawa hatuwezi kuwabeza wapinzani wetu.

Mbio za kulisaka taji la Ligi Kuu Bara mara nyingi zimekuwa ngumu hasa mzunguko wa pili, unapopoteza mchezo unajiweka kwenye mazingira magumu zaidi ya kutimiza malengo, tunatambua hilo na ndio maana tunaweka nguvu kubwa," alisema Nabi.

Aliongeza licha ya kuongoza katika msimamo wa ligi kwa tofauti ya pointi sita dhidi ya timu inayowafuatia, hali hiyo haiwafanyi wabweteke.

"Tunahitaji kushinda na kusonga mbele bila kujali wigo pointi tulionao dhidi ya wanaotufuatia katika msimamo, tunataka kukaa mahali salama mpaka mwisho wa msimu," aliongeza kocha huyo.

Ligi Kuu inatarajia kuendelea tena keshokutwa kwa Singida Big Stars kuwakaribisha Geita Gold FC na Tanzania Prisons kuwafuata Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Simba yaamsha

INATOKA UK. 32

watakwenda naye Zanzibar kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Aliongeza Simba inatarajia kuendelea kufanya usajili wa kishindo kwa kunasa nyota wapya na wachezaji wa zamani ambao bado inawahitaji kuwaongezea mikataba.

"Naendelea vizuri, huu ni mpira nafikiri nitajiunga na wenzangu mapema, kwa sasa siwezi kusema kitu chochote mpaka nitakapopona," Phiri, straika huyo ambaye ana mabao 10 mpaka sasa alisema.

Katika hatua nyingine, mchezaji mpya wa timu hiyo aliyejiunga nayo hivi karibuni akitokea Geita Gold, Mrundi Saido Ntibazonkiza amewaomba wanachana na mashabiki wa timu hiyo kumpa sapoti ili afanye vyema.

Michezo
Jumatano Desemba 28, 2022
Nipashe




## Gakpo, Liverpool sasa kimeeleweka

ROHO ZA YANGA



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele (kushoto), akiwa na kiungo mshambuliaji, Feisal Salum 'Feitoto' katika moja ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu. **PICHA: MTANDAO**

# HATIMAYE FEITOTO KUBAKIA JANGWANI

●●●Mazungumzo yafikia pazuri, sasa kulipwa mshahara mnono pamoja...

**Na Saada Akida**

KIUNGO mshambuliaji, Feisal Salum 'Feitoto' ambaye alitangaza kuvunja mkataba na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, ataendelea kubakia katika mitaa ya Twiga na Jangwani baada ya pande mbili hizo kufikia makubaliano, imefahamika.

Feitoto alivunja mkataba wake na Yanga kwa kuilipa klabu hiyo kiasi cha Sh. milioni 112 kama matakwa ya mkataba wake uliokuwa unatarajiwa kumalizika ifikapo mwaka 2024 huku tetesi zikidai nyota huyo anaelekea Azam FC.

Taarifa zilizopatikana jijini Dar es Salaam zinasema Feitoto na Yanga wamefikia hatua nzuri ya mazungumzo ambayo yatapelekea kuboresha mkataba wa nyota huyo kutoka Zanzibar ili aendelee kuvaa jezi za rangi ya kijani na njano.

Chanzo hicho kiliendelea kusema vigogo mbalimbali wamehusishwa katika kufanikisha makubaliano hayo na wanaamini kila kitu kitakwenda vizuri na kuwatuliza mashabiki na wanachama wa klabu hiyo.

"Feisal ni mchezaji wa Yanga, bado ana mkataba na sisi bado tunamhitaji kutokana na malengo yetu tuliyonayo katika mashindano ya ndani na ya kimataifa, hivyo si rahisi kumwacha aondoke.

Naamini hili linaenda kuisha na mchezaji anarudi kambini kuungana na wachezaji wenzake kwa ajili ya kuipigania timu, nawahakikishia Feisal ataendelea kuichezea Yanga, tunaenda kumboreshea stahiki zake," alisema kiongozi huyo ambaye hakutaka kuweka wazi jina lake.

Akizungumza na gazeti hili, Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji, alisema mara nyingi vita ya usajili huwa ni kubwa na kila timu inahitaji kupata mchezaji aliye katika ubora wa hali ya juu.

Haji alisema Feisal kuhusishwa na klabu nyingine si jambo jipya kwa sababu hali hiyo hutokea kwa wachezaji wazuri sehemu mbalimbali hapa duniani kwa timu kutafuta wachezaji ambao wataingia kwenye kikosi cha kwanza moja kwa moja.

"Najua hii ni vita ya ubingwa hivyo tumegundua wapinzani wanataka kuleta chokochoko ili kutuondoa kwenye malengo yetu, tumegundua hilo na tuko imara hakuna mchezaji tuliye na malengo naye ataondoka katika dirisha hili la usajili," alisema Haji.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, alisema baada ya mapumziko ya siku moja sasa akili na nguvu wanazihamishia katika mchezo wao unaofuata wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar utakaochezwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Manungu Complex ulioko, Turiani mkoani Morogoro.

Nabi alisema wanahitaji kuendeleza kasi ya ushindi na kuwapa furaha mashabiki wao katika kipindi hiki cha sikukuu.

"Bado tuna kazi ya kufanya kuhakikisha tunatetea ubingwa wetu, wachezaji wanapaswa kujitoa kwa nguvu zote katika kila mechi iliyoko mbele yetu ili tutimize

INAENDELEA UK. 31

## Simba yaamsha vita ya ubingwa

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi, Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amesema bado timu yake iko katika mbio za kupigania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Mgunda alisema wataendelea kupambana kusaka ushindi na kuongeza michezo 12 iliyobakia katika ligi hiyo kwa kila timu ndio itakayoamua.

Mgunda hakatishwi tamaa na tofauti ya pointi walizonazo na vinara wa ligi hiyo, Yanga kwa sababu bado safari iliyoko mbele ni ndefu.

"Tulikuja kusaka pointi tisa, tumepata saba, tunashukuru kwa sababu kama hukushukuru kwa kidogo, huwezi kushukuru kwa kikubwa. Tumeyafanyia kazi mapungufu yaliyoonekana katika mechi dhidi ya Kagera Sugar ambayo ilisababisha tutoke sare, KMC sio timu ya kubeza, ni moja kati ya timu nzuri kwenye Ligi Kuu na ina mwalimu mzuri kwa hiyo huwezi kwenda kucheza nao unawadharau.

"Kazi iliyobaki mbele yetu ni kuhakikisha tunapata ushindi katika kila mechi inayokuja, bado tuko kwenye njia ya ubingwa, haiishi mpaka iishe," alisema kocha huyo.

Naye Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliwapiga dongo Azam FC ambao wametangaza rasmi kujiondoa kwenye mbio za ubingwa akisema siku zote ngoma ya kitoto haikeshi.

"Tumemaliza ziara yetu Kanda ya Ziwa, tumepata pointi sita CCM Kirumba Mwanza na pointi moja Uwanja wa Kaitaba, japo hatukufanikiwa kwa asilimia 100, malengo ilikuwa ni kurudi na pointi tisa, lakini tumerudi na saba tunashukuru hata kwa hiki tulichokipata, vita inaendelea, tunaendelea kupambana," alisema Ahmed.

Aliongeza bado wana nafasi kubwa ya kupata ubingwa kupitia mechi 12 za ligi hiyo zilizobakia.

"Nimeona Azam wao wamejitoa kwenye mbio za ubingwa, ni kawaida, siku zote ngoma ya mtoto haikeshi, sisi hatujakata tamaa hadi mwisho, hizi mechi zilizosalia chochote kinaweza kutokea," Ahmed alisema.

Kuhusu straika, Mosses Phiri, alisema atakosa mechi ijayo dhidi ya Prisons itakayochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na baada ya hapo

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042